UDHANAISHI KATIKA RIWAYA ZA THOMAS KAMUGISHA: *KITU KIDOGO TU!* NA *HARUSI YA WENDAWAZIMU*

ABDALLAH MZUNGU CHIMERAH

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA KUHITIMU SHAHADA YA UZAMILI KATIKA LUGHA YA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA PWANI

MEI, 2021

UNGAMO NA IDHINI

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe wala haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada nyingine yoyote katika Chuo Kikuu chochote.

Sahihi… …… Tarehe: 11/04/2022

Abdallah Mzungu Chimerah

AG23/PU/36309/17

IDHINI

Tunathibitisha kuwa tasnifu hii ya shahada ya uzamili ilifanywa na mtahiniwa chini ya usimamizi wetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Pwani.

Hakuna sehemu ya tasnifu hii ambayo itatolewa kwa namna yoyote ile bila kibali kutoka kwa mwandishi na Chuo Kikuu cha Pwani.

Prof. Jonathan Furaha Chai

Sahihi…… …… Tarehe: 11/04/2022

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi, Chuo Kikuu cha Pwani

Dr. Rukiya Harith Swaleh

Sahihi…  …… Tarehe: 11/04/2022

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi, Chuo Kikuu cha Pwani

TABARUKU

Kwa babangu, Shebani Chimerah aliyehakikisha tunasoma kabla hatujalala. Pia, babangu mkubwa, Prof. Chimerah na Zahra Abdillahi walionishajiisha masomoni. Hatimaye, mwanangu Shaaban aliyetujia kazi hii ikimalizika.

SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu, aliyenijaalia uhai, ulionipa fursa ya kupanga na kutimiza malengo yangu, si ujanja wangu hata kidogo.

Pili, nawashukuru wasimamizi wangu Prof. Furaha Chai na Dkt. Rukiya Harith kwa kuniongoza katika kila hatua ya utafiti. Aidha nawashukuru wahadhiri wangu Prof. Rocha Chimerah na Dkt. Nancy Ngowa kwa shime yao katika safari hii. Nisimsahau Prof. Kahigi.

Pia nawashukuru babangu Mzee Shebani Chimerah, mamangu Amina Mgalla, babangu mdogo Mashudi, mama wadogo Chidodo na Mumbi, mama wakubwa Emma, Nyiramafaranga na Tabu, halati zangu Mwaka na Mwanakombo Mgalla, mjombangu Omar Farah, shangazi Spoti, rafiki yangu Roshni, ndugu zangu, Ramadhan, Athman, Fatuma na Abdallah (daktari), wote walijitolea kwa hali na mali kuhakikisha nimefika nilipofikia. Nisimsahau mke wangu Fatma Mwinyi, alipoolewa hakujua fungate ila kunitunza wakati nikifanya utafiti.

Mwisho, rafiki zangu Khalfan (Ustadh Ndevumbili) na Zahra tuliokutana tangu shahada ya kwanza tukawa zaidi ya ndugu. Aidha, wanafunzi wenzangu, Nyong’o, Hussein, Waliaula, Mathias na Gladys.

IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza udhanaishi katika matendo na maneno ya wahusika katika riwaya mbili za Thomas A. R. Kamugisha; *Kitu Kidogo Tu!* na *Harusi ya Wendawazimu.* Hivyo, madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuchunguza matendo na maneno ya wahusika ili kudhihirisha vipengele vya kidhanaishi vinavyojitokeza.

Utafiti huu umegawanywa katika sura tano; ya kwanza ni utangulizi yenye usuli wa mada, swala la utafiti, malengo ya utafiti, natija ya utafiti, upeo na mipaka ya utafiti na ufafanuzi wa istilahi na vifupisho. Sura ya pili imeeleza tafiti mbalimbali tangulizi za kuhusu udhanaishi na pia nadharia ya udhanaishi imefafanuliwa. Sura ya tatu imeeleza utaratibu wa utafiti, mbinu na vifaa vilivyotumiwa kukusanyia data na jinsi data hiyo ilivyochanganuliwa. Katika sura ya nne data iliyokusanywa imechanganuliwa. Sura ya tano imebeba muhtasari wa utafiti, hitimisho, mapendekezo kwa watafiti wengine na marejeleo. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni ya udhanaishi inayohusishwa na wanafalsafa kama Soren Kierkegaard (1813-1855), Jean Paul Sartre (1905-1980), Friedrich Nietzsche (1844-1900). Udhanaishi ni falsafa inayoshugulikia maswala kuhusu maisha; ni mtazamo unaokagua kwa upembuzi hali ya nafasi ya mtu katika ulimwengu anamoishi.

Mtafiti amegundua kuwa riwaya hizi mbili za Kamugisha ni za kidhanaishi kutokana na matendo na kauli za wahusika wake. Vipengele vya kidhanaishi kama utamaushi, ukengeushi, swala la uwepo wa Mungu, uhuru wa mtu binafsi na kuabudu mahitaji ya kimwili vimejitokeza. Data ilichanganuliwa kwa njia ya kithamano na matokeo kuwasilishwa kwa maelezo ya kinathari. Utafiti ulikuwa wa maktabani.

YALIYOMO

Ungamo na idhini……..……..……...ii

Tabaruku……...iii

Shukrani……..….....iv

Ikisiri……..……v

Yaliyomo……..…..……vi

Orodha ya majedwali……..……x

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI…….……..1

1.1 Usuli wa mada…….…….……1

1.1.1. Kumhusu mwandishi Thomas Kamugisha…….7

1.2. Swala la utafiti…….……8

1.3. Malengo ya utafiti……..…….9

1.4. Maswali ya utafiti…….....9

1.5. Natija ya utafiti……..10

1.6. Upeo na mipaka ya utafiti…….……..……..11

1.7. Ufafanuzi wa istilahi na vifupisho…….……13

SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO NA MSINGI WA NADHARIA….....15

2.1 Kitangulizi…….…….....15

2.2 Yaliyoandikwa kuhusu udhanaishi……..……..15

2.2.1. Mapitio yanayohusu tafiti na kazi nyingine katika fasihi kwa upande wa mbinu na matokeo…….……...15

2.2.2. Maandishi mbalimbali kuhusu nadharia ya udhanaishi ……..21

2.3 Msingi wa nadharia…….…….……25

2.3.1 Mihimili ya udhanaishi……27

2.4. Kihitimisho…….……...30

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI……31

3.1 Kitangulizi…….…….31

3.2 Aina ya utafiti…….….…….……..31

3.3 Muundo wa utafiti……..31

3.4 Uteuzi wa sampuli…….…….31

3.5 Data ya utafiti…….32

3.6 Mbinu za kukusanya data……...33

3.7 Vifaa vya kukusanyia data…….……33

3.8 Uchanganuzi wa data…….…….34

3.9 Uwasilishaji wa data……...36

3.10 Uaminiki na utegemewaji wa utafiti……36

3.11 Maadili ya utafiti…….…….36

3.12 Kihitimisho…….……..37

SURA YA NNE: UWASILISHI NA UCHANGANUZI WA DATA…….38

4.1 Kitangulizi…….…….38

4.2 **Uhuru wa mtu binafsi**…….…….38

4.2.1 Zamda apigania uhuru wa kujiamulia…….….……...39

4.2.2 Maimuna (shangazi la Zamda na Yasmin) atetea uhuru wa vijana kujiamulia…...44

4.2.3 Mariam- mwanafunzi wa Buda abadili maumbile yake……..45

4.2.4 Msichana wa gauni la rangi ya bahari anakataa ndoa…….……46

4.2.5 Chris haiheshimu ndoa yake…….…….....47

4.2.6 Musa Nshomile analaani dini kwa kumnyima uhuru……...…….……..48

4.3 Swala la Mungu…….….…….……48

4.3.1 Mzee (kwenye basi la kwenda Bukoba) amkana Mungu …….…….....50

4.3.2 Katoto wa Minane anakufa bila dini……...52

4.3.3 Mwalimu Tadeo na imani yake thabiti ya ulokole……..53

4.3.4 Mwalimu Martin anaishi kwa kudura…….55

4.3.5 Musa Nshomile anarudisha imani kwa Mungu……..…….56

4.3.6 Stella Tadeo na imani thabiti ya ulokole…….....58

4.4 Kifo……..……...59

4.4.1 Wazazi wa Musa Nshomile na ndugu zake wanaangamizwa na malale…….60

4.4.2 Maburuki na watuhumiwa wengine wanaangamia rumande ……61

4.4.3 Famila ya Garincha kijijini Kakonko yaangamizwa na kipindupindu……61

4.4.4 Zainab afariki dunia…….……...62

4.5 Ukengeushi…….……..……63

4.5.1 Musa Nshomile anakengeuka kitabia …….…….....64

4.5.2 Maimuna anakengeuka na mila za ndoa…….…….....66

4.5.3 Mwalimu Tadeo amruhusu bintiye kulala chumba kimoja na Musa…….…….67

4.5.4 Kachala Domokaya anakengeuka na useminari…….…….68

4.5.5 Garincha hajali wazee……..……..…....69

4.5.6 Chris (Christopher Mbwana) anafanya kinyume na ubatizo…….….....72

4.5.7 Zamda na Yasmin wanakengeuka kidini na kimaadili..…… ….....73

4.5.8 Eliza anajichanganya na wachumba wawili…….……...76

4.5.9 Vijana katika mkesha wa harusi wamekengeuka kimaadili……77

4.5.10 Saad Mwendawazimu anakengeuka na dini……..……78

4.5.11 Buda anakengeuka kimaadili…….…….....79

4.6 Utamaushi…….……82

4.6.1 Katoto wa Minane anatamauka na kujiua…….....83

4.6.2 Mahabusu anatamauka na kujiua…….……...85

4.6.3 Abdu anatamauka baada ya kukaa rumande kwa miaka…….87

4.7 Kuabudu mahitaji ya kimwili…….……88

4.7.1 Musa Nshomile anaishi na Irene bila ndoa…….....90

4.7.2 Eliza ashiriki mapenzi na wanaume watatu……91

4.7.2.1 Eliza na Garincha…….……..…..91

4.7.2.2 Eliza na Chris……...92

4.7.2.3 Eliza na Jim Kichaa…….…….94

4.7.3 Garincha asaliti uchumba kwa kuwa na Fay Parker……95

4.7.4 Chris ashiriki mapenzi na wanawake watatu…….…….96

4.7.5 Mariam (mke wa Musa) amsaliti mumewe, na dini yake……...96

4.7.6 Chris na Garincha wanastarehe na wanawake……98

4.7.7 Nora (mama huruma) na ngono za kiholela ……..…….....99

4.7.7.1 Nora na Garincha…….…….....99

4.7.7.2 Nora na Buda…….…….…….....100

4.7.8 Mama John (mke wa Buda) anavunja ndoa yake kwa uasherati…….....102

4.7.9 Eva auza mwili kujikimu……...103

4.7.10 Kachala msimulizi wa kisa ananunua ngono……..103

4.8 Utupu wa maisha/ ombwe/ ubatili……104

4.8.1 Musa Nshomile anashindwa kuyapa maisha yake maana (anatoweka)……104

4.8.2 Isaya Omulangi anahubiri uduni wa binadamu…….....107

4.9. Kihitimisho…….111

SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO……..112

5.1 Kitangulizi……112

5.2 Muhtasari……..…112

5.3 Hitimisho……..116

5.4 Mapendekezo…….....117

MAREJELEO……..….119

VIAMBATISHO…….……..126

Cheti cha maadili……....126

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 3.1: Mfano mwafaka wa uchanganuzi wa data……...35

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa mada

Riwaya imefafanuliwa na wataalamu mbalimbali kuwa ni kisa kirefu cha kubuni kilichoandikwa kwa lugha nathari na kuchapishwa kama kitabu. Khamis (1983), anaeleza kuwa riwaya ni sanaa ya nathari inayoelezea kwa mtiririko, hadithi, kwa njia ya matukio na vitukio vinavyojiri katika muungano wa wakati. Tofauti na ushairi au hata tamthilia, ina upana na urefu wa mwandishi kujifaragua, hasa katika majitapo ya wahusika, nafasi ya mazingira na urefu wa wakati. Kulingana na maelezo haya, tunaona kuwa riwaya inampa mwandishi nafasi ya kusimulia mambo mengi kadri awezavyo bila kufungika katika ufinyu wa wakati au maudhui.

Naye Njogu na Chimerah (1999) wanaifafanua riwaya kuwa ni utungo mrefu wa kubuni, na wenye ploti, uliotumia lugha ya nathari. Riwaya ni hadithi ndefu ambayo ina visa na vitushi, migogoro na inayosimulia mambo yanayohusiana na jamii. Njogu na Chimerah (keshatajwa) wanaongeza kipengele cha jamii katika ufafanuzi wao. Ni bayana kuwa kazi yoyote ya fasihi lazima ijikite kimaudhui katika migogoro ya jamii inamotungiwa. Fasihi ni kioo cha jamii, hivyo basi kazi ya fasihi lazima imulike jamii inamotokea, kwa uzuri na ubaya wake, ili jamii yenyewe inapotazama kioo hiki iweze kutambua ni wapi palipo na tatizo panapohitaji kurekebishwa. Hivyo, riwaya hutoa nafasi nzuri kwa mwandishi kuisawiri jamii kinagaubaga kwa kutompimia wakati au nafasi.

Kihistoria, riwaya ni utanzu wa juzi zaidi ukilinganishwa na tanzu nyingine za fasihi kama tamthilia na ushairi. Kulingana na Margaret Doody (1996), chimbuko la riwaya linahusishwa na fasihi ya Wagiriki na Warumi inayopata takriban miaka elfu mbili iliyopita. Hata hivyo, wataalamu wengi wanakubaliana kuwa riwaya ya kwanza kabisa kuandikwa ni *Tale of Genji (1010)* iliyoandikwa na mwanamke wa Kijapani kwa jina la

Murasaki Shikibu. Ukilinganisha tarehe hii na karne ya 10 ambayo inakisiwa kuwa mtunzi mashuhuri wa nyimbo na mashairi ya Kiswahili Fumo Liyongo aliishi na kutunga nyimbo na mashairi yake, ni bayana kuwa utanzu huu wa riwaya ni wa juzi.

Huko Ulaya, inasemekana miongoni mwa riwaya za kwanza zaidi ni riwaya iliyoitwa *Hayy ibn Yaqdhan* iliyoandikwa na Abu Bakr ibn Tufayl kwa lugha ya Kiarabu huko Andalusia mwanzoni mwa karne ya kumi na mbili. Tafsiri ya riwaya hii kwa Kiingereza iliathiri baadhi ya waandishi wa awali kama Daniel Defore aliyeandika *Robinson Crusoe (1719).*

Utanzu huu wa riwaya ulianza kukita mizizi huko magharibi katika karne ya 19 kulipokuwa na mapinduzi ya viwanda. Mapinduzi haya yalifanya kuandika na kuchapisha kazi za riwaya kuwa rahisi hivyo waandishi wakaanza kuongezeka.

Kulingana na Chiraghdin na Mnyampala (1978), katika karne ya 19 wageni mbalimbali kutoka huko Ulaya walitembelea Afrika Mashariki kama watalii, wanabiashara na wamishenari. Wamishenari hawa wakawa na mchango mkubwa katika kuendeleza uandishi wa kazi za Kiswahili. Ohly (1981) anaeleza kuwa Dkt. Steere alianza kukusanya na kuhariri ngano kutoka kwa wakazi wa Zanzibar mwaka wa 1870. Mbali na kukusanya ngano hizi za Kiswahili, wamishenari hawa walianza kutafsiri maandishi mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili na kulingana na Njogu na Chimerah (1999) tafsiri hizi ndizo zilizokuwa msingi wa riwaya ya Kiswahili.

Miongoni mwa kazi hizo zilizotafsiriwa ni *Mazungumzo ya Alfu-Lela Ulela* (Juzuu 1-4) (1928) - kilichotafsiriwa na Edwin Brenn na kuhariririrwa na F. Johnson. Riwaya kadhaa za kimagharibi kama vile *Mashimo ya Mfalme Suleiman*- Rider Haggard; *Kisima Chenye Hazina* – R. L. Stevenson; *Mashujaa* – Charles Kingsley; Safari *za Guliva* –

Jonathan Swift; *Hadithi za Esopo*- B.S Mang'anda, na nyengine za mashariki kama *Hekaya za Abunuwasi na Hadithi Nyingine* pia zilitafsiriwa.

Baada ya wamishenari hawa kutamalaki, mwishoni mwa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20 wakoloni wakaingia na kutawala Afrika. Kulingana na Njogu na Chimerah (1999), ukoloni huu ndio ulioibusha riwaya ya Kiswahili. Kwa hivyo, historia ya riwaya ya Kiswahili inafungamana na historia ya maendeleo ya jamii za Afrika ya Mashariki. Hii ina maana kwamba, mtu anapotaka kueleza juu ya chimbuko la riwaya ya Kiswahili basi anapaswa kutazama maendeleo ya jamii ya Waswahili (watu wa Afrika Mashariki) katika vipindi mbalimbali vya maendeleo yake kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni.

Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa polepole pakaanza kuibuka maandishi ya nathari yaliyotokana na Waafrika wenyewe. Kwa mfano, kitabu cha *Uhuru wa Watumwa* (1934), kilichoandikwa na James Mbotela, ni usimulizi wa kinathari unaoshughulikia uhusiano baina ya mataifa ya kimagharibi na ya Kiafrika. Na kadri ya uwanda ulivyozidi kupanuka, ndivyo waandishi walivyopata ujasiri wa kujaribu maudhui mbalimbali kama ya upelelezi ambayo yalikuwa hayajashughulikiwa kabisa. Mfano wa hali hii ni riwaya za Muhammed Said Abdulla, kama vile *Mzimu wa Watu wa Kale* (1960), *Siri ya Sifuri* (1974), na *Kisima cha Giningi* (1968).

Ijapokuwa riwaya za awali zilihusu zaidi maadili na masuala ya kidini kama katika *Adili na Nduguze* (1952); *Nakupenda lakini* (1968), *Kurwa na Doto* (1966); *Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi* (1971), pia mvutano uliokuwepo baina ya wakoloni na Waafrika ulikuwa wadhihirishwa katika baadhi ya riwaya za awali. Aidha, maandishi mengine ya fasihi yalihusu matarajio ya jamii itakikanayo baada ya ukoloni, kama katika *Siku ya Watenzi Wote* (1968), *Kufikirika* (1968) na *Kusadikika* (1991).

Njogu na Chimerah (1999) wanasema ni bayana kwamba baada ya 1970, riwaya nyingi zilianza kujihusisha na uongozi na usaliti wa kisiasa; na hapo ndipo riwaya ya kisasa ya Kiswahili inapoweza kusemekana imeibukia. Wasanii waliweza kutazama nyuma na kuona miaka kumi ya uhuru, na namna miaka hiyo ilivyofungua njia za ulundikaji mali miongoni mwa wachache, huku kukiwepo ukandamizwaji wa wengi. Uhuru wa kisiasa uliwapa wasanii maudhui tofauti ya kushughulikia, kama vile unafiki, ukoloni mamboleo, ufisadi, usaliti wa umma, ujamaa kama mfumo wa siasa, na utawala wa kiimla.

Miongoni mwa maudhui haya mapya yaliyoshughulikiwa na waandishi wa baada ya uhuru katika fasihi ya Kiswahili ni maudhui ya udhanaishi. Udhanaishi ni falsafa iliyopata mashiko sana katika nchi za magharibi katika kipindi cha vita vikuu vya dunia na hata baada yake. Katika kipindi hiki maisha yalionekana kukosa maana kabisa kwa mateso kushamiri. Kwanza binadamu waliuwana wenyewe kwa mamilioni. Chumi mbalimbali zikaporomoka na kuwafanya wananchi wateseke sana. Maadili ya jamii mbalimbali pia yakavurugika. Katika hali hii ya mateso na ya kutamausha, baadhi ya wanafalsafa kama Martin Heidegger, Jean-Paul Sartre, na Albert Camus wakawa miongoni mwa wataalam wa mapema kushughulikia udhanaishi katika maandishi yao mbalimbali (Bennett, 2011).

Baada ya ukoloni, Afrika Mashariki pia ilijikuta katika kipindi cha kutamausha na chumi kuzorota kwa sababu ya uongozi mbaya na usaliti wa kisiasa. Hali hii iliibua waandishi wa kidhanaishi katika fasihi ya Kiswahili, ambao kama wenzao wa kule Ulaya walijikuta wakiuliza swali lile lile maarufu kwa wadhanaishi wote- maisha yana maana gani?

Kulingana na Poyi (2021), Euphrase Kezilahabi ndiye mwandishi maarufu wa kidhanaishi katika fasihi ya Kiswahili kutokana na kazi zake katika tanzu zote za fasihi.

Baadhi ya kazi hizi ni *Rosa Mistika* (1971), *Kichwamaji* (1974b), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), *Gamba la Nyoka* (1979), *Nagona* (1990), na *Mzingile* (1991) ambazo ni riwaya. Tamthlia ya *Kaptula la Umarx* (1999) na diwani za mashairi za *Kichomi* (1974), *Karibu Ndani* (1988) na *Dhifa* (2008).

Rettová (2016), anaongeza waandishi wafuatao miongoni mwa waandishi wa kidhanaishi katika fasihi ya Kiswahili: Abdilatif Abdalla- *Sauti ya Dhiki* (1973), William Mkufya- *Ua la Faraja* (2004), Mohamed Suleiman- *Kiu* (1972) na *Nyota ya Rehema* (1976) na Claude G. Mung'ong'o- *Njozi Iliyopotea* (1980).

Hawa ni baadhi tu ya wataalamu ambao kama wataalamu wengine wengi wanaochambua kazi za fasihi ya Kiswahili kwa misingi ya kidhanaishi, wanashindwa kuzitambua riwaya hizi za Thomas Kamugisha: *Kitu Kidogo Tu!* na *Harusi ya Wendawazimu* kuwa ni riwaya za kidhanaishi mbali na kuwa zimesheheni sifa zote za udhanaishi. Maudhui kama ya ufisadi na usaliti wa umma kisiasa ndiyo yanayotawala hasa katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* (2000). Kutoka mwanzo, mwandishi anaonyesha jinsi nchi ilivyoporomoka kiuchumi na kimaadili baada ya kupata uhuru. Katika riwaya hii, mwandishi amesawiri vizuri shida zote wanazopitia wananchi kwa serikali yao kufeli kuendesha nchi. Usafiri umezorota, bidhaa hazipatikani madukani, mishahara hailipwi kwa wafanyakazi wa serikali kama walimu, shule zinaanguka, hakuna dawa zahanatini na zile chache zinazopatikana zinafichwa zikiuzwa na wauguzi, wananchi wanashikwa na kufungwa bila kuhukumiwa kisheria. Mwandishi anasawiri wahusika wake katika hali ya mateso na matatizo mengi. Kwa matatizo haya, wahusika wengine wanatamauka na kuamua kujitoa uhai.

Katika riwaya ya *Harusi ya Wendawazimu* (1980) vilevile, mwandishi ameonyesha jinsi vijana walivyokengeuka. Vijana wanasawiriwa wakipuuza masharti na kaida zinazofungamana na ndoa na kuifanya iwe taasisi ya kuheshimika katika jamii za

Kiafrika. Msichana kuchumbiwa na vijana wawili wakati mmoja ni mfano tu wa jinsi vijana walivyokengeuka kutoka kwa maadili ya jamii za Kiafrika. Vijana wanapigana kukata mikatale ya kitamaduni na kujitafutia uhuru wao. Jambo ambalo linasababisha migoro kati yao na wazee wao.

Kukengeuka, kukata tamaa na kujitoa uhai ni miongoni mwa mihimili ya udhanaishi. Udhanaishi ni falsafa inayojaribu kuonyesha matatizo wanayopitia binadamu katika maisha yao. Unamsawiri binadamu katika upweke wake na jinsi anavyoishi na kufanya maamuzi yanayoathiri maisha yake. Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa wadhanaishi wengi hutilia mkazo mateso yanayomkumba binadamu. Maudhui wanayoyashughulikia ni kama vile kifo, uhuru wa mtu binafsi, wajibu wa binadamu duniani, ubinafsi, kukata tamaa, na udhaifu wa kibinadamu.

Vilevile, udhanaishi ni falsafa inayokwepa imani ya kijonzi juu ya maana ya kuishi na kutilia mkazo matatizo halisi yanayomsibu binadamu. Hujadili hali kama vile kihoro, ufupi wa maisha, fadhaa, mashaka, pekecho, utupu wa maisha na uchovu na jinsi zinavyoathiri maisha ya binadamu. Jazanda zinazoashiria kiungulia, uchovu, pekecho na kiwewe zinatumika kusawiria hali ya binadamu.

Aidha, udhanaishi ni falsafa inayoshikilia kuwa ukengeushi huanza pale mtu anapojaribu kufikiria kibinafsi na kutenda kinyume na kaida na miiko iliyozoeleka katika jamii. Katika kutafuta uhuru wake wa mawazo na matendo, binadamu anakengeushwa na Mungu, jamaa au familia yake, asili yake na yeye mwenyewe.

Hizi zote ni sifa zinazopatikana katika riwaya hizi. Mwandishi amejaribu kusawiri wahusika wanaopitia matatizo mengi, wanaokengeuka, wanaotamauka na wanaojitoa uhai kwa ugumu wa maisha. Kutokana na kusheheni huku kwa sifa za kidhanaishi katika riwaya hizi mbili, na uchache au hata ukosefu wa tafiti zinachanganua udhanaishi katika

riwaya hizi, Mtafiti aliona kuwa udhanaishi ni nadharia mwafaka kuchambulia riwaya hizi na kuziweka katika tapo la riwaya za kidhanaishi.

1.1.1 Kumhusu mwandishi Thomas Kamugisha

Thomas Kamugisha alizaliwa mwaka wa 1941 kijijini Kabale wilaya ya Muleba mkoani Kagera nchini Tanzania. Alisoma katika shule ya msingi ya Kabale kabla ya kujiunga na shule ya upili ya Rubya na kisha kumalizia katika shule ya upili ya Pugu.

Mwaka wa 1967 alijiunga na Chuo cha Oxford huko Uingereza alikofanya *Special Diploma in Social studies.* Baadaye mwaka wa 1981 aliendeleza masomo yake katika Chuo Kikuu cha Dar es Salam alikofuzu na shahada ya sanaa.

Baada ya masomo yake, Kamugisha alifanya kazi kama mwandishi katika shirika la uchapishaji la Tanzania Publisher House (TPH). Katika hii kazi yake alijishughulisha na shughuli mbalimbali zihusuzo uandishi kwa jumla. Alikuwa katibu mtendaji wa *Publishers Association of Tanzania* (PATA). Alishiriki kikamilifu katika mwamko uliokuwapo katika sekta ya uandishi, uchapishaji na usambazaji wa vitabu mwaka wa 1989 hadi 2008. Mwamko huu ulishirikisha waandishi, wachapaji na wasambazaji. Aidha, alikuwa mratibu wa *The Network of Technical Publications in Africa* (TEPUSA) kutoka mwaka wa 1987 hadi 1994. Aliweza kuandika riwaya tatu; *Harusi ya Wendawazimu* (1980), *Kitu Kidogo Tu!* (2000) na *Safari ya Mwalimu Katoto* (2004). Mbali na kazi yake ya uandishi Kamugisha aidha alijihusisha na ukulima wa kiwango kidogo.

Katika maandishi yake Kamugisha anayazungumzia maisha namna yalivyo. Anajishughulisha sana na jamii; jinsi watu wanavyoishi katika jamii, namna jamii inavyobadilika kutokana na usasa ulioathiriwa na umagharibi. Aidha, anasawiri namna serikali ilivyofeli katika kutimiza ahadi na majukumu yake kwa wananchi na

anaonyesha kufeli huku kwa serikali kwa kuangazia athari zake kwa wananchi wa kawaida na namna wanavyoendelea na maisha yao. Tunaweza kusema kuwa katika maandishi yake Kamugisha amejihusisha sana na maisha ya jamii kwa jumla na jinsi hali mbalimbali zikiwemo siasa za serikali, elimu mtu anayojipatia na usasa zinavyoathiri maisha ya kila siku ya jamii ya Tanzania.

Kutokana na uandishi wake, tunaweza kusema kuwa Kamugisha aliegemea falsafa ya kisosholojia kwa jinsi alivyoshughulikia maswala ya jamii na tabia tofauti za wanajamii na jinsi watu tofauti wanavyokabili hali tofauti katika jamii. Anaiangazia jamii kwa jicho la upembuzi. Ni wazi kwamba masomo yake ya Elimujamii aliyoyapokea chuoni Oxford yalimwathiri katika uandishi wake.

1.2 Swala la utafiti

Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa riwaya ya kisasa ya Kiswahili iliibuka baada ya 1970 kwa sababu kipindi hicho wasanii wengi waliacha kujikita sana katika maudhui ya maadili na kuanza kushughulikia maudhui mapya kulingana na mabadiliko na mambo yaliyokuwa yakitokea kwa sababu ya mabadiliko haya. Miongoni mwa mambo hayo ni uongozi na usaliti wa kisiasa, ulundikaji mali miongoni mwa wachache huku kukiwepo ukandamizwaji wa wengi, unafiki, ukoloni mamboleo, ufisadi, usaliti wa umma, ujamaa kama mfumo wa siasa, na utawala wa kiimla. Mabadiliko haya huitingisha jamii na kuifanya itoke katika kaida zake. Wanajamii wakaanza kujifikiria upya katika mazingira yao haya mapya, kama ilivyoshuhudiwa katika nchi za magharibi mwanzoni mwa karne ya ishirini wakati wa vita vikuu vya dunia na hata baada yavyo. Katika kujifikiria huku mwanajamii anaweza kukengeuka akataka kuwa huru na akajipapatua kutoka kwenye kaida zote za jamii zinazomnyima uhuru, ikiwemo imani kwa Mungu anayesubiri kumhesabia matendo yake na kumlipa. Ama akatamauka

akajitoa uhai kwa kuona maisha si chochote ila ubatili tu. Ama pia akaamua kusubiri ili akapate jazaa yake njema huko ahera itakayompuzisha na madhila ya ulimwengu.

Yote hayo yaliyotajwa hapo juu ni mihimili ya nadharia ya udhanaishi na inajitokeza waziwazi katika riwaya za *Kitu Kidogo Tu!* na *Harusi ya Wendawazimu.* Nasimiyu (2016) anaeleza kuwa nchi ya Tanzania ilipitia mabadiliko mbalimbali ya kijamii na kihistoria wakati wa ukoloni na baada ya uhuru. Mabadiliko hayo yaliathiri utunzi wa mashairi kifani na kimaudhui. Si utunzi wa mashairi tu ulioathiriwa kimaudhui bali pia utunzi wa riwaya kama inavyodhihirika katika riwaya hizi mbili, ilhali hakuna utafiti wowote wa riwaya hizi mbili ulioongozwa na nadharia ya udhanaishi. Hali hii ilimpa mtafiti mshawasha wa kuzitafitia riwaya hizi mbili kwa misingi ya kidhanaishi.

1.3 Malengo ya utafiti

i. Kubainisha vipengele vya udhanaishi vinavyopatikana katika riwaya za *Kitu Kidogo Tu!* na *Harusi ya Wendawazimu* za Kamugisha.

ii. Kuchanganua namna vipengele hivi vya udhanaishi vinavyotokeza kupitia matendo na maneno ya wahusika katika riwaya za *Harusi ya Wendawazimu* na *Kitu Kidogo Tu!*

1.4 Maswali ya utafiti

i. Ni vipengele gani vya udhanaishi vinavyopatikana katika riwaya za *Harusi ya Wendawazimu* na *Kitu Kidogo Tu?*

ii. Ni namna gani vipengele hivi vya udhanaishi vinatokeza katika riwaya za *Harusi ya Wendawazimu* na *Kitu Kidogo Tu?*

1.5 Natija ya utafiti

Hough (2018) anaeleza kuwa hakuna kazi yoyote ya uhakiki iliyokamilika. Huku ni kusema kuwa kila kazi yoyote ya uhakiki inayofanywa ni muhimu kwa sababu imechangia katika uwanda wake wa usomi. Kwa mantiki hii, utafiti huu ni wa manufaa katika usomi wa fasihi ya Kiswahili. Kwanza kabisa utafiti huu umechambua riwaya ambazo, kulingana na uchunguzi wa awali uliofanywa na mtafiti, riwaya hizi hazijaangaziwa sana kiusomi, na hazichambuliwa kabisa kwa misingi ya udhanaishi. Utafiti huu basi ni muhimu kwa sababu umeziweka riwaya hizi mbili katika usomi wa fasihi ya Kiswahili kwa kuzichambua.

Pili, Khamis (2008:8) anamnukuu Masinjila (1992:2) akisema kuwa katika uelezaji wa matatizo ya kitaaluma ni vigumu kupata muktadha usioelekezwa na nadharia. Hivyo basi utafiti huu uliongozwa na nadharia ya udhanaishi. Huu pia ni mchango mwengine muhimu katika fasihi ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu katika utafiti huu nadharia ya udhanaishi ilifafanuliwa kwa undani na mihimili yake pia ikafafanuliwa. Huu ni mchango wa maelezo ya kinadharia kwa Kiswahili. Nadharia huasisiwa kisha ikafafanuliwa na wasomi mbalimbali kulingana na uelewa wao wa vipengele kadhaa vya nadharia hiyo na pia kulingana na falsafa zao na tajriba zao mbalimbali. Hivyo basi watu tofauti wanaweza kutoa maelezo tofauti kidogo ya nadharia moja kulingana na namna wanavyoielewa. Mfano mzuri ni wa nadharia hii ya udhanaishi iliyo na mirengo miwili bainifu: mrengo unaomwamini Mungu na unaomkana Mungu. Watafiti wengi huegemea mrengo mmoja ili kutimiza malengo ya utafiti wao. Wengine hukita utafiti wao katika mhimili mmojawapo wa nadharia hii pia kwa kulingana na malengo ya tafiti zao. Katika utafiti huu mirengo yote miwili ilikuwa muhimu. Kwa hivyo mihili yake imefafanuliwa na kudadavuliwa kwa kina kadri iwezekanavyo. Kwa hivyo utafiti huu ni hazina tosha kwa mtafiti mwengine yeyote wa baadaye ambae angependa kuuelewa udhanaishi kwa kina katika mirengo yake.

Utafiti huu pia umechunguza kwa kina udhanaishi katika kazi za mwandishi ambaye hasa si mdhanaishi bali mwanasosholojia. Hii ni shajiisho kwa watafiti wengine nao kutumia nadharia ya kidhanaishi kutafiti kazi nyinginezo zisizoandikwa na wadhanaishi ili iwe rahisi kulinganisha mitazamo ya waandishi hawa mbeleni.

Aidha, utafiti huu ni muhimu katika jamii kwa sababu umechambua namna mwandishi anavyoyasawiri maisha ya jamii. Migogoro iliyo kwenye riwaya hizi imefafanuliwa vyema kabisa na sababu zake pia zikafafanuliwa. Mtu yeyote atakayepitia utafiti huu basi atafahamikiwa kuhusu migogoro hiyo na vyanzo vyake na uchanganuzi na mependekezo yetu yanaweza kumsaidia kutafuta njia mwafaka ya kusulihisha migogoro hii ya kijamii pindi itakapomkumba.

Mwisho, utafiti huu utakuwa muhimu katika kuongeza hazina ya marejeleo ya kazi za fasihi ya Kiswahili haswa katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Pwani. Hii itasaidia kukiweka Chuo Kikuu cha Pwani katika ramani ya marejeleo ya kazi za fasihi ya Kiswahili hivyo kufanya watafiti kuzuru Chuo na maktaba yake kila wanapotaka kufanya tafiti zao mbalimbali kuhusu fasihi ya Kiswahili.

1.6 Upeo na mipaka ya utafiti

Utafiti huu ulihusu ubainishaji wa vipengele vya udhanaishi katika riwaya mbili zilizoandikwa na Kamugisha; *Kitu Kidogo Tu!* na *Harusi ya Wendawazimu* na kueleza jinsi vipengele hivyo vinavyojitokeza kupitia matendo na maneno ya wahusika. Kwanza, vilifafanuliwa vipengele vyote vya kidhanaishi vinavyopatikana katika riwaya hizi. Mtafiti hakujikita katika kipengele kimoja tu cha udhanaishi. Kwa sababu hii, mtafiti asingeweza kuchunguza riwaya ya tatu ya Kamugisha; *Kifo cha Mwalimu Katoto (2004).* Kwa kuongeza riwaya hii ya tatu utafiti ungekuwa mpana mno haswa tukizingatia wakati na changamoto za kifedha.

Utafiti huu pia ulijikita katika kuchunguza kauli na matendo ya wahusika yenye sifa za kidhanaishi pekee. Matendo na kauli nyengine zozote za wahusika ambazo hazikuingia katika kigezo hiki hayakushughulikiwa katika utafiti huu.

Aidha, utafiti huu uliongozwa na nadharia moja pekee ya udhanaishi. Nadharia hii ilitosha kabisa kuuendesha utafiti huu na kutimiza malengo ya utafiti. Hapakuwa na pengo lolote lililohitaji nadharia nyengine ili liweze kuzibika.

Mwisho, utafiti huu ulijikita katika kuchanganua udhanaishi unavyotokeza katika riwaya hizi mbili. Hazikuchunguzwa mbinu za lugha wala mbinu za uandishi. Aidha, hatukufanya ulinganishi wowote wala kutofautisha riwaya hizi na kazi nyengine zozote za kidhanaishi zinazotambulika sana katika fasihi ya Kiswahili.

1.7 Ufafanuzi wa istilahi na vifupisho

Katika sehemu hii maelezo yametolewa kuhusu istilahi na vifupisho vilivyotumiwa katika utafiti.

Hadith- Hizi ni kauli na matendo ya mtume Muhammad (S.A.W) na matendo ya masahaba wake ambayo aliyakubali yakifanywa. Katika Uislamu, kuna vyanzo vinne vya sheria, Kurani, *Hadith*, *ijma* na *Qiyas*. Hadith zimegawanywa mara tatu, kuna *saheeh*, ambazo hukubalika kuwa hazina makosa, *Hassan*, ambazo huwa na makosa kidogo ambayo si ya kimsingi na hatimaye kuna *dhaif* ambazo zina makosa mengi ya kimsingi kwa hivyo hazina mamlaka sana katika maswala ya sheria za Kiislamu.

N.k- inamaanisha na kadhalika.

S. A. W (Salallahu Aleihi Wasalam)- rehema na amani zimshukie. Hili ni tamko linalotumiwa kumtakia mtume Muhammad rehma na amani kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Waislamu hutakikana kumwombea mtume Muhammad rehema na amani kila anapotajwa.

T. Y – Tafsiri yetu.

Ubatili/utupu - hii ni falsafa ya utupu. Inashikilia kuwa kila kitu katika ulimwengu huu hakina maana yoyote, yaani si chochote.

Ubinadamu/Utu- hii ni falsafa ambayo inaweka umuhimu mkubwa kwa binadamu na namna anavyoishi na wala si katika Mungu au miungu.

Udhanaishi- Udhanaishi ni falsafa inayoshughulikia maswala kuhusu maisha; ni mtazamo unaokagua kwa upembuzi hali ya nafasi ya mtu binafsi katika ulimwengu anamoishi.

Udhanaishi wa ukanaji Mungu/wa kikafiri - huu ni mrengo wa falsafa ya kidhanaishi unaoongozwa na ukanaji Mungu.

Udhanaishi wa Kikristo - Huu ni mrengo wa falsafa ya kidhanaishi unaoongozwa na imani kwa Mungu. Kierkergaard ni miongoni mwa wadhanaishi wa Kikristo.

Ukengeushi - Ukengeushi una maana ya mtengo/mbanduko au kuhisi ugeni. Hali hii hutokea katika mahusiano mbalimbali katika jamii kama baina ya mtu binafsi na kazi au jukumu lake, mtu na matokeo ya kazi yake, mali yake, Mungu wake na hata jamii yake. Katika mahusiano haya, hutokea wakati ambapo kunakosekana umoja na hivyo hisi za utengano kutokea.

Utamaushi- Ni istilahi inayotokana na neno “kutamauka”. Kutamauka ni kutokuwa na furaha kwa kujua na kuhisi kwamba hakuna tumaini katika maisha namna yalivyo. Pia hutumiwa kumaanisha udhanaishi.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDIKO NA MSINGI WA NADHARIA

2.1 Kitangulizi

Katika sehemu hii, mapitio ya kazi mbalimbali kuhusu udhanaishi yanajadiliwa. Nadharia ya udhanaishi na misingi yake pia inafafanuliwa. Mtindo unaotumiwa katika kufafanua kazi hizo ni ule wa tarehe. Kwa maana, zitaanzwa kuorodheshwa kazi zilizofanywa kitambo hadi zile zilizofanywa hivi karibuni.

2.2 Yaliyoandikwa kuhusu udhanaishi

Mada hii imegawanywa katika vijimada vidogo viwili: Mapitio yanayohusu tafiti na kazi nyingine katika fasihi kwa kuzingatia mbinu na matokeo na ya pili ni maandishi mbalimbali kuhusu nadharia ya udhanaishi. Katika kijimada cha kwanza, tafiti mbalimbali zilizohusu udhanaishi zitapitiwa na katika sehemu ya pili maelezo ya wataalamu mbalimbali kuhusu udhanaishi yatafafanuliwa.

2.2.1 Mapitio yanayohusu tafiti na kazi nyingine katika fasihi kwa kuzingatia mbinu na matokeo

Gwachi (1991), alichunguza ukengeushi wa wahusika wasomi katika riwaya za Kezilahabi: *Rosa Mistika, Kichwa maji, Dunia Uwanja wa Fujo* na *Gamba la Nyoka*. Amechambua jinsi wahusika wasomi walivyosawiriwa na hali zilizosababisha ukengeushi wao na mapendekezo yanayopendekezwa na mwandishi kuhusu suluhu ya hali hiyo. Anaonyesha daraja mbalimbali za ukengeushi zinazoonyeshwa na wasomi katika uhusiano wao na wanajamii wengine kama vile, ukengeushi wa kukosa mamlaka, kukosa adabu, kutengwa pamoja na kujitenga na wanajamii na kujitenga na nafsi. Aidha, amechunguza msomi na uhusiano wake na jamii pamoja na mamlaka au uwezo anaopatiwa na jamii hiyo. Utafiti wa Gwachi ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu

kwanza alichunguza wasomi ambao pia ndio wahusika wakuu katika riwaya hizi mbili za Kamugisha: *Kitu Kidogo Tu!* na *Harusi ya Wendawazimu.* Ijapokuwa ameongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamaa, ameitumia nadharia hiyo kuchunguzia ukengeushi ambao ni mhimili mmoja katika mihimili ya udhanaishi. Utafiti huu wa Gwachi (keshatajwa) ulikuwa muhimu katika utafiti wetu kwa sababu tulipata maelezo ya kina kuhusu ukengeushi wa wahusika. Ukengeushi ni kipengele kimoja cha kidhanaishi tulichokifafanua katika utafiti wetu na utafiti wa Gwachi (keshatajwa) ulitusaidia kufanya hivyo.

Musau (1995) amelinganisha riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) ya Kezilahabi na *Tess of the D'Urbervilles* (1891) ya Hardy. Katika kulinganisha kwake, Musau amejaribu kuonyesha jinsi riwaya hizi zinavyoingiliana katika kipengele cha udhanaishi kinachoeleza kuwa ijapokuwa mwanadamu yuko huru kuishi anavyotaka ulimwenguni, ila kuna mambo mengi katika maisha kama maradhi ambayo humkumba ilhali hana uwezo wa kuyabadilisha. Anashadidia mawazo haya kwa kutoa mifano kutoka riwaya ya Hardy anapotumia maneno kama: "Aliyelaaniwa", "Aliyejaaliwa" na ilipodhihirika kuwa Tess (mhusika mkuu katika riwaya ya *Tess of the D'Urbervilles*) atanyongwa, mwandishi anasema kuwa "miungu walikuwa wameuhitimisha mchezo wao na Tess". Musau anasema, "haya yote yanatuelekeza kufikiria kuwa maisha ya Tess hayakuwa mikononi mwake lakini yalikuwa yanadhibitiwa au yanachezewa na miungu au viumbe wengine wenye nguvu za miungu." (1995:65). Haya ndiyo yale mawazo ya Kierkegaard (keshatajwa) kuwa, "mtu haishi kwa nguvu zake bali ni kikaragosi cha nguvu zilizomuumba". Utafiti huu wa Musau (keshatajwa) ulitusaidia kuelewa namna wadhanaishi wanavyoeleza maisha ya mwanadamu na misukosuko anayokumbana nayo na jinsi yeye mwanadamu mwenyewe wakati mwingi hushindwa kurekebisha mkondo unaofuatwa na maisha yake . Wahusika kama hawa pia tunakutana nao katika utafiti

wetu. Hata hivyo, tofauti na utafiti wetu, Musau analinganisha wahusika wakuu katika kazi anazochambua ilhali sisi hatukufanya ulinganishi wowote.

Mungah (1999), amechunguza dhana ya maisha katika riwaya mbili za Kezilahabi: *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991). Ijapokuwa mtafiti alitumia nadharia ya kisosholojia, maswala aliyoyatafiti yanahusiana na ya udhanaishi. Udhanaishi kama nadharia unahusu ‘dhana ya maisha’. Katika sura ya nne, amechunguza jinsi mwandishi Kezalahabi alivyoathiriwa na mazingira mbalimbali ya kidhanaishi. Anasema mazingira haya yalianza kipindi cha ukoloni Kezilahabi alipozaliwa. Akaathiriwa na shule aliyopelekwa haswa ya kiseminari ambako alishindwa kufuzu na kuwa padre. Kisha Kezilahabi akaathiriwa na mazingira mapya baada ya ukoloni alipoona serikali mpya ya mtu mweusi inazidi kumgandamiza mwananchi wake na kumsababishia mateso zaidi. Mungah (keshatajwa) anasema yote haya yalimfanya Kezilahabi kujiuliza upya kuhusu maana ya maisha kwa mateso mwanadamu anayopitia. Kuongezea athari hizi, Kezilahabi akapatana na vitabu wa wadhanaishi kama Albert Camus (1913-1960), Samuel Beckett (1906-1989) alipofika chuo kikuu. Utafiti huu ni muhimu kwetu kwa sababu umechunguza dhana ya maisha ambayo pia tuliichunguza na pia amechunguza udhanaishi ambao ndio mada yetu kuu. Kwa hivyo utafiti wake ulitusaidia kuvielewa zaidi vipengele hivyo.

Mose E. (2005), amechunguza taashira za kifo katika tamthilia za *Mukwava wa Uhehe* (1979), *Amezidi* (1995), *Kilio Cha Haki* (1981) na *Visiki* (1984). Mtafiti alitumia nadharia ya vikale kuchunguza taashira mbalimbali za kifo katika tamthilia za Kiswahili. Kifo ni kati ya vipengele vikuu vya nadharia ya udhanaishi. Mose (keshatajwa) alibaini kuwa taashira za kifo zilizotumiwa katika tamthilia za Kiswahili ni kama ushujaa, uzalendo, utupu wa maisha na uozo wa mawazo miongoni mwa nyingine. Katika utafiti wake, amerejelea mawazo ya wadhanaishi kadhaa kama vile; Samuel Becket

akinukuliwa na Mueller (1964), Camus, Kierkegaard n. k. Utafiti huu pia ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu umeshughulikia kipengele cha kifo kwa kina. Kutokana na utafiti huu tulipata uelewa zaidi kuhusu kifo na athari zake kwa wanajamii. Aidha, utafiti wa Mose (keshatajwa) ulitusaidia kueleza imani ya jamii za Kiafrika kuhusu swala la kifo.

Rehak (2007) anatumia nadharia ya udhanaishi kulinganisha na kutofautisha vipengele vya upweke na kunyong'onyea/kufa moyo katika riwaya mbili, *Kichwamaji* (1974) ya Kezilahabi na *L'etranger* (1942) ya Camus. Rehak (keshatajwa) anafanya hivyo kwa kulinganisha na kulinganua sifa za wahusika wakuu katika riwaya hizo, Kazimoto wa *Kichwamaji* na Meursault wa *L'etranger.* Mtafiti amelinganisha sifa za kidhanaishi na kuzitofautisha vilevile na amegundua kuwa mbali na kuwa wahusika wa riwaya zote hizi wanaonyesha sifa za kidhanaishi, Kazimoto bado anajali kuhusu maisha ya jamii inayomzunguka, tofauti na Meursault ambaye anakiri kuwa maisha na vifo vya watu wengine (hata mamake alipokufa) havimhusu na kinachomhusu zaidi ni uhai na uhuru wake yeye mwenyewe. Utafiti huu ulikuwa muhimu katika utafiti wetu kwa sababu ulitusaidia kueleza kuhusu uhuru wa mwanadamu na jinsi uhuru huo unavyomwathiri katika jamii yake.

Migiro (2012), ametumia nadharia ya udhanaishi wa kifeministi kuchunguza motifu za usufi katika utenzi wa *Kiokozi cha Banati*. Kutokana na utafiti wake, Migiro (keshatajwa) alibaini kuwa motifu mbalimbali za usufi zilizomo katika Utenzi wa *Kiokozi cha Banati* zinatokana na misingi ya imani na mwongozo uliomo katika kielelezoasili cha Kurani takatifu pamoja na *Sunna* na *Hadithi* za Mtume Muhammad (S.A.W). Udhanaishi huu uliojikita katika misingi ya imani ya kidini ndio ule udhanaishi wa Kierkegaard wa kumwamini Mungu na uwezo wake juu ya wanadamu. Utafiti huu ulikuwa muhimu katika utafiti wetu haswa tulipowachanganua wahusika walioshika dini

kama Stella na Mwalimu Tadeo. Utafiti wa Migiro (keshatajwa) Ulitusaidia kueleza nafasi ya dini kwa wahusika na jinsi inavyoathiri maisha yao.

Makoyo (2014), anaeleza jinsi nadharia ya udhanaishi inavyoweza kutumiwa katika elimu ya Kenya ili kuweza kutayarisha wananchi wanaoweza kujitegemea katika jamii. Katika tasnifu yake yenye mada "*A critique of Christian education for self reliance in Kenya in light of existentialism",* Makoyo (keshatajwa) anaikosoa elimu ya Kenya ambayo anasema imejikita katika misingi ya dini ya Kikristo ambayo inafunza watu kuamini tu bila kuuliza maswali. Anasema kuamini huku kunawafanya watu washindwe kujitegemea kwa sababu wanaogopa kufanya maamuzi muhimu katika maisha yao kwa kuhofia ghadhabu za Mungu. Makoyo (keshatajwa), kama watafiti wengine wa udhanaishi wa kikafiri waliomtangulia, anapendekeza Mungu atolewe katika elimu ya Kenya na maisha ya wanafunzi ili wafunzwe kufanya maamuzi muhimu maishani mwao yatakayowafanya wajitegemee bila kuogopa kuwa baadaye Mungu atawauliza na kuwaadhibu kwa sababu kulingana naye, huyo Mungu mwenyewe hayuko.

Katika utafiti huu wake, Makoyo (keshatajwa) anasisitiza ubinafsi wa mtu, kuwa mtu ajifunze kufanya maamuzi muhimu katika maisha yake na awe tayari kwa matokeo ya maamuzi hayo. Makoyo (keshatajwa) anasema nadharia hii ikitekelezwa katika mfumo wa elimu ya Kenya, kila mtu atajitegemea hivyo kupunguza matatizo mengi yanayokumba Wakenya kama vile umaskini. Katika utafiti wake huu, Makoyo (keshatajwa) ameshughulikia mfumo wa elimu ya Kenya. Hakuchunguza riwaya hizi mbili za *Kitu Kidogo Tu!* na *Harusi ya Wendawazimu,* wala hakuchunguza kazi yotote ya fasihi. Aidha, katika utafiti wake ameegemea mrengo wa wadhanaishi wasioamini uwepo wa Mungu ilhali katika utafiti wetu tumeshughulikia wahusika wanaoegemea mirengo yote miwili, ya kuamini na kutoamini Mungu. Vilevile, Makoyo (keshatajwa) ameshughulika sana na kipengele cha uhuru wa mtu binafsi. Katika utafiti wetu

tutaongozwa na vipengele vyote vya udhanaishi kwa jumla wala si hiki kimoja cha uhuru pekee. Hata hivyo, utafiti wa Makoyo (keshatajwa) ulitusaidia tulipokuwa tunawachanganua wahusika ambao ugumu wa maisha uliwafanya wamkane Mungu.

Rettová (2016) anaeleza kuwa tangu Kezilahabi alipoanzisha dhana ya udhanaishi katika fasihi ya Kiswahili kupitia riwaya zake mbili, *Kichwamaji* (1974) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), kumekuwa na mazoea ya kutumia udhanaishi katika kuchambua kazi zozote za fasihi zinazoonekana kuwa za kifalsafa. Anaendelea kuchambua kazi nyengine za kidhanaishi kama mashairi kutoka diwani ya *Sauti ya Dhiki* (1973). Pia anachambua *Ua la Faraja* (William Mkufya 2004) anayoiita 'riwaya ya tatu ya kidhanaishi ya Kiswahili'. Aidha, anataja riwaya ya *Kiu* (1972) na *Nyota ya Rehema* (1976) za Mohamed Suleiman kama riwaya za kidhanaishi. Katika utafiti wake, Rettová (keshatajwa) hakusema chochote kuhusu riwaya za *Harusi ya Wendawazimu* na *Kitu Kidogo Tu* za Thomas Kamugisha ambazo kufikia wakati wa utafiti wake huo zilikuwa zishatungwa na kuchapishwa tayari. Utafiti huu utasaidia kupanua zaidi kazi zinazochambuliwa kwa misingi hii ya kidhanaishi.

Katika kazi zote tangulizi ambazo mtafiti aliweza kuzipitia kama zilivyotajwa hapo juu, riwaya hizi mbili za Kamugisha zilikuwa hazijashughulikiwa kwa misingi ya kidhanaishi. Hivyo, palikuwa na haja ya utafiti huu ili kujaribu kuziba mapengo kama yalivyojitokeza hapo juu. Aidha, utafiti huu umesaidia kupanua kazi zinazochambuliwa kwa misingi ya kidhanaishi ambazo watafiti wengi wa hapo awali wameishia kuegemea zaidi katika kazi za Kezilahabi. Kuna pengo la uchambuzi wa kazi za waandishi wengine wa kidhanaishi kama Kamugisha ambalo utafiti huu ulinuia kuliziba.

2.2.2 Maandishi mbalimbali kuhusu nadharia ya udhanaishi

Nadharia hii hujaribu kueleza uhuru wa mtu binafsi, uwezo wa mtu kujifikiria na kujiamulia ni wajibu wa mtu mwenyewe katika ulimwengu. Udhanaishi husistiza kuhusu ubinafsi wa mtu na uhuru wake wa kufanya uamuzi wa kumfaa mwenyewe katika majukumu yake, Makoyo (2014). (T.Y).

Njogu na Chimerah (1999) katika *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu* wanaeleza kuwa wadhanaishi wengi hutilia mkazo mateso yanayomkumba binadamu. Maudhui wanayoyashughulikia ni kama vile kifo, uhuru wa mtu binafsi, wajibu wa binadamu duniani, ubinafsi, kukata tamaa, na udhaifu wa kibinadamu.

Naye Njogu na Wafula (2007) katika *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi* wanaeleza kuwa udhanaishi ni falsafa kuhusu ‘dhana ya maisha’. Ni falsafa inayohusiana na ‘utamaushi’, istilahi inayotokana na neno “kutamauka”. Kutamauka ni kutokuwa na furaha kwa kujua na kuhisi kwamba hakuna tumaini katika maisha.

Udhanaishi ni dhana iliyokuwa inajaribu kueleza mazingira na hali ya kutamausha katika kipindi maalum cha kihistoria. Ilikita sana Ujerumani baada ya kushindwa katika vita vya pili vya dunia. Katika kipindi hiki watu waliafikiana na nadharia ambazo mihimili yake ilikuwa hofu, kihoro, kutamauka na kufeli (Wamitila 1997:16).

Baadhi ya wadhanaishi wa karne ya ishirini wanaotambulika sana ni pamoja na Martin Heidegger (1889-1976) na Karl Jaspers (1883-1969) kutoka Ujerumani, Wafaransa Gabriel Marcel (1889-1973) na Jean-Paul Sartre (1905-1980), Mhispania José Ortega y Gasset (1883-1955), Nikolai Berdyaev (1874-1948) mwenye asili ya Ki-Rusi na Nicola Abbagnano (1901-1990) kutoka Italia.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa katika karne ya ishirini, udhanaishi ulipata msukumo mpya kutoka kwa mwanafalsafa wa Kijerumani Friedrich Nietzsche na wengine kama Martin Heidegger, Gabriel Marcel na Karl Jaspers. Anaeleza kuwa pamoja na kuuelezea

mtazamo huu kwa mapana, wanafalsafa hawa wanaingiza ndani yake dhana ya kutomwamini Mungu.

Nyakati hizo za mwanzo wa karne ya ishirini, katika mataifa ya magharibi kulikuwa na vita vya kwanza na vya pili vya dunia. Maisha yalionekana kutokuwa na maana kwa jinsi vita hivyo viliangamiza mamilioni ya watu. Aidha maisha yalikuwa magumu kwa chumi kuporomoka. Wakati wanafalsafa wengine kama Nikolai Berdyaev wakiendelea kushikilia udhanaishi wa kikristo wa Kierkegaard na kuonyesha matumaini, wengi walihisi kutokuwa na matumaini maishani, na wengine kama Sartre wakadai kwamba Mungu amekufa, kwa sababu kama angelikuwa hai, asingeliwaruhusu kuteseka kama walivyokuwa wakiteseka na kuwacha mamilioni ya watu wasio na hatia kuangamia.

Hata hivyo, Sartre si wa kwanza kudai kuwa Mungu amekufa, mawazo yake yaliathiriwa na mwanafalsafa wa Kijerumani wa karne ya kumi na tisa Fredrick Nietzsche (1844-1900). Nietzsche (1882/1974) katika *The gay science* anadai kuwa Mungu amekufa. Tamko hili lake pamoja na misimamo ya wenzake vinakuwa misingi muhimu ya kuzuka kwa udhanaishi wa ukanaji Mungu.

Nietzsche (1887/2003) anasema, “Mungu amekufa. Anabaki katika umauti huo. Na ni sisi tuliomuuwa… Si itabidi sasa sisi tuwe miungu ndo tuwe stahiki wa tendo kama hilo?” (T.Y). Nietzsche (keshatajwa) aliitoa kauli hii kusisitiza uhuru wa mwanadamu, kuwa mwanadamu yuko huru kufanya maamuzi yoyote na kuishi maisha yake anavyotaka yeye bila kujali kuulizwa kwa sababu mwanadamu ni hakimu wa maisha yake, na kuishi hivi basi mwanadamu anafaa kumkana Mungu. Charlseworth (1975) anayaunga mkono mawazo haya kwa kusema kwamba ikiwa Mungu yuko basi mwanadamu hawezi kuwa huru, na kama mwanadamu yuko huru basi Mungu hayuko. Nietzsche, akinukuliwa na Brown (1974:139) anasema: “…Kwa hakika sisi wanafalsafa huona furaha kuu kwa machweo mapya ya ripoti kuwa Mungu amekufa... roho zetu

zinafurika kwa furaha, mshangao na matarajio… anga yaonekana imefunguliwa tena… Sasa meli zetu zitang'oa nanga na kuelekea baharini tayari kukumbana na shida zote za bahari… Kila janga sasa litahusishwa na aliyekumbwa nalo... bahari ni yetu sasa na bahari huru kama hii haijawahi kuweko maishani...”

Nietzsche (1974:187) anaeleza kuwa dhambi ni uvumbuzi wa Wayahudi na Ukristo umejaribu kufanya ulimwengu uwe wa Kiyahudi.

Akinpelu, (1981:155), akizungumzia kuhusu uhuru alionao mwanadamu anasema watu wanapowachwa huru kujiamulia mambo yao, hawana budi ila kujitafutia maana ya maisha yao. Hivyo, wataelewa kuwa matatizo yanayowakumba wanadamu si kwa sababu ya nyota zao au Mungu (majaaliwa) bali ni wao wenyewe (maamuzi yao). (T.Y).

Waandishi wengi ambao wanajadili kuhusu utamaushi wanatilia mkazo matatizo halisi yaliyomsibu mwanadamu na wanakwepa imani ya kinjozi na kifikra juu ya maana ya kuishi. Kuwa Mungu yupo au aliuumba ulimwengu ni suala ambalo hawalishughulikii kwa sababu halioani na mantiki ya fikra zao. Baadhi ya maudhui yanayotajwa na kuelezwa na watamaushi ni kama: uhuru wa mtu binafsi, uwezo wa mtu wa kujifikiria na kujiamulia na wajibu wa binadamu katika ulimwengu. Kwa vile mwanadamu anaweza kuwa chochote, ubinafsi ni muhimu kwa sababu jukumu la kujitekelezea na kujiridhisha ni la kibinafsi. Maudhui mengine yaliyotagaa katika utamaushi ni; ukengeushi, hali ya kutokuwa na uhakika (chochote chaweza kutokea), kukata tamaa, na mauti.

Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa kwa upande mwingine, kuna wale wanaoamini kwamba utamaushi ni upinzani yakini dhidi ya mielekeo na mitazamo iliyokuwa ikichipuka ambayo ilitilia maanani umuhimu wa jamii kuliko mtu binafsi. Hivyo basi, mtu alihitaji kupingana na jamii kwa kutetea ubinafsi wake, ubinafsi ambao

ulitilia maanani umuhimu wa jamii kuliko mtu binafsi. Ubinafsi ambao daima ulikuwa ukinyimwa uhuru kwa masharti na mikatale ya kijamii.

Hata hivyo, wadhanaishi wote huzungumzia kwa hamasa tanzia iliyokurubiana na maisha ya binadamu. Wanaonyesha kwamba juhudi za mtu za kujitafutia maana ya maisha mara nyingi huishia katika mvunjo au uvunjikaji wa juhudi hizo, hasa katika mauti. Mwisho wa mwanadamu ni kifo. Utamaushi unajadili hali kama fadhaa, mashaka, na uchovu na jinsi zinavyoathiri maisha ya binadamu.

Aidha, wadhanaishi wote (wanaoamini na wasioamini Mungu) wanakubaliana kuwa kuna hatari na mipaka katika maamuzi yake mwanadamu. Na hatari kubwa zaidi ni ukengeushi ambao hushusha thamani ya mtu. Ili kuepuka hatari kama hizi, wadhanaishi wa kidini (kama Marcel, Karl Barth, na Rudolf Bultmann), wanasema kuna hakika ya Mungu kukuepusha na hatari kama hizo pale tu utakapomwamini na kumwabudu.

Charlesworth (1975) anatambua kuwa katika juhudi hizi za kila mtu kujitafutia maana ya maisha yake kuna vizingiti kama vile fadhaa, hofu, ukengeushi, uchovu na kukata tamaa. Anaposhindwa kupata maana ya maisha basi mtu huweza kujiua. Wadhanaishi wasioamini Mungu wanashikilia kuwa maisha hayana maana yoyote isipokuwa utakayoipa wewe na wadhanaishi wanaoamini Mungu wanaamini maisha yanaweza kuwa na maana ambayo sisi wanadamu hatuwezi kuelewa.

Njogu na Chimerah (1991) wanafafanua kuwa, katika fasihi ya Kiswahili, mwandishi Euphrase Kezilahabi ndiye anayeandika zaidi akiegemea nadharia ya udhanaishi. Katika vitabu vyake kuanzia *Rosa Mistika* (1971), *Kichwamaji* (1974) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), tunakutana na wahusika wasiokuwa na matumaini maishani na hata wengine wanaishia kujiua kwa ugumu wa maisha yao. Waandishi wengine wa fasihi ya Kiswahili wanaoweza kuhakikiwa kwa kutumia udhanaishi ni Mkufya- *Ziraili* na *Zirani*

(1999), Khamis – *Amezidi* (1995), *Tata za Asumini* (1990) na *Janga la Werevu* (2011). Riwaya hizi zimesheheni masuala ya kidhanaishi kama vile kihoro, swala la Mungu, ubwege n.k.

2.3 Msingi wa nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya udhanaishi. Udhanaishi ni falsafa inayoshugulikia masuala kuhusu maisha; ni mtazamo unaokagua kwa upembuzi hali ya nafasi ya mtu katika ulimwengu anamoishi. Pia ni falsafa inayozungumzia uhusianao uliopo kati ya mtu na Mungu na iwapo mtu anapaswa kuamini kuwepo kwa Mungu.

Udhanaishi si dhana ngeni katika fasihi, kulingana na *Encyclopedia Britanica.1981 toleo. X, uk.73-77,* udhanaishi ni dhana inayoweza kuhusishwa na mwanafalsafa Socrates kupitia kauli yake ya *'know thyself'.* Hata hivyo, wataalamu wengi wanamtambua mwanafalsafa wa Ki-Deni Soren Kierkegaard (1813-1855) kuwa baba wa udhanaishi kutokana na mawazo yake katika vitabu vyake: (1843) *Fear and Trembling* (1843), *The Concept of Dread* (1844) na *The Sickness Unto Death* (1849).

Katika maandishi yake haya, Kierkegaard anashikilia kwamba mtu haishi kwa nguvu zake bali ni kikaragosi cha nguvu zilizomuumba. Na ni katika kuzicha nguvu hizi ambapo mtu huyu anaweza kupata utulivu wa kiroho. Anaeleza kuwa nguvu hizi zinazomtawala ni za Mungu, na kuwa binadamu anapoishi hutenda dhambi na ili apate utulivu wa kiroho inambidi atubu dhambi hizo. Anaendelea kusema kwamba udhanaishi ni dhana ya hofu pale ambapo binadamu huogopa adhabu kutoka kwa Mungu kwa hivyo amefunikwa na wasiwasi na hataki kumkosea Mungu. Kierkegaard (keshatajwa) anaamini kuwepo kwa Mungu kwa binadamu wote.

Anasisitiza kuwa binadamu ni mtu binafsi (hali ya kujijali) na hupata kimbilio kutoka kwa mivutano ya maisha kupitia kwa Mungu. Imani hii ilishika nguvu sana kwenye ukristo, huu ukawa mwanzo wa udhanaishi wa Kikristo.

Kulingana na Kierkegaard (keshatajwa) ubinafsi haswa ni mtu kujitambua kwanza yeye ni nani na maisha yetu yana lengo gani na tutaishi vipi ili kufikia lengo hilo. Iwapo juhudi zetu zitakuwa za kutafuta anasa na raha za duniani tu (na kujisahaulisha), basi kuna uwezekano tunaishi bila malengo au tunaishi maisha yasiyo na maana (Makoyo, 2014 akimnukuu Hanmony, 1996). (T.Y).

Kierkegaard alieleza kuhusu vipindi vitatu katika maisha ya mtu ambavyo kati yavyo hakuna maendeleo yoyote: kipindi cha ujumi, katika kipindi hiki mtu huishi kwa kujali raha za wakati anamoishi pekee bila kujali kesho. Kipindi cha pili ni cha uhalali/adabu (ethical stage), ambapo maisha huwa yameimarika na kuendelea kupitia kazi na ndoa. Kipindi cha tatu ni cha dini (religious stage) ambacho hutambulika kwa imani. Imani ambayo huwa na uhakika wa kuogofya, uoga ambao huonyesha kwa hakika uhusiano wa kisiri alionao mja na Mungu. Mbali na falsafa hii kuwepo tangu karne ya kumi na tisa, neno *existentialism* (udhanaishi) lilianza kutumiwa rasmi na mwanafalsafa Jean Paul Sartre (1945) baada ya msamiati huo kupendekezwa kwake na mwanafalsafa Gabriele Mercel.

Kwa mujibu wa Jean Paul Sartre, ambaye ndiye mwasisi mkuu wa udhanaishi baada ya vita vikuu vya dunia, mtu huzaliwa au hujipata ametumbukia kwenye ombwe la aina fulani. Yuko huru kuishi huku akikabiliana vilivyo na ulimwengu uliomzunguka. Kwa kuwa hana uwezo juu ya masuala kama maumivu na mateso, anaweza kukata tamaa. Hata hivyo, kabla ya kukumbwa na mauti, mtu huyo atafanya matendo yanayoyapa maisha yake maana.

Katika tamthilia yake *No exit*, Sartre (1956), alisisitiza kuwa “kuzimu ni watu wengine” (yaani viumbe wengine ambao si binadamu). Hii ni ishara kuwa kila mtu ana uwezo wa kuchagua na uhuru wa kila mtu unaweza kuathiri uhuru wa watu wengine. Alisisitiza pia kuwa dini haiwezi kutatua shida za binadamu. Isitoshe, aliegemea katika swala la ubinafsi wa mtu. Sartre anasema mtu kwanza huhisi kwamba anaishi, kisha mambo mengine yakamfungukia katika hali yake ya kuishi.

Sartre (1965) katika *Being and Nothingness*, anasema kwa kuwa hakuna Mungu, basi binadamu hajapangiwa chochote hivyo ni jukumu la kila mtu binafsi kujitafutia maana ya maisha yake.

Nadharia hii inasaidia kuhakiki maisha ya mwanadamu anayeishi katika ulimwengu uliojaa shida na matatizo mengi yanayosababishwa na binadamu mwenyewe. Shida anazozipitia ni kama vita, njaa, uchumi kuzorota, kukosa kazi na ajali barabarani. Matatizo haya yanamfanya mwanadamu kukata tamaa na kushuku iwapo kweli Mungu yuko.

Akiongozwa na nadharia hii, mtafiti alichunguza na kuhakiki riwaya hizi mbili za Kamugisha kupitia matendo na kauli za wahusika zilizo na vipengele vya udhanaishi kama vilivyojadiliwa na Søren Kierkegaard (1813-1855) na Jean Paul Sartre (1905-1980).

2.3.1 Mihimili ya udhanaishi

Ifuatayo ni mihimili ya udhanaishi kama ilivyojadiliwa na wataalamu Søren Kierkegaard (1813-1855) na Jean Paul Sartre (1905-1980);

1. **Uhuru wa mtu binafsi**

Uhuru wa mtu binafsi, uwezo wa mtu wa kujifikiria na kujiamulia ni wajibu wa binadamu katika ulimwengu. Kuna uhuru wa kufanya uamuzi na uamuzi wa kuwa huru. Hivyo, mwanadamu yuko huru kufanya maamuzi yoyote, ila maamuzi yake yanaweza kumfanya azidi kuwa huru au afungike zaidi. Wadhanaishi wanasema hakuna mtu aliyepangiwa atakavyoishi, ni mtu mwenyewe maamuzi yake kujitafutia maana ya maisha yake kwa kuwa mwanadamu si chochote isipokuwa atakavyoamua mwenyewe kuwa.

2. **Swala la Mungu**

Swala la kuwepo au kutokuwepo kwa Mungu ni moja kati ya mihili inayojadiliwa sana na wadhanaishi. Kuna wadhanaishi wanaoamini uwepo wa Mungu na wanashikilia kuwa maisha ya mtu yana maana jinsi yalivyo, na kuwa tunaweza tusielewe ila Mungu mwenyewe anajua maana hiyo. Hivyo mwanadamu asikate tamaa, awe na imani kwa sababu imani kwa Mungu pekee huyapa maisha maana. Hata hivyo, kuna wanaudhanaishi wasioamini uwepo wa Mungu. Wanashikilia kuwa mwanadamu ana jukumu la kutafutia maisha yake maana na kwamba yuko huru kuyapa maisha yake maana yoyote anayotaka yeye kwa kuishi anavyotaka, bila kujali kuwa ataadhibiwa siku ya kiama. Kwao, Mungu alikufa kwa hivyo hakuna wa kuwauliza chochote.

3. **Kifo**

Udhanaishi hutilia mkazo matatizo halisi yanayomsibu binadamu. Hujadili hali kama vile kihoro, ufupi wa uhai, fadhaa, mashaka, pekecho, utupu wa maisha na uchovu na jinsi zinavyoathiri maisha ya binadamu. Jazanda zinazoashiria kiungulia, uchovu, pekecho na kiwewe zinatumika kusawiria hali ya binadamu. Mwisho, huangazia kwa hamasa tanzia iliyokurubiana na maisha ya binadamu. Huonyesha kwamba juhudi za mtu za kujitafutia maana ya maisha mara nyingi huishia katika mvunjo au uvunjikaji wa

juhudi hizo, hasa katika mauti. Mwisho wa binadamu ni kifo. Hivyo, kifo ni ithibati tosha kuwa maisha hayana maana namna yalivyo.

4. **Ukengeushi**

Ukengeushi una maana ya mtengo au mbanduko au kuhisi ugeni. Hali hii hutokea katika mahusiano mbalimbali katika jamii. Mtu binafsi katika jamii hana nafasi ya kujiamulia matendo yake badala yake analazimika kutenda kulingana na kaida fulani maalumu zilizopangwa na jamii pana. Hivyo, Ukengeushi huanza pale mtu anapojaribu kufikiria kibinafsi na kutenda kinyume na kaida na miiko iliyozoeleka. Huanza kuwa na migogoro ya ndani kwa ndani anapopambana na nguvu hatari ambazo zinajaribu kummeza na kumwangamiza. Anajiamulia matendo yake. Katika kutafuta uhuru wake wa mawazo na matendo, binadamu anakengeushwa na Mungu, jamaa au familia yake, asili yake na yeye mwenyewe.

5. **Utamaushi**

Kukata tamaa. Ijapokuwa mwanadamu yuko huru kuamua na kuwa chochote anachotaka kuwa, anafaa kujua kuwa uhuru huu una mipaka hasa katika mapungufu ya kimaumbile. Asipogundua mipaka yake na akajaribu kufanya mambo na yasiwezekane kwa ajili ya mapungufu haya, mwanadamu anaweza kukata tamaa kwa kukosa alichokitaka hivyo kushindwa kuyapa maisha yake maana. Mwanadamu anaposhindwa kuyakabili maisha namna yalivyo na kushindwa kujitafutia maana ya maisha yake, basi anaweza kufanya uamuzi pekee alio na uwezo nao, kujitoa uhai.

6. **Kuabudu mahitaji ya kimwili**

Kwa vile binadamu yuko huru kufanya anachotaka, ni wajibu wake kushughulikia mahitaji yake ya kimwili kwa njia anayotaka yeye. Hivyo ni sawa mtu kushiriki katika matendo kama zinaa, ngono za jinsia moja, kuwa na wapenzi wengi, kulewa n.k ili kukidhi mahitaji ya mwili wake. Kwa wadhanaishi, taasisi kama ndoa si muhimu alimuradi mtu anapata mahitaji yake ya kimwili.

7. **Utupu wa maisha/ ombwe**

Mwanadamu si chochote, kwa sababu kulingana na wadhanaishi hakuna hata falsafa moja inayoweza kueleza mwanadamu ni kitu gani. Aidha, kifo kinapokuja humfuta mwanadamu (individual being) akawa hayupo tena, kukabaki utupu. Kabla ya kuzawa mwanadamu huwa kuna utupu na baada ya mauko yake huwa kuna utupu. Mwanadamu huwako katikati ya utupu; mbele yake kuna utupu na nyuma yake kuna utupu/ombwe/ubatili.

2.4 Kihitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia mapitio ya maandishi mbalimbali ya awali ambayo kwa namna anuwai tumeona jinsi yalivyokuwa mchango mkubwa katika utafiti huu wetu. Aidha, tumeonyesha jinsi tafiti hizo mbalimbali ni tofauti na huu utafiti wetu hivyo kuufanya utafiti huu kuwa muhimu.

Katika sura hii pia tumefafanua za wasomi mbalimbali kuhusu nadharia ya udhanaishi iliyotumiwa kuendeshea utafiti huu. Aidha, tumeifafanua nadharia ya udhanaishi kwa kina, tukawataja waasisi wake na kufafanua mihimili yake mbalimbali.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Kitangulizi

Katika sehemu hii mtafiti anaeleza kuhusu aina ya utafiti huu, mbinu alizotumia kufanyia utafiti, utaratibu wa utafiti, mbinu za kukusanya data, mbinu za kuchanganua data na mbinu za kuwasilisha data iliyopatikana.

3.2 Aina ya utafiti

Utafiti huu ni wa kithamano. Utafiti wa aina hii huhusisha kukusanya data na kisha data hiyo ikachanganuliwa kwa njia ya maelezo bila kutumia tarakimu. Utafiti huu ni wa kithamano kwa sababu data iliyokusanywa ilichanganuliwa na kuelezwa kwa lugha nathari kwa kuzingatia malengo ya utafiti wenyewe.

3.3 Muundo wa utafiti

Utafiti huu ni wa kimaelezo. Riwaya zilizotafitiwa zilisomwa kwa kina. Data iliyokusanywa ikachanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya kimaelezo kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Aidha, tafiti mbalimbali zinazohusu udhanaishi zilisomwa na maelezo yake kutumiwa kuupa nguvu utafiti wetu.

3.4 Uteuzi wa sampuli

Sampuli ni kitu kimoja au baadhi ya vitu vinavyochukuliwa kutoka kwa kundi kubwa la vitu vya namna moja ili kuliwakilisha kundi zima. Kuna data za sampuli mbili, sampuli lengwa na sampuli nasibu. Sampuli lengwa hupatikana kwa mbinu ya usampulishaji kusudio. Hivyo basi, usampulishaji ni mchakato wa kuteua sampuli mwafaka ambayo mtafiti anaona itamfaa kwa kumpatia data faafu ya utafiti wake. Kombo na Tromp (2006) wanaeleza kuwa usampulishaji kusudio hutumiwa pale ambapo mtafiti hulenga kimakusudi kundi fulani analoonelea kuwa lina uwezo wa kuzalisha data zenye sifa na

habari anazozihitaji. Powell na Connaway (2004) wanaeleza kwamba, katika usampulishaji kusudio, sampuli huteuliwa kwa kuzingatia vigezo ambavyo vinahusiana na maswali ya utafiti. Hivyo basi katika utafiti huu, riwaya mbili za Kamugisha *Kitu Kidogo Tu!* na *Harusi ya Wendawazimu* zilichukuliwa kama sampuli lengwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti.

Sampuli nasibu nayo ilipatikana kwa kudurusu vitabu, makala, majarida, tafiti za awali na tovuti mbalimbali ambazo zilikuwa na data iliyohusiana na utafiti huu. Data iliyopatikana hapa ilisaidia kueleza kuhusu riwaya na nadharia ya udhanaishi. Maelezo haya yalisaidia kuupa nguvu uchanganuzi wa data iliyopatikana.

3.5 Data ya utafiti

Katika utafiti huwa kuna aina mbili kuu za data inayokusanywa. Kuna data ya msingi na data ya upili. Kothari (2008) anaeleza kuwa data ya msingi ni data ghafi ambayo inakusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti kwa ajili ya utafiti wake na haijawahi kukusanywa na mtafiti mwengine yeyote kwa ajili ya utafiti. Vilevile, Kothari (keshatajwa) anaeleza kuwa data ya upili ni aina ya data ambayo hukusanywa kutoka katika maandiko na machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti. Madhumuni ya kukusanya data ya upili ni kujaliza data ya msingi kwa kushadidia hoja za data ya msingi wakati inapochanganuliwa. Data ya upili hukusanywa kutoka katika vitabu, makala, majarida, tasnifu, magazeti, tovuti na wavuti.

Katika utafiti huu aina zote mbili za data zilikusanywa. Data ya msingi ilikusanywa kutoka kwenye riwaya mbili za Kamugisha zilizotafitiwa. Riwaya hizi ni *Kitu Kidogo Tu!* na *Harusi ya Wendawazimu.*

Data ya upili ilikusanywa kwa kudurusu machapisho mbalimbali katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Pwani. Vitabu, Majarida, Makala na tasnifu mbalimbali zilizolingana

na mada ya utafiti huu zilisomwa kwa kina. Aidha, wavuti na tovuti mbalimbali zikiwemo za magazeti na za maktaba mbalimbali ulimwenguni zilisakurwa. Miongoni mwa maktaba hizi ni maktaba ya Chuo Kikuu cha Kenyatta, Chuo Kikuu cha Moi, Chuo Kikuu cha Nairobi na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

3.6 Mbinu za kukusanyia data

Kuna mbinu mbalimbali zinazoweza kutumika kukusanyia data ya utafiti. Searle (2012) anaeleza kuwa mtafiti huteua mbinu mojawapo ya kukusanyia data yake kulingana na malengo yake na vilevile muundo wa utafiti wake. Kwa misingi hii, mbinu iliyotumika kukusanyia data ya utafiti huu ni uchambuzi wa kimaudhui. Kwa mujibu wa Kothari (2008), uchambuzi wa kimaudhui ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambayo humpatia mtafiti data baada ya kusoma kwa kina matini iliyoteuliwa kutafitiwa. Katika kusoma huko ndipo mtafiti hukutana na sehemu inayohusiana na malengo ya utafiti wake. Kwa kuwa data ya utafiti huu ni kauli na matendo ya wahusika yenye sifa za udhanaishi, mtafiti alivisoma kwa kina vitabu vilivyotafitiwa. Kisha, wahusika ambao matendo au kauli zao zilidhihirisha sifa za mhimili fulani wa udhanaishi waliorodhoshwa chini ya mhimili huo na baadaye kuchanganuliwa. Vile vile mtafiti alisoma tafiti mbalimbali za awali na Makala zilizohusiana na utafiti huu ambazo zilimsaidia kutoa maelezo zaidi katika utafiti wake.

3.7 Vifaa vya kukusanyia data

Utafiti huu ulikusanya data kwa kutumia kifaa cha kukusanyia data kiitwacho usomaji. Kifaa cha usomaji kilitumiwa na mtafiti alipokuwa akifanya utafiti wake maktabani. Katika usomaji huo, vitafitiwa mbalimbali vilisomwa, zikiwemo riwaya mbili za Kamugisha: *Kitu Kidogo Tu!* na *Harusi ya Wendazimu* zilizotoa data ya msingi. Data iliyokusanywa kwa kutumia kifaa hiki cha usomaji ilinakiliwa kwenye tarakilishi

ilipohifadhiwa na hatimaye kuchanganuliwa. Aidha, data ya upili ilikusanywa kutoka kwenye vitahiniwa vyengine mbalimbali kwa kutumia kifaa hiki cha usomaji. Vitafitiwa hivi ni kama majarida, Makala, tasnifu, vitabu, wavuti na tovuti mbalimbali. Vilevile, data hii ya upili ilihifadhiwa kwenye tarakilishi na hatimaye kutumiwa kushadidia hoja wakati wa uchanganuzi wa data.

3.8 Uchanganuzi wa data

Utafiti huu ni wa kithamano. Hivyo, data iliyokusanywa ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya kimaelezo katika lugha nathari. Kwanza, mhimili wa nadharia ya udhanaishi uliorodheshwa na maelezo ya kufafanua mhimili huo pia yakatolewa. Chini ya mhimili huo, wakaorodheshwa wahusika mbalimbali kutoka riwaya zote mbili ambao matendo na kauli zao zilidhirisha sifa za mhimili huo wa udhanaishi ulioorodheshwa. Kisha, hayo matendo na kauli za wahusika hao zikachanganuliwa kudhihirisha jinsi udhanaishi unavyojitokeza. Jedwali lifuatalo ni mfano mwafaka wa jinsi data ilivyochanganuliwa:

Jedwali 3.1: Mfano mwafaka wa uchanganuzi wa data

Mihimili	Maelezo
1. Utamaushi. Kwa kuwa mwanadamu hana uwezo juu ya masuala kama maumivu na mateso, anaweza kukata tamaa. Njia moja ya kuonyesha kukata tamaa ni kujitoa maisha mwenyewe kama wanavyofanya wahusika wafuatao kutoka riwaya za Kamugisha;	**a. Katoto** Katoto, mhusika katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* alijitoa uhai kwa kujitia kitanzi kwa ugumu wa maisha kama anavyoeleza mwandishi; *… Katoto wa Minane alikuwa ananing'inia kwenye kamba huku kichwa chake kimeinama upande wa bega la kushoto.* Mwandishi anaendelea kusema; *Bwana katoto kajitoa roho mweyewe…* **b. habusu** Abdu akimnukuu habusu mwenzake: *"… Nakumbuka usiku wa siku ya mwisho aliniita akaniambia, "Abdu unajua nina mke na watoto watatu," akasema, 'ukijaaliwa kurudi nyumbani wape salamu hizi, salamu za mwisho. 'Nikamuuliza kwa nini alikuwa anasema hivyo, akanijibu kuwa usiku ule alitarajia kulala usingizi wa mwisho. Nilimkataza asiendekeze mawazo hayo. Kesho yake asubuhi alikutwa ananing'inia chooni. (uk. 124)*

3.9 Uwasilishaji wa data

Data ya utafiti huu ilikusanywa, ikachanganuliwa na kisha ikawasilishwa kwa njia ya kimaelezo. Data iliwasilishwa kwa njia ya kimaelezo kwa sababu utafiti ulikuwa wa kithamano. Kwanza kabisa iliorodheshwa mihimili mbalimbali ya udhanaishi na maelezo yakatolewa kuhusu mihimili hiyo. Pili, waliorodheshwa wahusika ambao kauli na matendo yao yalilingana na mihimili iliyoorodheshwa. Kisha maelezo yakatolewa kuhusu jinsi sifa za mihimili iliyotajwa zinavyojitokeza katika matendo na kauli hizo. Maelezo yote haya yalitolewa kwa uzingatifu mkuu wa malengo ya utafiti wenyewe.

3.10 Uaminiki na utegemewaji wa utafiti

Uaminiki wa utafiti unatokana na kuwa mtafiti ametumia mbinu za utafiti zilizo mwafaka kiakademia kiasi kwamba endapo utafiti huo utafanywa tena katika mazingira yaleyale, kupitia vifaa vilevile vya utafiti basi utatoa matokeo sawia.

Mbinu iliyotumika kukusanyia data ya utafiti huu ni uchambuzi wa kimaudhui unaohusisha usomaji wa matini lengwa kwa kina huku ukizingatia malengo ya utafiti. Kwa kuwa data ya utafiti huu ni kauli na matendo ya wahusika yenye sifa za udhanaishi, mtafiti alivisoma kwa kina vitabu vilivyotafitiwa maktabani. Kisha wahusika ambao matendo au kauli zao zilidhihirisha sifa za mhimili fulani wa udhanaishi waliorodhoshwa chini ya mhimili huo kabla ya kuchanganuliwa kwa njia ya maelezo.

3.11 Maadili ya utafiti

Kwa mujibu wa Kumar (1999), miongoni mwa vitu muhimu anavyopaswa kuzingatia mtafiti ni maadili ya utafiti yanayohusu kupata kibali cha utafiti pamoja na kutunza siri za watafitiwa. Kwanza kabisa, mtafiti alipata barua rasmi na cheti cha maadili kutoka katika kamati ya maadili ya Chuo Kikuu cha Pwani. Stakabadhi hizi zilitoa idhini rasmi ya kuruhusu utafiti huu ufanyike. Pili, mtafiti alihakikisha kuwa dondoo zote

zimenukuliwa kwa usahihi na vyanzo vya data ya upili kunukuliwa ipasavyo ili kuepuka wizi wa mawazo na maandishi ya kiakademia. Tatu, baada ya utafiti kukamilika, tasnifu iliwasilishwa katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Pwani ilikotahiniwa ili kubaini iwapo mtafiti hakunakili kazi za watafiti wengine na kuzifanya zake, kitendo ambacho ni kinyume na maadili ya kiakademia. Tasnifu hii ilipita mchujo huo.

3.12 Kihitimisho

Katika sura hii mtafiti ameeleza kuhusu mbinu za utafiti zilizotumika kuendesha na kufanikisha utafiti huu. Mambo yaliyoelezwa ni muundo wa utafiti, usampulishaji wa data, mbinu za ukusanyaji wa data, vifaa vilivyotumika kukusanyia data, jinsi data iliyopatikana ilivyochanganuliwa, uwasilishaji wa data, uaminiki wa utafiti na maadili ya utafiti huu.

SURA YA NNE

UWASILISHI NA UCHANGANUZI WA DATA

4.1 Kitangulizi

Katika sura hii, data iliyokusanywa ilichanganuliwa na kuwasilishwa. Mtafiti alizisoma kazi hizo mbili za Kamugisha- *Kitu Kidogo Tu!* na *Harusi ya Wendawazimu* kisha kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya udhanaishi, akaeleza matendo na kauli za wahusika zinazoonyesha sifa za mihimili hiyo. Mihimili (vipengele) hii iliyojitokeza katika riwaya hizi mbili ni uhuru, swala la Mungu, kifo, ukengeushi, utamaushi, kuabudu mahitaji ya kimwili na utupu/ubatili. Mihimili iliorodheshwa na ikafafanuliwa. Baada ya mhimili kufafanuliwa, waliorodheshwa wahusika ambao kauli au matendo yao yanaendana na sifa za mhimili huo na ufafanuzi ukatolewa pia. Mhimili wa kwanza kufafanuliwa ni uhuru kama ifuatavyo:

4.2 Uhuru wa mtu binafsi

Katika udhanaishi, kuwa huru ina maana kuasi dini na sheria zake zote zinazojaribu kumwambia binadamu namna ya kuishi maisha yake. Kuasi mila na desturi ambazo zinajaribu kumfungia mtu kwa kumtaka aishi maisha ya namna fulani. Kwa hivyo binadamu anapoamua kuwa huru huwa ameamua kukengeuka na kila kitu kinachojaribu kumwekea sheria na mipaka ya mambo na maamuzi anayoweza kuyafanya katika maisha yake. Anaweza kuiasi hata nafsi yake.

Osore (2008) anasema, “Kwa Wakristo, Bibilia ni kitabu kitakatifu chenye sheria zilizowekwa na Mungu… kina masharti ya kufuatwa na kuwachwa na Mkristo. Aidha, Bibilia inasema kuhusu madhara ya kutenda dhambi”.

Hali ni ii hii kwa Waislamu na Kurani yao. Kama ilivyo Bibilia, Kurani nayo ni kitabu cha dini kilichojaa sheria zinazofaa kufuatwa na mwanadamu ili asimkosee Mungu

wake. Kwa hivyo, kuwa muumini kuna maana kuwa kuna sheria zinazokunyima uhuru wa kufanya mambo mengine.

Katika riwaya hizi mbili za Kamugisha, kunao wahusika wanaodhihirisha kuwa wanathamini uhuru wao zaidi na wanakana mila na desturi za jamii na dini zinazojaribu kuwanyima uhuru wa kuishi wanavyotaka wao. Kauli na matendo ya wahusika wafuatao zinaonyesha jinsi wanavyopigania uhuru wao na wanavyoenda kinyume na mila za jamii na sheria za dini.

4.2.1 Zamda apigania uhuru wa kujiamulia

Katika *Harusi ya Wendawazimu*, tunakutana na msichana Zamda ambaye anaamua kuasi na kupuuza kila kitu kinachojaribu kumwekea mipaka katika uhuru wake. Linapozuka jambo la ndoa kwake na dadake Yasmin, Zamda anatokea kudharau sheria za dini kuhusu swala hilo na hata anaamua kumtusi babake anapojaribu kuleta tofauti ya dini kuzikataa posa zao. Dini ya Uislamu, ambayo ndiyo dini ya familia ya akina Zamda na Yasmin ina misimamo yake kuhusu ndoa. Mbali na kuwa swala hili bado lina mushkeli miongoni mwa maulama wa dini hiyo, imekubalika kuwa ndoa kati ya mwanamke Muislamu na mwanamume Mkristo au mtu yeyote ambaye si wa dini hiyo basi hairuhusiwi. Kurani 2:221;

"*Wala msiwaowe wanawake washirikina mpaka waamini… wala msiwaoze wanaume washirikina (wanawake Waislamu) mpaka waamini…"*

Katika kufafanua aya hii, mtafsiri anasema:

Ama Manasara na Mayahudi (ambao huitwa Ahlil Kitab- Wenye kupewa vitabu vya mwenyezi Mungu) inawajuzia wanaume wetu (Waislamu) kuoa wanawake wa kikwao. Lakini wanawake wa kikwetu hawaolewi na wanaume wa kikwao. Haramu kabisa na haisihi ndoa hiyo. (uk. 51)

Saad Mwendawazimu, baba yao akina Zamda, anapojaribu kuleta swala la tofauti ya dini kama pingamizi ya kukubali posa ya bintiye Yasmin kutoka kwa Garincha, Zamda ambaye hakuwa kwenye kikao hiki anaonyesha kughadhabishwa na jambo hili na waziwazi akakana mamlaka yoyote ya dini na hata ya babake katika jambo kama hili. Mwisho, anasema yuko huru kuwafahamisha tu kuhusu maamuzi yake na kwamba hajali kuhusu sheria hizo za dini wala za wazazi kujaribu kumzuia kuolewa na Chris. Zamda anaonyesha waziwazi kuthamini uhuru wa mtu binafsi kujiamulia maisha yake bila kufungwa na kigezo chochote. Yasmin anapoonyesha shaka kuhusu ombi la Garincha kutaka kumwoa katika kipindi cha wiki moja kuwa hakitakaa sawa kwa babake, Zamda anapuuza mamlaka hayo ya babake kama inavyodhihirika katika kauli ifuatayo:

"*Na kuhusu swala la baba vilevile sioni kama ni kikwazo, anayeolewa ni wewe wala siyo yeye…"* (uk. 60).

Baadaye pia Yasmini anapoonyesha wasiwasi wa kumkabili Garincha baada ya Garincha kukosana na baba yao, Zamda bado anasawiriwa akimpuuza babake na mamlaka yake:

"Yasmin namna gani?" Alisema Zamda. "Kwani Garincha hajui kuwa siyo wewe uliyemtukana, kama anakupenda atakuoa, baba kitu gani?" (uk. 99)

Kwa mara nyengine Zamda anapuuza mamlaka ya babake. Huku ni kusema kuwa mamlaka ya babake juu yake hayafai kuyaathiri maamuzi yake Zamda na kumnyima uhuru wake wa kujiamulia. Huku ni kuthamini uhuru wa mtu binafsi.

Na hata anapogundua baba yake amemtusi Garincha, Zamda anakuja juu na kumtusi babake na kupuuza mafunzo ya dini kuhusu uharamu wa ndoa na mtu asiye Muislamu kama inavyodhihirika:

“Baba anasema nini? Yeye ni nani kumhoji juu ya dini yake? Nauliza yeye ni nani? Kwa nini kutuingilia? Yeye alipomwoa mama nani kati yetu aliyemuingilia. Ningejua kabla hajaondoka ningemwambia usoni mwake. Ngoja aje alogwe kesho aniulize mimi! Nini mambo ya dini, mambo ya mahari kwani ni yeye anayeolewa? Hana shukrani. Hivi baba anaishi enzi gani enzi ya ‘kompyuta’ au enzi za Sultani Kipingo?... baba kitu gani?” (uk. 98)

Kwa maneno haya, Zamda ameonyesha kuwa anachojali zaidi ni uhuru wa maamuzi yake na hajali kuhusu dini au wazazi. Anamshawishi ndugu yake pia kumpuuza babake na kufuata moyo wake kufanya maamuzi yake. Zamda anasingizia mabadiliko ya enzi, kuwa kitambo ndiko watu walipofuata sheria hizo za dini na wazazi ila si enzi zao za *kompyuta.* Enzi hizi kila mtu anafaa kuwa huru kufanya maamuzi yake.

Lakini dini kwanza inasisitiza kuhusu umuhimu wa wazazi na inaamrisha wafuasi wake wawaheshimu katika kila jambo isipokuwa watakapoamrishwa kumshirikisha Mwenyezi Mungu, na kwa hili pia Kurani inasema uwakatalie lakini kwa upole wala usiwakosee heshima na kupaza sauti yako juu ya sauti zao, usiwaambie hata *Ah!* yaani hata usiwagunie;

“*Na Mola wako amehukumu kuwa msimwabudu yoyote ila yeye tu. Na (ameagiza) kuwafanyia wema (mkubwa) wazazi. Kama mmoja wao akifikia uzee, (naye yuko) pamoja nawe au wote wawili basi usiwaambie hata Ah! Wala usiwakemee. Na useme nao kwa msemo wa hishima (kabisa).” (Kurani 17:23).*

Unaweza kukengeuka ukakana vipengele fulani vya dini na mila za jamii, na unaweza kukengeuka ukaamua kuwa huru kabisa. Zamda amekengeuka kabisa, hivyo anathamini uhuru wake kuliko kitu chengine chochote. Hajali mafunzo ya dini na athari yake juu yake, wala mamlaka ya wazazi wake.

Kuwa huru husababishwa na migogoro ya mtu na nafsi yake kwanza. Kabla mtu yeyote hajajitokeza kuanza kupinga kaida, mila, desturi na mfumo wa kawaida ambao jamii aliyomo imefuata bila kujua namna nyengine ya kufanya mambo kwa muda mrefu, kwanza lazima aishinde migogoro na nafsi yake. Mazoea yana tabu. Anapopata ujasiri wa kuikanya nafsi yake na kuielekeza katika uhuru anaotaka yeye ambao mara nyingi huwa kinyume na mazoea ya jamii alimokulia ndipo kisha huamua kujitokeza na kupinga mila na desturi na kuchagua kufuata uhuru wake. Kupigana na jamii ndio kazi yenyewe kwa sababu ya imani zilizowekwa.

Kwa mfano, kwa kupinga na kukataa kufuata amri ya wazazi tu hukusababishia kupata laana sembuse kuwatusi kama anavyofanya Zamda. Zamda aliishia kupata tabu katika ndoa yake. Chris alirudiana na Eliza na akawa hamjali tena Zamda, akawa kazi ni kumfokea. Pengine kuwa hivi ni sadfa tu, kwa sababu si hata Yasmin anasawiriwa akiishi vyema na mumewe Garincha aliyemtusi babake. Lakini pia inapotokea kuwa kama ilivyotokea kwa Zamda katika jamii itasemekana ni laana ya babake inayomfanya ateseke. Meursault, katika *The stranger* ya Albert Camus (1942) anaishia kuhukumiwa kinyongo kwa kosa la mauaji lakini sababu iliyomfanya hakimu kushawishika haikuwa ya mauaji bali tabia alizokuwa nazo hasa katika mazishi ya mamake. Meursault hakuonyesha hisia zozote za huzuni alipohudhuria mazishi ya mamake. Hakutaka kuona maiti yake, akavuta sigara kando ya jeneza yake, akanywa kahawa, hakulia na mazishi yalipoisha hakusubiri ila alirudi moja kwa moja kwake nyumbani. Siku iliyofuata akaenda kuogelea na mpenzi wake mpya na akaendelea na maisha yake kana kwamba hakukutokea chochote. Kaida za jamii nyingi ni kuwa wanatarijia unapopoteza mtu wa karibu kama mama mzazi unafaa kuomboleza kwa muda. Kwa mfano katika jamii ya Waduruma *“unazagazwa”,* yaani unaketishwa, ukae na usiinuke ila kwa mambo muhimu kama kwenda msalani wakati wote wa matanga, na matanga mengine

yalichukua hadi wiki moja. Usipokaa muda huu ima kwa kupuuza au hata kwa kukosa nafasi jamii inaamini kuwa utarukwa na akili uwe kichaa. Meurslaut yeye aliangukia adhabu ya kifo na Zamda alijipata katika ndoa ya mateso. Hata hivyo, Ingo Elbe (2020) anasema mtu anapokuwa huru kufanya maamuzi, matokeo si muhimu. Cha muhimu ni kuwa mtu amefanya maamuzi bila kufungwa na mila wala kaida zozote zinazonyima mtu uhuru wake wa kufanya maamuzi hayo.

Gwachi Mayaka (1991) anawataja wahusika kutoka kazi nyengine bunilizi waliokosana na wazazi wao wakafukuzwa nyumbani walipohitilafiana nao kimawazo hasa katika utamaduni na dini. Wahusika hawa ni Rosa katika riwaya ya *Rosa Mistika* (1974) ya E. Kezilahabi anayemfokea babake anapojaribu kukanywa dhidi ya kutembelewa na wanaume nyumbani kwao. Aidha, Mayaka (keshatajwa) anamtaja Joshua wa riwaya ya *The River Between* (1965) ya N. Wa Thiong'o anayewafukuza binti zake wawili-Muthoni kwa kushiriki ukeketaji unaopingwa na dini yake ya Kikristo na Nyambura anayesuhubiana na Waiyaki ambaye bado hajaokoka. Wahusika hawa wanakosana na wazazi kwa kujitafutia uhuru wa kujiamulia kama afanyavyo Zamda katika *Harusi ya Wendawazimu.* Ni wazi kuwa imani kwa Mungu huleta utengano baina ya binadamu na matendo au hata nafsi yake. Hii ni aina ya ukengeushi wa kisaikolojia.

Kwa watamaushi, ukengeushi ni hali ya kuonyesha migogoro ya ndani kwa ndani katika mtu binafsi kuonyesha hiari na uchaguzi wake wakati anapopambana na nguvu hatari ambazo zinajaribu kummeza na kumwangamiza. Satre (keshatajwa) anaiita hali hii 'Mtu akiwa na upweke katika umati wa watu'. Katika jamii, kuna miiko na maadili ambayo ni lazima yafuatwe na wanajamii wote. Wakati wowote yanapovunjwa, anayehusika anaweza kufukuzwa kutoka katika jamii hiyo ama kutengwa. Haya yanatokana na tamaduni mbili zinazohitilafiana - utamaduni wa jadi na ule wa kisasa.

Ili kukwepa migogoro hii inayosababishwa na watu kujitafutia uhuru katika jamii, Tariq (2017) anasema kuwa ijapokuwa ni muhimu kujiamulia, hatuwezi kukwepa ukweli wa mazingira tulimozaliwa na kukulia, hivyo basi tunapofanya maamuzi tutumie akili na tuzingatie hayo.”

4.2.2 Maimuna (shangazi la Zamda na Yasmin) atetea uhuru wa vijana kujiamulia

Maimuna ni shangazi la kina Zamda na Yasmin katika riwaya ya *Harusi ya Wendawazimu*, ndiye aliyekuwa akikaa nao mjini. Maimuna anasawiriwa kama mtu ambaye hakuwa na budi ila kukubali kuwa nyakati zimebadilika na vijana wako huru kufanya mambo yao. Hii ndio sababu aliwaachilia wasichana wa Kiislamu kualika wanaume kwake, kuwapikia na kuwanunulia pombe wanywe na kuwaacha wapelekwe densi za usiku. Maimuna alipoongea na kakake, Saad, alikiri kuwa vijana wako huru kufanya mambo yao na kujiamulia na kuwahusisha wazazi ni wao wenyewe kutaka. Maimuna alitetea uhuru wa Zamda na Yasmin kufunga ndoa na wanaume wasiokuwa waislamu;

“Watoto wa siku hizi wanajiamulia, kutufahamisha ni heshima wala si wajibu, mimi nawatetea.” (uk.88)

Maimuna anatetea waziwazi uhuru wa vijana kujiamulia. Uhuru wa kujiamulia ni sifa kuu ya udhanaishi. Kulingana na Sartre (1945), mwanadamu anafaa kufanya maamuzi yake bila kuathiriwa na kaida au sheria zozote zinazofuatwa na jamii hiyo.

Tunaweza kusema kuwa tofauti na Saad aliyeishi vijijini, Maimuna aliishi mjini na Zamda na dadake Yasmin. Pengine kuishi mjini miaka mingi kulimfanya azoee kuwa utamaduni unabadilika na akakubali mabadiliko hayo. Tofauti na kakake ambaye ndio mara ya kwanza kukumbana na mabadiliko hayo kupitia posa za binti zake wawili. Posa zenyewe zilipelekwa siku chache tu kabla ya harusi, kinyume pia na tamaduni za

kitambo ambapo posa ingepelekwa kisha watu wakapewa muda wa kupanga harusi na kujumuika na ndugu, jamaa na marafiki kusherehekea ndoa hiyo.

Saad akizungumza kuhusu watoto wake, Zamda na Yasmin anagusia swala la uhuru ambao vijana wanautaka sana. Kwa uhuru huu, vijana wanapuuza mila zote na kufanya mambo kulingana na vile wanavyotaka hao. Saad anauliza ni wasichana gani wanaojitayarisha kuolewa ila hawakai nyumbani wakatawa ila wanazunguka na wanaume usiku. Saad anasema wasichana wa siku hizi wala hawana ndoa ila ni malaya kwa sababu wanapenda kula na kulala na vijana ovyoovyo.

Hata hivyo, mawazo haya ya Saad ni tofauti na ya dada yake Maimuna ambaye waziwazi anatetea uhuru wa vijana kujiamulia lolote watakalo. Ingawa uhuru huo unaenda kinyume na maadili ya jamii na sheria za dini, bado maimuna anasema ni haki yao vijana.

4.2.3 Mariam- mwanafunzi wa Buda abadili maumbile yake

Kulingana na udhanaishi, mtu yuko huru kufanya na kuwa chochote anachotaka kuwa. Katika *Harusi ya Wendawazimu,* Mariam aliyekuwa mwanafunzi wa Buda na aliyesoma na Tina anasawiriwa kuwa alijichubua na kubadili rangi ya ngozi yake kwa madawa na kuwa mweupe. Tina anamwambia mwalimu wake Buda;

"Ndiyo ni Mariam naye tulikuwa naye Maneromango… Yeye si chotara bali amebadili ngozi yake, hasa uso kwa kutumia madawa, na nywele ni dawa wala si za bandia." (uk. 147)

Mariam anaamua kutumia uhuru wake kujichubua na kubadili rangi ya ngozi yake. Aina hii ya uhuru pia tunaiona katika nchi za magharibi kama vile Marekani. Kwa uwezo mkubwa wa kiteknolojia uhuru huu wa kubadili maumbile unafanywa kwa kufanyiwa upasuaji wa kuwekwa plastiki. Kunao kama msanii Michael Jackson aliyechonga pua,

akabidili ngozi ikawa nyeupe kama ya mzungu mweupe na akaweka na nwyele za singa. Wanawake nao hufanyiwa upasuaji wa kufurisha maziwa yao, makalio na kunao pia wanaochagua kupunguzwa mbavu ili wapate umbo kama la vibonzo vya katuni. Kunao pia waliozaliwa wanaume wakafanyiwa upasuaji wa kuwabadilisha kuwa wanawake. Mfano mzuri ni Caitlyn Jenner wa Marekani. Yote haya yanatokana na kuwa kila mtu yuko huru kufanya anachotaka bila kubanwa na sheria zozote za dini wala jamii. Katika *Harusi ya Wendawazimu,* Mariam- mwanfunzi wa Buda ametumia uhuru wake kujibadili maumbile.

4.2.4 Msichana wa gauni la rangi ya bahari anakataa ndoa

Siku ya harusi, katika riwaya ya *Harusi ya Wendawazimu,* Saad Mwendawazimu alikuwa nyuma ya msichana mmoja aliyekuwa akimwambia mvulana aliyekuwa naye kuwa ndoa haiwezi. Hii ina maana kuwa aliamua asingeolewa. Ila mwili una mahitaji yake, kumaanisha angetaka kuzima mahitaji ya mwili wake basi angeamua kujihusisha na mapenzi nje ya ndoa, kitu ambacho bado hakijakubalika kuwa cha heshima au cha kawaida katika jamii za Kiafrika, na aidha ni dhambi katika dini. Lakini huyu msichana ameamua kuwa huru, kinyume kabisa na tamaduni Kiafrika, na haswa kinyume kabisa na dini;

"Harusi za Dar es Salam zinakuwa nyingi kwa sababu ndoa zinadumu majuma au miezi wala sio miaka. Ndoa mimi siiwezi, nionavyo, harusi ni nzuri kama ni ya mwingine siyo yako." (uk. 115).

Ndoa bado ni sehemu muhimu katika jamii haswa ya Afrika. Ili ndoa ifungwe huwa na sheria zake mahsusi. Aidha ndoa huwa na sheria zake zinazowafunga wanandoa ndoani. Kwa wadhanaishi, mwanadamu hafai kufungwa kwa sheria yoyote ile. Anafaa kuwa huru kabisa kufanya chochote anachotaka. Kunao baadhi ya wadhanaishi kama Sartre na Simon de Boviour ambao waliamua kutoingia ndoani kama huyu msichana wa gauni la

rangi ya bahari. Yote haya ni katika juhudi za kujitafutia uhuru. Simon de Boviour katika kitabu chake *The Second sex* (1949) alisema kuwa kila mtu yuko huru kujiamulia anayetaka kulala naye, wanaume wakitaka kuoana ni sawa na wanawake wakitaka kuoana pia ni sawa, uhuru wanao. Watu hawafai kujinyima uhuru kwa kujifungia ndoani.

4.2.5 Chris haiheshimu ndoa yake

Kama walivyokuwa Sartre na Simone de Beauvoir kushiriki ngono kiholela, Chris katika *Harusi ya Wendawazimu* anasawiriwa kama mtu ambaye haheshimu ndoa yake na Zamda muda mfupi tu baada ya harusi. Chris alirudia uhusiano wake na Mariam mtalaka wa Musa, mwanamke ambaye alikiri kuwa wasingefumaniwa na Musa aliyekuwa ni mume wa Mariam wakati huo basi asingefikiria kuhusu ndoa;

Alimwona Mariam, akajisemea kuwa kama haingekuwa kufumaniwa kwake mwanamke yule labda hangeamua kuoa. (uk. 113)

Hii ni kumaanisha kuwa Chris alikuwa ametosheka na jinsi maisha yake yalivyokuwa na alikuwa anaufurahia uhuru wake wa kushiriki mapenzi na wanawake tofauti bila kuingia ndoani nao. Wakati huu tayari alikuwa na Zamda kama kimada wake. Na hata baada ya ndoa aliendelea na tabia hii. Alikuwa na Eliza na Mariam kama vimada;

"*…Siku hizi Chris anakwenda kwa Zamda kubadili nguo labda na kufoka ili asisahaulike kama yeye ndiye mwenye nyumba. Siku zote utamkuta kwa Eliza, Jumapili kwa Mariam akikandwakandwa."* (uk. 158)

Chris asingefumaniwa kwa Mariam mke wa Musa wala asingefikiria kuoa. Tushaona kuwa udhanaishi unapinga asasi hii ya ndoa kwa jinsi inavyomnyima mtu uhuru wa kushiriki ngono na yeyote amtakaye. Na Chris japo alikuwa ndoani na Zamda, hakuithamini ndoa hiyo, bado alijiona yuko huru kushiriki ngono na Eliza na Mariam.

4.2.6 Musa Nshomile analaani dini kwa kumnyima uhuru

Katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* mhusika Musa Nshomile anapomchumbia Stella, ambaye ni mlokole, anaonyesha wasiwasi juu ya vikwazo vinavyowekwa na tofauti kati ya dini yake ya Kiislamu na dini ya Stella ya Ukristo.

Musa alilaani tena ulokole. Hata hivyo, maelezo ya Stella yalikuwa yakitia matumaini. 'Madhali hakukataa moja kwa moja yumkini angekubali. Wasiwasi wake ulikuwa suala la dini. hata kama Stella angeafiki je baba yake kweli angekubali mtoto wake aolewe na muislamu? Au atamtaka Musa abadili dini?' Musa aliwaza. (uk. 95)

Hapa, dini inaonekana kama taasisi inayomnyima mtu uhuru hata kujiamulia kuhusu mchumba wake maishani. Kwanza Stella anakataa kumjibu Musa ombi lake akitarajia uamuzi huu atafanyiwa na Mungu. Kisha bado kuna swala la tofauti ya dini ambalo linampa Musa Nshomile wasiwasi iwapo babake Stella, mwalimu Tadeo ataridhia muungano wao au dini itatumika kama kikwazo. Sartre (1945) anasema udhanaishi ni nadharia inayosisitiza vitendo. Mwanadamu anafaa kufikiri na kuamua matendo na awe tayari kukumbana na matokeo ya maamuzi na matendo yake. Hapa tunamwona Stella anashindwa kuamua kukubali uchumba wa Musa Nshomile hadi apate ufunuo kutoka kwa Mungu, anashindwa kufanya maamuzi katika maisha yake. Mafunzo ya dini yanamnyima hata uhuru wa kufikiri na kujifanyia maamuzi yake kuhusu mume wa kuishi naye.

4.3 Swala la Mungu

Swala la kuwepo au kutokuwepo kwa Mungu ni moja kati ya mihimili inayojadiliwa sana na wadhanaishi. Kuna wadhanaishi kama Kierkagaard (1813-1855) wanaoamini uwepo wa Mungu na wanashikilia kuwa maisha ya mtu yana maana jinsi yalivyo, na kuwa tunaweza tusielewe ila Mungu mwenyewe anajua maana hiyo. Hivyo mwanadamu asikate tamaa, awe na imani kwa sababu imani kwa Mungu pekee huyapa maisha

maana. Kierkagaard (keshatajwa) anaiita imani hii *the leap of faith.* Hata hivyo, kuna wadhanaishi kama Nietzsche (1844-1900) na Sartre (1905-1980) wasioamini uwepo wa Mungu. Wanashikilia kuwa mwanadamu ana jukumu la kutafutia maisha yake maana na kwamba yuko huru kuyapa maisha yake maana yoyote anayotaka yeye kwa kuishi anavyotaka, bila kujali kuwa ataadhibiwa siku ya kiama. Kwao, Mungu alikufa kwa hivyo hakuna wa kuwauliza chochote. Hawa mara nyingi hutoa kauli kama "Mungu amekufa" au kukejeli uwepo wake kwa kusema amezeeka wala hawezi tena kufanya majukumu yake juu ya viumbe vyake.

Nanjala (2015) anasema udhanaishi ni falsafa inayozungumzia uhusiano uliopo kati ya mtu na Mungu na iwapo mtu anapaswa kuamini kuwepo kwa Mungu. Kierkegaard (keshatajwa) anaeleza tatizo la ubinafsi wa binadamu kutokana na imani ya kikristo. Katika kitabu chake *Fear and Trembling* (1983), Kierkegaard anatoa ubishi kwamba falsafa ya maisha huwa na maana mtu anapotii malimwengu. Kulingana naye binadamu anatambua maana katika maisha kwa kufanya yanayompendeza Mungu, atahakikisha matendo yake yanatii maadili yanayoamrishwa na malimwengu.

Katika riwaya hizi mbili za *Harusi ya Wendawazimu* na *Kitu Kidogo Tu!* tunakutana na wahusika wa mirengo yote hii miwili. Kunao waliokata tamaa na matatizo yanayowakumba na wakaishia kumkana Mungu kama ilivyokuwa na wadhanaishi wa awali ambao vita vya dunia na matatizo yaliyotokana na vita hivyo yaliwafanya kukata tamaa na kusema kuwa Mungu amekufa. Aidha kunao wahusika katika riwaya hizi mbili ambao bado wanashikilia thabiti imani katika Mungu na wanamwomba wakitarajia ajibu maombi yao na kuziondoa shida zinazowakumba na kuikumba nchi nzima ya Tanzania. Wahusika hawa ni wafuatao;

4.3.1 Mzee (kwenye basi la kwenda Bukoba) amkana Mungu

Fredrick Nietzsche na Jean Paul Sartre ni wadhanaishi wanaojulikana zaidi kwa mawazo yao ya kumkana Mungu. Nietzsche aliudhika na jinsi kanisa la kikatoliki lilivyokuwa likiendesha mambo yake, hivyo akaamua kujitenga nalo na hatimaye kudai kuwa Mungu amekufa na kanisa ndilo kaburi lake, kwa hivyo binadamu wako huru. Sartre naye, alitatizwa na matatizo binadamu wanayojisababishia wenyewe kama ubaguzi wa rangi, ukoloni na vita vya dunia ambavyo viliua mamilioni ya watu bila Mungu kuingilia kati. Kwa kuwa Mungu aliwaacha binadamu watesane namna hiyo bila kuingilia kati, Sartre hakuona umuhimu wowote wa Mungu katika maisha ya binadamu kwa hivyo akaamua kumkana pia yeye. Sartre (1965) alidai kuwa hakuna Mungu na hivyo basi hakuna silika imara ambayo humshurutisha binadamu kutenda jambo fulani. Anamtazama binadamu kama mwenye kuwajibika kwa matendo yake lakini mwenye upweke katika uhuru unaoogofya wa kuchagua na kujiendeleza katika ulimwengu usiokuwa na maana. Tofauti na wadhanaishi wanaomwamini Mungu mwenye uwezo mkubwa wa kutatua matatizo ya wanadamu, wadhanaishi wa ukanaji Mungu wanapingana na imani ya kumtegemea Mungu ili kuwatatulia matatizo yao.

Katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* mhusika Mzee ambaye alikuwa akisafiri na Musa kwenye basi la kwenda Bukoba, anaonyesha tashwishi katika uwepo wa Mungu kama alivyofanya Sartre (Keshatajwa). Tashwishi yake inatokana na matatizo anayoyapata na yanayowakumba Watanzania wote kwa jumla. Mzee anaonyesha shauku iwapo Mungu yupo, na kama yupo basi ana shauku juu ya nguvu na uwezo wake kama Mungu. Kulingana naye, kama Mungu yuko basi amezeeka vibaya hivyo hana uwezo tena juu ya viumbe vyake. Mazungumzo yake na mhusika Musa Nshomile ni kama hivi;

Katika mazungumzo hayo, Musa anasema:

“Naona tunapitia kipindi kigumu.”

Yule Mzee akasema kuwa Siyo kipindi kigumu bali Mungu amezeeka. Tena amezeeka vibaya. Tayari kapofuka, haoni tena yanayotendeka hapa duniani. Maskio yake nayo yameziba, hawezi tena kuskia kilio chetu. Hata pua zake nazo zimeziba. Hawezi kunusa uozo ulioko hapa.

Baada ya kufikiria imani yake na ya akina Stella, Musa akasema:

"Hapana, Mungu yuko na anayaona yote na atatusaidia."

Yule Mzee akajibu;

Labda yupo! Kama yuko basi ametusahau, ametupa kisogo. Pengine anatuadhibu kwa makosa ya kusingiziwa; kwani tumekosa nini? Au tunaadhibiwa kwa makosa ya baba zetu! Angalia, gonjwa hili la UKIMWI linavyodondosha watu wa mkoa huu, wakubwa kwa wadogo, bila huruma. Hapana, Mungu wetu hayupo, kama yupo kalala, kazeeka. (uk. 100)

Huyu Mzee anatilia shaka uwepo wa Mungu kwa sababu haoni msaada wake katika matatizo yote ambayo Watanzania wanapitia. Haya ndiyo mawazo ya wadhanaishi wasioamini Mungu na hawaogopi kumkana au kumkejeli wanapopata nafasi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Nagona* (1990) pia Kezilahabi anamkejeli Mungu kwa kauli ii hii kuwa Mungu amezeeka;

"Atakuwa naye amezeeka kutuwekea mtego huu mara ya pili." Nilipiga kelele; "Hakuna shetani wa kunichumia haya matunda nikala? Hakuna dhambi ya asili!" (uk.22)

Kezilahabi, kama huyu Mzee katika gari la kuelekea Bukoba anamkejeli Mungu kwa kusema amezeeka, na pia anaikejeli dhambi ya asili kama ilivyo katika Bibilia. Hata anaitisha msaada kwa Shetani ambaye anafaa kuwa adui wa binadamu kwa ulaghai wake na kumshawishi binadamu kujiingiza katika maasi yasiyopendwa na Mungu. Huyu Mzee katika gari la kuelekea Bukoba anaonyesha kuwa hana imani tena kabisa katika

uwepo wa Mungu na uwezo wake juu ya matendo ya binadamu. Kusema amezeeka vibaya hata haoni tena, hasikii tena na wala hawezi hata kunusa ni kuonyesha anavyomdunisha Mungu. Kuwa Mungu hawezi tena kufanya lolote, hata yale mambo ya kawaida binadamu wanayofanya kwa urahisi. Huku ni kumdunisha na kukejeli utukufu wake.

4.3.2 Katoto wa Minane anakufa bila dini

Katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* kuna mhusika Katoto wa Minane. Katoto wa Minane alikuwa Mrundi wa Gitenda aliyekimbia vita vya wao kwa wao huko kwao baada ya jamaa zake wote kuuawa katika vita. Tangu wakati huo, Katoto amekumbwa na matatizo hadi mwisho wake alipojiua. Wakati wa mazishi yake, inabainika kuwa katika wanakijiji wenzake wote hakuna hata mmoja aliyekuwa na ufahamu kuhusu imani ya dini ya Katoto. Ni makisio yetu kuwa matatizo yale yalimfanya Katoto asijihusishe tena na imani za dini, kama ilivyokuwa kwa wadhanaishi wa awali huko magharibi waliokengeushwa na vita vya dunia kama tulivyotangulia kueleza.

Wanyarwanda walikuwa na imani kuwa Mungu angezunguka ulimwenguni kote wakati wa mchana ila usiku angerudi kulala Rwanda. Waliamini kuwa wao walikuwa vipenzi vya Mungu. Ila miaka ya tisini kulikuwa na vita vya wenyewe kati ya Watutsi na Wahutu vilivyosababisha vifo vya takribani watu laki tisa. Matokeo ya vita hivyo ni kuwa Wanyarwanda wengine waliamini kuwa Mungu wao amekufa ndio maana akawaacha wakauwana namna hiyo. Kwa hivyo, kuwa dini au imani ya Katoto wa Minane haikujulikana hata na majirani zake, si ajabu naye ikawa aliamua hataki tena kujihusisha na imani ya Mungu ambaye asingewasaidia wakati walipomhitajizaidin, kama vile tu Satre (keshatajwa) alipoathiriwa na vita vya pili vya dunia akafuata udhanaishi wa kikafiri. Katika mazishi yake Katoto, Bwana Isaya Omulangi anasema;

"...tumemzika mwenzetu Katoto bila kufuata taratibu za dini kwani hatujui kama alikuwa na dini yoyote au la." (uk. 116)

Tunaamini iwapo Katoto angalikuwa na imani hata chembe katika dini basi ingejulikana. Binadamu ni kiumbe wa kutangamana, katika mtagusano huo imani yake isingefichika.

4.3.3 Mwalimu Tadeo na imani yake thabiti ya ulokole

Katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* aidha kuna mhusika mwalimu Tadeo. Mwalimu Tadeo ni mlokole na amesawiriwa si kama mtu msomi tu bali mtu mwenye imani thabiti kwa Mungu wake. Aidha, mwalimu Tadeo amefaulu kuiweka familia yake kuwa thabiti katika imani ya Mungu na wasingefanya chochote, hata kula bila, kumwomba Mungu abariki chakula chao. Tofauti na yule Mzee katika basi la kwenda Bukoba ambaye matatizo yalimfanya asione umuhimu wa Mungu katika maisha yake, mwalimu Tadeo alimtegemea Mungu amsahilishie matatizo wanayoyapata ingawa yalizidi kuongezeka kila uchao.

Mwalimu Tadeo alikuwa tayari ashastaafu kazi ya ualimu. Mbali na kuwa kazi hii ya ualimu wa shule ya msingi haikuwa na mshahara wa kutosha hivyo kufanya iwe vigumu angalau kujiwekea akiba ya kutumia baada ya kustaafu, mwalimu Tadeo alitumia akiba yake yote akifuatilia marupurupu yake ya kustaafu katika afisi za serikali bila ya mafanikio yoyote. Pesa zake za akiba ziliisha akashindwa kuendelea kuzifuatilia pesa za kustaafu, akakaa nyumbani akimwomba Mungu kwa dhati awasahilishie shida zao.

Kulingana na Kierkagaard (keshatajwa), binadamu ni mtu binafsi na hupata kimbilio kutoka kwa mivutano ya maisha kupitia kwa Mungu. Mwalimu Tadeo aliamua kumtegemea Mungu kwa kumwomba kila uchao awasahilishie dhiki zao kama inavyodhihirika katika maombi haya:

"*Ee Bwana tuko mbele yako tukikuomba umlinde Tadeo mtumishi wako uliyempa jukumu la kuiangalia familia hii…umlinde na umwimarishe mama wa nyumba hii, Anna, umzidishie nguvu za mwili na za kiroho… umlinde binti yetu Mary, anayefanya kazi ya ualimu hapa kijijini…kwa vile Mary hajapata mshahara wake kwa miezi sita sasa umwepushe na mawazo ya kugoma, bali umjaze Roho Mtakatifu ili asihisi kiu wala njaa…Kwa vile Mary hana vitabu vya kufundishia tunakuomba Ee Bwana ummiminie busara na hekima ili, kwa nguvu zako, aweze kukariri kichwani yote yapatikanayo katika vitabu… tunakuomba umlinde na huyu binti yetu mwingine, Stella, anayesoma Chuo Kikuu, tunaomba akubali na avumilie mateso yote wanayoyapata wanakijiji hapa… Ee Bwana muumba vyote, tunaomba ukiokoe kijiji chetu cha Mushule; Uwaokoe watawaliwa na watawala wa kijiji hiki… Ee Bwana tunakuomba uwafariji wote wanaodhulumiwa hapa kijijini na sehemu zote za nchi hii… (uk. 56)*

Katika maombi marefu namna hii, mwalimu Tadeo aliombea kila mtu, kuanzia yeye mwenyewe, mkewe, Anna, binti zake Stella na Mary, Musa na wengine wote katika nchi hiyo. Hata wale wanaodhulumiwa na wanaodhulumu wenzao pia waliombewa. Ametaja matatizo ya walimu kutolipwa mishahara kwa miezi sita, mambo mengine ambayo ni matatizo yanayosababishwa na binadamu mwenyewe.

Kulingana na wadhanaishi wasioamini Mungu, matatizo kama haya yanahitaji binadamu mwenyewe afikirie na atumie akili yake kuyatatua wala si kuomba na kukaa kumtegemea Mungu ayatatue. Kezilahabi (keshatajwa) kama mmoja wa wadhanaishi wakanaji Mungu, pia katika *Nagona* na *Mzingile* anasisitiza umuhimu wa mwanadamu kufikiri ili kutatua matatizo yake. Hata hivyo, imani ya wadhanaishi wanaoamini uwepo wa Mungu kama Kierkagaard (keshatajwa) ni kuwa binadamu ni kikaragosi tu cha Mungu aliyemuumba. Anaishi kwa nguvu za Mungu na jinsi Mungu anavyopenda,

hivyo binadamu hawezi kubadilisha chochote katika maisha yake bila Mungu mwenyewe kupenda na kuruhusu yabadilike.

Hivyo, kwa watu wenye imani kama mwalimu Tadeo, maombi ndiyo njia pekee ambayo mambo yanaweza kubadilika katika nchi ya Tanzania. Ndio maana anaomba wafarijiwe hata wale wenye vyeo na wanawadhulumu wenzao. Wakibadilika hao ndio mwanzo wa mabadiliko ya nchi. Ila yote hayo yako mikononi mwa Mungu, nje kabisa na uwezo wa binadamu. Na haya ni dhahiri kwa sababu yeye mwenyewe Mwalimu Tadeo juhudi zake zote za kutafuta haki yake zilifeli. Hakuna kilichobadilika. Kwa Mwalimu Tadeo kutegemea maombi pekee ni jambo sahihi kwake kwa sababu jitihada zake zote kwa uwezo wake kama mwanadamu hazikufua dafu.

Mawazo haya yanashadidiwa na Mungah (1999) anaposema baadaye mwanadamu alimhusisha Mungu katika kila jambo alilotenda na shida zilipomfika alizishitakia kwa Mungu. Mungu hapa anatazamwa na mwanadamu kama suluhisho la shida zinazomkabili na hasa katika kuelezea kitendawili cha maisha yake. Baada ya binadamu kutia juhudi kubwa kujaribu kusaka ukweli unaodhihirishwa na maisha yake, analemewa na kukimbilia katika imani ya Mungu. Binadamu anajiona kama ambaye hana uwezo na nguvu zozote bila Mungu. Binadamu hujiendeshea mambo yake lakini hukimbilia Mungu wakati yupo kwenye shida.

4.3.4 Mwalimu Martin anaishi kwa kudura

Katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* Mwalimu Martin anazungumza na Musa Nshomile kuhusu matatizo anayopitia kama mwalimu. Anakiri kuwa matatizo hayo yamesababishwa na binadamu mwenyewe ambayo ni serikali, ila anaamini jinsi anavyofaulu kuishi katika matatizo yale ni kwa nguvu za Mwenyezi Mungu tu. Kama

yale mawazo ya Kierkergaard (keshatajwa) kuwa mwanadamu haishi kwa nguvu zake ila ni kikaragosi cha nguvu za Mungu. Mwalimu Martin anasema;

"Mimi na walimu wenzangu hatujalipwa mishahara yapata miezi sita sasa. Tunaishi kwa kudra ya Mwenyezi Mungu." (uk. 77)

Kulingana na *Kamusi Elezi ya Kiswahili,* kudura ni mapenzi au nguvu za Mungu; apendavyo Maulana. Kwa hivyo mwalimu Martin kusema kuwa anaishi kwa kudra ni kuwa anatambua na anakubali uwezo na mapenzi ya Mungu juu yake.

4.3.5 Musa Nshomile anarudisha imani kwa Mungu

Katika kutafuta maana ya maisha yake baada ya kupona homa kali ya malaria ambayo karibu imuuwe, Musa Nshomile anasawiriwa akijisaili kuhusu maana ya maisha na imani katika dini. Musa anaona maisha hayana maana namna yalivyo, kuwa binadamu wengine wako katika "lindi la sahau" na labda kuwa na imani thabiti kwa Mungu ndiyo njia pekee ya kuona maana ya maisha kama ilivyo familia ya mwalimu Tadeo. Musa katika mawazo yake anajisaili;

Hawa watu, kina Stella, ndio binadamu mmoja katika watu kumi. Labda hawa binadamu mmoja ndio watavuta watu tisa kutoka katika lindi la sahau kama walivyomvuta yeye toka kuzimu! Kisha mawazo yake yakafikia juu ya imani ya kina Stella. Kujitoa kwao kwa Yesu, ulokole, imani kali! Alikumbuka kuwahi kuskia ikisemwa kuwa ulokole ni kuchanganyikiwa. Kama ulokole ni kuchanganyikiwa, bora kuchanganyikiwa kwa Yesu kuliko kuchanganyikiwa katika kitu kidogo kama ilivyo katika hao tisa. (uk. 91)

Musa ametaja lindi la sahau. Mawazo haya yanalingana na ya Kierkagaard (keshatajwa), alipogawanya maisha ya binadamu katika vipindi/daraja tatu kuu; kipindi cha ujumi, katika kipindi hiki mtu huishi kwa kujali raha za wakati anamoishi pekee bila kujali

kesho. Kipindi cha pili ni cha uhalali/adabu (ethical stage), ambapo maisha huwa yameimarika na kuendelea kupitia kazi na ndoa. Na kipindi cha tatu ni cha dini (religious stage) ambacho hutambulika kwa imani. Imani ambayo huwa na uhakika wa kuogofya, uoga ambao huonyesha kwa hakika uhusiano wa kisiri alionao mja na Mungu.

Lindi la sahau alilolitaja Musa Nshomile ni daraja ya kwanza katika hizo daraja tatu za Kierkagaard (keshatajwa). Musa anasawiriwa akiisaka tena imani yake kwa Mungu. Tangu riwaya ianze hakuna pahali hata pamoja Musa alionekana kuwa na imani yoyote ya dini. Ila katika mazungumzo yake na yule Mzee katika basi la kwenda Bukoba Musa anasawiriwa kuwa mtu mwenye imani ya Mungu;

"Hapana, Mungu yuko na anayaona yote na atatusaidia." (100)

Riwaya inaanza Musa akiwa katika daraja ya kwanza ya ulimbwende katika zile daraja tatu za Kierkagaard. Alipokuwa Uingereza, Irene alimshawishi waoane ila Musa alikuwa hata hajawazia kitu kama hicho japo umri wake ulimruhusu kuoa. Alikwepa mambo ya ndoa;

"Kumbe unajua!" Irene alimaka. "Hapana hujui. Hunijui mimi wala hutapata kunijua. Labda ungejua ungenioa."

Musa hakuufurahia mkondo wa mazungumzo, lakini kama mwanamume aliyekula fadhila ya huyo mwanamke, ilibidi amliwaze. (uk. 5)

Musa hakuwa na nia yoyote ya kuingia katika ndoa wakati ule. Hata alipofika Tanzania bado wazo la kuoa halikuwa limemkaa vizuri. Ila alipopatana na Stella aliyemwuguza malaria, si imani kwa Mungu tu iliyoanza kujidhihirisha bali alionyesha nia ya kutaka kumwoa Stella, bintiye mwalimu Tadeo. Alitoka daraja ya kwanza ya Kierkagaard akaenda ya pili na ya tatu.

4.3.6 Stella Tadeo na imani thabiti ya ulokole

Stella, kwa imani yake katika dini anaamini kabisa kuwa hawezi kufanya chochote bila usaidizi na uongozi kutoka kwa Mungu na roho mtakatifu wake, hata uamuzi katika jambo la kupenda na kuolewa. Anakiri kuwa katika moyo wake anampenda Musa na angependa kuolewa na Musa ila hawezi kusema moja kwa moja hadi amwombe Mungu amwongoze katika uamuzi huo. Anamwomba Mungu pia amwepushe na majaribio yote ya uasherati. Stella anaanza kwa kumshukuru Mungu kwa kumwelekeza Musa na kumfikisha kwao nyumbani. Pia anamwomba mwenyezi Mungu amwongoze Musa naye aokoke kama wao.

Baada ya kuombwa uchumba na Musa Nshomile, Stella alishindwa kutoa jibu na badala yake akaweka imani kwa Mwenyezi Mungu na kumwachia amwamulie, kama ifuatavyo katika kauli hii:

"Swali lako ni sawa na swali langu. Mimi sina uwezo wa kujibu maswali haya. Ajuaye, mwenye majibu ya kila kitu yuko juu. Tumwombe atupe jibu. Sina chembe ya shaka kuwa atatujibu. Sasa tuongee mengine." (uk. 95)

Uswahilini kuna msemo "ndoa hupangwa mbinguni", hii ni imani sawa na hii ya Stella kuwa hakuna kitu chochote kilicho mikononi mwake kukifanyia maamuzi yoyote isipokuwa Mungu pekee ndiye anayepanga na anajua ni lipi la sawa kwa kila mmoja. Kwa Stella, maisha yake yote amemwachia Mungu, ayapangie anavyotaka hadi mwisho. Kwa hivyo kwa Stella kila kinachotokea Mungu anajua zaidi sababu zake. Kama ilivyo imani ya Kierkagaard (keshatajwa), Stella amekubali kuwa yeye ni kikaragosi cha nguvu za Mungu na hawezi hata kujitafutia mume isipokuwa ambaye atapewa na Mungu.

4.4 Kifo

Udhanaishi hutilia mkazo matatizo halisi yanayomsibu binadamu. Hujadili hali kama vile kihoro, ufupi wa uhai, fadhaa, mashaka, pekecho, utupu wa maisha, uchovu na jinsi zinavyoathiri maisha ya binadamu. Jazanda zinazoashiria kiungulia, uchovu, pekecho na kiwewe zinatumika kusawiria hali ya binadamu. Mwisho, huangazia kwa hamasa tanzia iliyokurubiana na maisha ya binadamu, huonyesha kwamba juhudi za mtu za kujitafutia maana ya maisha mara nyingi huishia katika mvunjo au uvunjikaji wa juhudi hizo, hasa katika mauti. Mwisho wa binadamu ni kifo. Hivyo, kifo ni ithibati tosha kuwa maisha hayana maana yoyote.

Mtindo wanaotumia wadhanaishi ni taswira wanayomchorea msomaji picha mbalimbali za maisha ya kuteseka anayopitia mwanadamu ulimwenguni. Hii ni kuonyesha kuwa maisha hayana maana jinsi yalivyo.

Kulingana na maelezo haya, maisha hayana maana namna yalivyo. Na kinachokosesha maisha maana ni ugumu wake. Kuwa kila siku mwanadamu anafaa kukabiliana na hali fulani ambazo hana uwezo nazo. Hali hizi ni kama magonjwa, majanga, mafuriko na mwisho wa yote haya ni kifo. Kifo ambacho kinaweza kumpata mtu wakati wowote bila yeye mwenyewe kuwa na uwezo wa kujikinga dhidi yake. Kifo kinapokuja kama hivyo humkatizia mwanadamu maisha yake na mipango yake yote. Kwa ajili hii, mwanadamu huishi na wasiwasi, hana hakika na maisha, chochote chaweza kutokea na hana uwezo wowote wa kukizuia.

Wahusika wafuatao kutoka riwaya hizi mbili wanakumbwa na majanga ya kaisili na maradhi yanayowakatizia maisha yao.

4.4.1 Wazazi wa Musa Nshomile na ndugu zake wanaangamizwa na malale

Katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* mwandishi anasema katika kijiji cha Ntumagu, wilayani Burumalo alikozaliwa Musa Nshomile kulikumbwa na maradhi ya malale ambayo yaliangamiza watu wengi wakiwemo wazazi na ndugu zake Musa. Maradhi, utupu na ufupi wa maisha ni katika sifa za udhanaishi. Wadhanaishi wote wanazungumzia tanzia aliyokurubiana nayo mwanadamu, ambayo ni kifo. Mwisho wa mwanadamu ni kifo. Wazazi wa Musa hawakuishi kumwona mwana wao Musa akikua. Ndugu zake Musa aidha hawakupata fursa ya kuishi wakazeeka, kifo kiliwachukua mapema;

Musa mwenyewe alizaliwa katika kijiji cha Ntumagu wilayani Biharamulo. Tarehe sahihi ya kuzaliwa kwake hakuna mtu hai mwenye kumbukumbu nayo. Lijulikanalo ambalo wengi hulitumia kukisia umri wake, ni kwamba akiwa bado mtoto mchanga ulizuka ugonjwa sehemu hizo wa malale. Serikali kwa vile haikuwa na uwezo wa kudhibiti mbung'o, wadudu waambukizao ugonjwa huo, ilibidi iwahamishe watu kuwapeleka sehemu nyengine. Lakini hii ilikuwa baada ya ugonjwa huu kuua watu wengi wakiwemo wazazi na ndugu wa Musa. Musa alichukuliwa na shangazi yake aliyehamia katika kijiji cha Mushule, wilayani Muleba. (uk. 22)

Vifo kama hivi vya halaiki kutokana maradhi ya kuambukiza au majanga ya kiasili ni mbinu moja inayotumiwa na wadhanaishi kumsawiri mwanadamu katika ulimwengu huu wa kibwege, ambao mwanadamu hana uwezo wowote juu ya mambo yanayomtokea maishani mwake. Kupitia wahusika hawa, mwandishi anatusawiria jinsi ambavyo mwanadamu hana uwezo wowote juu ya masuala kama maradhi na kifo. Vinapoamua kumzuru mwanadamu basi hana uwezo wowote wa kuviepuka.

4.4.2 Maburuki na watuhumiwa wengine waangamia rumande

Wadhanaishi wote wanazungumzia tanzia iliyomkurubia binadamu, ya kwamba juhudi zote anazozifanya binadamu huishia kwenye mvunjo, yaani kifo. Mwisho wa mwanadamu ni kifo. Abdu, katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* Anaeleza kuhusu watuhumiwa wenzake wanne waliokuwa wanangoja kuhukumiwa baada ya wengine kuachiwa na wengine kukimbia rumande. Abdu anasema kuwa wafungwa hawa wanne wote walikufa. Mmoja alijinyonga, ila kati ya hao watatu wengine, wawili walikufa kwa kipindupindu na mmoja ambaye ni Maburuki alikufa kwa kukosa hewa safi kwa kurundikwa wengi kwenye chumba kidogo. Abdu anasema;

"*Wenzangu walikufa, wawili waliondolewa na kipindupindu wakati kilipolikumba gereza hili. Mmoja aliondolewa Kiilemera… ni Maburuki, mtuhumiwa mwenzangu."* (uk. 123)

Hawa hawakujiua, ila kifo kiliwakuta na kuwapokonya maisha yao. Ni sifa ya udhanaishi kuonyesha kuwa maisha hayana maana namna yalivyo, na hata ukijaribu kuyatafutia maana mwisho wake ni kifo. Kwa kawaida, kifo cha namna hii alichokufa Maburuki ni kifo kinachoweza kuepukika, ila Maburiki hakukiepuka. Hii ni sifa moja ya udhanaishi, kuonyesha maisha ya mwanadamu si chochote, kifo chake hakitabiriki na anaweza kuangamizwa na kitu chochote, hata kisichofaa kumwangamiza.

4.4.3 Familia ya Garincha kijijini Kakonko yaangamizwa na kipindupindu

Mwanadamu anapoishi kuna mambo mengi yanayotokea na kumwathiri ila hana uwezo wowote juu yayo. Mambo hayo ni miongoni mwa majanga ya kiasili kama mafuriko, mtetemeko wa ardhi, radi na maradhi ya kuambukiza. Katika riwaya ya *Harusi ya Wendawazimu* pia kuna mripuko wa maradhi ya kipindupindu. Miaka michache baada ya Garincha kuzaliwa kijijini kwao Kakonko kulikuwa na mripuko wa maradhi ya Kipindupindu yaliyowaua wanakijiji wengi wakiwemo wazazi na ndugu zake Garincha;

Lijulikanalo ni kwamba miaka michache baada ya kuzaliwa kwake kijiji cha Kakonko kilikumbwa na baa la ugonjwa wa kipindupindu. Baa hili liliuwa watu wengi wakiwemo wazazi na ndugu zake Garincha, yeye pekee kati yao ndiye aliyenusurika. (uk. 11)

Kama tulivyotangulia kusema, wanadamu huwa hawana uwezo katika majanga na mripuko wa maradhi kama haya. Mripuko wa maradhi kama kipindupindu hasa katika nchi ambazo hazijaendelea kama za Afrika Mashariki, Tanzania inapopatikana, huwa janga haswa ambalo huangamiza watu wengi. Mwaka wa 2020 ni mfano mzuri tunaposema kuwa binadamu huwa hana uwezo juu ya majanga kama mripuko wa maradhi. Kufikia Mei, takwimu zilizotelewa ni kuwa mripuko wa homa ya korona ulikuwa umeangamiza zaidi ya watu laki tatu na elfu arubaini ulimwenguni kote. Hizo nchi zilizoendelea ndizo zilizoathirika sana minghairi ya kuendelea kwao. Maradhi kama haya huyakata maisha ya binadamu na kuyafanya yakose maana. Hii ndio picha ambayo mwandishi anatuchorea kuhusu wahusika hawa katika *Harusi ya Wendawazimu* wanaoangamizwa kwa halaiki na maradhi haya ya kuambukiza.

4.4.4 Zainab afariki dunia

Katika riwaya ya *Harusi ya Wendawazimu*, baada ya wazazi wa Garincha kufa wakati wa mripuko wa homa ya kipindupindu, Garincha alichukuliwa na shangazi lake, Zainab, aliyemlea na kumpeleka shule hadi darasa la saba kisha naye akafa na kumwacha bila wa kumwangalia;

Mwanamke huyu aliyejulikana kwa jina la Zainab alimfadhili vya kutosha; alipofariki dunia (Ee udongo! Tulia taratibu juu ya mifupa ya Zainab) Garincha alikuwa yuko katika darasa la saba. (uk. 11)

Kama isingelikuwa serikali kumchukua na kumsomesha baada ya kupita mtihani wake wa shule ya msingi, ndoto zote za Garincha za kwendelea na masomo zingekufa na kifo cha shangazi lake. Juhudi za mwanadamu kujitafutia maana ya maisha huishia kwenye mvunjiko wa juhudi hizo kupitia kifo. Ingelikuwa uwezo wake, Zainab angeishi hadi akahakikisha Garincha amemaliza kusoma na anaweza kujitegemea. Ila kwa kuwa mwanadamu hana uwezo wowote juu ya masuala kama kifo, kifo kilimchukua mapema na kukatisha juhudi zake za kumlea Garincha.

4.5 Ukengeushi

Ukengeushi una maana ya mtengo au mbanduko au kuhisi ugeni. Hali hii hutokea katika mahusiano mbalimbali katika jamii. Mtu binafsi katika jamii hana nafasi ya kujiamulia matendo yake badala yake analazimika kutenda kulingana na kaida fulani maalumu zilizopangwa na jamii pana. Hivyo, Ukengeushi huanza pale mtu anapojaribu kufikiria kibinafsi na kutenda kinyume na kaida na miiko iliyozoeleka. Huanza kuwa na migogoro ya ndani kwa ndani anapopambana na nguvu hatari ambazo zinajaribu kummeza na kumwangamiza. Anajiamulia matendo yake. Katika kutafuta uhuru wake wa mawazo na matendo, binadamu anakengeushwa na Mungu, jamaa au familia yake, asili yake na tabia zake yeye mwenyewe.

Tariq (2017) anasema, “Udhanaishi unapendekeza mwanadamu kujiamulia, na hawezi kufuata imani (metanarrative) au mkondo fulani wa mawazo isipokuwa atajifunga mwenyewe. Hata hivyo, katika uhuru huu yuko pweke kwani jukumu la kujitafutia maana ya maisha yake ni lake binafsi. Katika juhudi hizi, baada ya kujitenga na imani za kijadi zilizomweleza mwanadamu, anautazama ulimwengu kwa pazia ya utosahihi (inauthenticity), na anagundua ukweli kuhusu imani aliyokuwa nayo ya ulimwengu huu usiomaana. Mwanadamu anapata kihoro kutokana na ukweli huu, kuwa hawezi tena kutegemea imani za awali alizoshikilia kuhusu ulimwengu, ama hata kusema huu ndio

ukweli kuhusu ulimwengu. Anapogundua hivi, anagundua kaida zote za jamii ni za kujitungia hivyo anaamua kutozifuata, tendo hili linamtenga zaidi na jamii inayomwona mkengeushi.” (T.Y)

4.5.1 Musa Nshomile anakengeuka kitabia

Katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* baada ya Musa Nshomile kupitia matatizo na kuona kuwa hakuna aliyejali uadilifu, alipofika katika hoteli ya *New Africa Hotel* alijaribu kudanganya kuwa alilipa kitambo ili awekewe nafasi ya chumba katika hoteli hiyo. Hii si tabia aliyotua nayo kutoka ndegeni saa kadhaa zilizopita. Kama anavyosema Tariq (keshatajwa), Musa anagundua kuwa kaida alizokuwa akizifuata ni za kujitungia wala hazimsaidii tena katika mazingira yake mapya. Hivyo, anakengeuka kutoka kwa tabia yake nzuri ili kuweza kuingiliana na mazingira yake mapya;

Jina la Musa halikuwepo, uongo ukiwekwa kando, na Musa alijua hivyo. Lakini alikuwa anajirekebisha haraka ili aende sambamba na mazingira ya nchi alivyoyakuta. (uk. 16)

Huu ni ukengeushi wa mtu kutoka kwa nafsi yake, ambazo ni tabia zake. Mwandishi anasema yafuatayo kumhusu Musa;

Musa alifadhaika. Pamoja na siku nyingi za maandalizi na hulka yake ya kutii sheria na kufuata utaratibu… (uk. 7)

Kuwa saa chache baadaye alidanganya kuhusu utaratibu ambao ni hulka yake kuufuata inaonyesha mwanzo wa kukengeuka kwake kimaadili. Musa anakengeuka kutoka kwa tabia yake nzuri na anaanza kudanganya.

Gwachi Mayaka (1991) anashadidia haya kwa kusema kuwa mtu anaweza kuwa amewekewa masharti au kanuni ambazo zinatinga na kuongoza uamuzi wake katika matendo yake. Anajikuta hawezi kutenda kivyake akitumia akili na uwezo wake. Mtu

kama huyu basi ametenganishwa na matendo yake na hivyo amekengeushwa. Wakati mwingine serikali au mfumo wa utawala unaweza kuchukua nafasi hii. Watawala na wanasiasa wanaweza kunyanyasa watu wasio na uwezo kufikia kiwango cha hawa watu kukosa kujiamini katika jambo lolote.

Tunaona kinachomfanya Musa Nshomile kukengeuka ni mfumo wa utawala kama ilivyoelezwa na Mayaka (keshatajwa). Musa Nshomile hakuweza kufanya lolote isipokuwa kubadilika kutoka kwa tabia yake ili aingiliane na maisha alivyoyakuta nchini Tanzania. Japo hapo uwanja wa ndege alijaribu kushikilia maadili yake ya kutotoa hongo, yale mambo aliyokumbana nayo alipoabiri gari, ya kutusiwa na kudharauliwa, akaona jambo pekee ni kubadili tabia kuingiliana na maisha yanavyoenda.

Hata alipoenda kuonana na binamu yake, Abdu, huko rumande, tunamwona Musa akitoa hongo kwa askari wa zamu ili apewe muda mwingi wa kusema na binamu yake;

“Elfu,” yule askari alisema. “Shilingi elfu moja.”

“Nakubali,” Musa Nshomile alijibu. “Lakini sina shilingi elfu moja, nina shilingi mia.” Musa alisema hivyo huku akitoa shilingi mia na kumpa yule askari kupitia kidirisha cha lango la gereza. (uk. 105)

Musa Nshomile na binamu yake Abdu Shaaban walipokuwa wakiendelea na mazungumzo yao, yule askari alikuja tena kumtaka Musa aondoke kwa kuwa muda umekwisha ila Musa bila hata kusema alitia mkono mfukoni akatoa hongo.

“Muda umekwisha,” askari alisema huku akiangalia saa yake.

Tafadhali meja tupe dakika chache tuhitimishe mazungumzo yetu,” Abdu aliomba.

“Hapana, nasema muda umekwisha.”

Naye Musa, bila kusema lolote alitia mkono mfukoni akatoa noti ya shilingi kumi na kumpa askari yule. Askari, bila kuiangalia noti ile alisema, "Nawapa dakika kumi na tano za mwisho." (uk. 121)

Haya ni matendo ambayo yanaonyesha kuwa Musa alikuwa amekengeuka kabisa na tabia yake ya awali ya kutoshiriki tabia zisizofaa kama hizi za kutoa hongo. Tariq (2017) anasema kuwa ukengeushi huu wa nafsi (tabia) unatokana na jinsi mtu mwengine anavyokuchukulia. Ni mtazamo huu wa watu wengine ndio unamfanya mwanadamu kupoteza utambulisho wake binafsi. Hivyo, tofauti kati ya jinsi watu wengine wanavyokuona na jinsi unavyojiona ndio humfanya mtu kuchanganyikiwa.

Musa ni mfano mzuri wa watu waliochanganyikiwa kutokana na hali hii. Jamii inamwona hana maana kwa sababu hakurudi na *pick up* na dola kutoka Ulaya ilhali mwenyewe anajiona na maana kuwa msomi wa uzamifu. Anachanganyikiwa na anakengeuka kutoka tabia yake. Maadili yake yote aliyojifunza huko Uingereza anayawacha.

4.5.2 Maimuna anakengeuka na mila za ndoa

Katika *Harusi ya Wendawazimu,* Maimuna anasawiriwa akitetea uhuru wa Zamda na Yasmin kufunga ndoa na wanaume wasiokuwa waislamu. Aidha, anatetea hulka ya vijana ambayo inakinzana na kaida iliyokuwa zamani kuhusu mambo ya ndoa kama inavyodhihirika katika dondoo hili;

"Watoto wa siku hizi wanajiamulia, kutufahamisha ni heshima wala si wajibu, mimi nawatetea." (uk.88)

Kauli hii ya Maimuna inamsawiri kama mtu aliyekubali mabadiliko japo mabadiliko haya yanapingana na kaida za jadi hasa katika kanuni za ndoa. Huku ni kukengeuka. Aliacha kaida za kijadi za mahusiano ya kindoa na kukubaliana na mabadiliko.

Amekengeuka kutoka kwa tamaduni na dini pia inayohitaji msichana kupata idhini ya baba yake ili aolewe.

Kwanza, utamaduni wa Uswahilini huhitaji posa ipitie kwa wazazi. Wazazi wakiridhia posa hiyo na mahari ikitolewa basi ndipo ndoa ifungwe. Pili, katika dini ya Kiislamu, wazazi hawafahamishwi tu kuhusu uchumba na ndoa za binti zao, bali wazazi ndio hutoa idhini kama walii wa wana wao. Ila tunaona Maimuna anapuuza kaida zote hizi za kitamaduni na kidini na kutetea jinsi mpya ya vijana wanavyochukulia swala la ndoa. Ni dhahiri kuwa Maimuna amekengeuka kutoka kwa kaida za kitamaduni na za kidini pia.

4.5.3 Mwalimu Tadeo amruhusu bintiye kulala chumba kimoja na Musa

Katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* familia ya mwalimu Tadeo imesawiriwa kuwa familia yenye imani thabiti sana katika ukristo. Watoto wake wana nidhamu sana wakilinganishwa na wasichana wengi katika hii riwaya. Hata Stella anashindwa kuukubali uchumba wa Musa akitumaini Mungu atamjibia ombi hilo kwa kumwomba amwongoze. Hata hivyo, kwa mwalimu Tadeo kumruhusu mwanawe Stella kulala chumba kimoja na barubaru shababi kama Musa Nshomile ni kinyume na maadili ya Kiafrika na hata ya dini hiyo ya kikristo. Mwalimu Tadeo anamhimiza Stella kwenda kulala chumba kimoja na Musa Nshomile ambaye tayari alikuwa ashaanza kupata nafuu na kurudisha nguvu zake. Hata walipolala pamoja Musa alijaribu kumbandikia Stella mkono, Stella asingemkemea Shetani kuna uwezekano makubwa yangetokea. Mwalimu Tadeo anamwambia Stella;

> "*Nenda kalale mtoto mchanga. Kawe karibu na mgonjwa." (uk.97)*

Hata baada ya Stella kumwambia babake kuwa anampenda Musa, haikuwa sababu yake kuona hatari ya wao kulala chumba kimoja usiku kucha. Kwanza aliafikiana na bintiye kuwa Musa Nshomile ni kijana mzuri. Maadili ya Kiafrika wala ya kikristo hayaruhusu

msichana kulala chumba kimoja na mvulana ambaye hajamwoa. Kaida hizi ziliwekwa Sababu yake ni kupunguza majaribu yatakayosababisha zinaa kutokea. Ila Mwalimu Tadeo anayakiuka na kumruhusu bintiye kulala chumba kimoja na Musa. Huku ni kukengeuka na kutoka kwenye maadili ya dini na ya kiutamaduni.

4.5.4 Kachala Domokaya anakengeuka na useminari

Katika riwaya ya *Harusi ya Wendawazimu,* Kachala domokaya alikuwa mseminari ila akafukuzwa kanisani kwa sababu ya kupenda wanawake kama inavyodhihirika:

"Kachala alisema bila wasiwasi nami sikuweza kupinga kwa vile kachala huyo alikuwa mwanafunzi mseminari mpaka alipofukuzwa kwa sababu ya warembo." (uk. 4)

Huko ni kukengeuka kutoka kwa maadili ya kiseminari. Na hata kauli hii ilipotolewa Kachala huyo alikuwa baa akinywa pombe. Kuonyesha wazi yuko mbali kabisa na mafunzo yote ya kiseminari aliyopitia. Huku ni kukengeuka kutoka kwa maadili ya kidini, au hata kutoka kwenye dini yenyewe.

Osore (2008) akichambua *Kichwamaji* ya Kezilahabi anashadidia mawazo haya kuwa mseminari huhitajika kuwa na adabu na kuwa na tabia nzuri. Kwa kumtazama Kazimoto ni rahisi kuona majaribu wayapitiayo waseminari katika ulimwengu wa sasa ambapo ngono za kiholela (zinaa) ni jambo la kawaida, ilhali wao wanatakikana kutoikaribia. Inaonyesha ugumu uliopo katika kulinda kiapo chao cha kutoshiriki zinaa.

Kezilahabi alifukuzwa shule ya seminari kwa sababu walimu wake walisema hana "mwito" wa kuwa padre. Hili lilimfanya kukengeuka kabisa na akawa mdhanaishi bora na maarufu zaidi katika fasihi ya Kiswahili. Kachala Domokaya naye alifukuzwa katika shule ya seminari baada ya kukengeuka na kuvunja kiapo chake cha kutoshiriki zinaa. Baada ya kufukuzwa, akaendelea na ukengeushi wake. Akawa mlevi na akaendelea

kushiriki zinaa. Huku ni kukengeuka kutoka kwa maadili ya kiseminari, ya dini ya kikristo. Maadili ambayo Kachala huyu aliyapitia, ila akashindwa kuyafuata.

4.5.5 Garincha hajali wazee

Katika riwaya ya *Harusi ya Wendawazimu*, Garincha anasawiriwa kama mtu aliyekengeuka katika maswala ya mila na desturi za uchumba na ndoa. Eliza alipomwambia kuwa sio mila yao msichana kukubali mchumba bila idhini ya wazazi wake, Garincha anamwambia awachane na mila hizo. Mtafiti anaamini kuwa kukengeuka huku kwa Garincha kunatokana na kuwa yeye Garincha tangu darasa la saba ameishi bila mzazi. Hivyo, kwake yeye yuko huru kujiamulia mambo yake mwenyewe tofauti na watu wengine kama Eliza ambaye mbali na kusingizia mila katika jambo kama hili, ni dhahiri kuwa kwa kiasi fulani anatambua mamlaka ya wazazi juu yake. Hivyo, ukengeushi wa Garincha umetokana na kuwa amekosa mamlaka ya wazazi tangu udogoni, ndio maana hayatambui mamlaka hayo hata kwa watu wengine.

Aidha, Garincha ameongeza na elimu aliyoipata shuleni iliyomfanya azidi kukengeuka zaidi kutoka kwenye maadili na mila za Kiafrika. Kushadidia suala la wasomi wa Kiafrika kukengeushwa na elimu wanayoipata shuleni, Mayaka (1991) anasema kuwa ukengeushi wa wasomi unatokea wakati wao, kutokana na elimu na usomi wanakuwa na falsafa au mtazamo unaopingana na kanuni, mwenendo na misingi ya jamii zao. Baada ya kung'olewa mizizi ya utamaduni wao, wasomi hujifunza kuishi maisha ya ubinafsi na kutojali watu wengine. Wengine wanaishia kuwadharau na kutowatii wazazi wao. Dondoo ifuatayo inadhihirisha ukengeushi huu wa mhusika Garincha alipojaribu kumwomba uchumba mhusika Eliza;

"*Siyo mila yetu kwa msichana kukubali mchumba bila idhini ya wazazi wake."*

Garincha akajibu;

"*Achana na mila. Mila ngapi bado unazifuata?"*

"*Ni kweli mila nyingi za kimatengo hatuzifuati siku hizi lakini mila ya ndoa bado ina nguvu." (uk. 18)*

Mazungumzo haya yanaonyesha kuwa Garincha amekengeuka sana kuliko hata mabadiliko yenyewe yalipokuwa yamefikia wakati huo. Marika yake bado wanathamini mila kama za ndoa, na bado wanatambua mamlaka ya wazee juu ya mila hizo. Ila Garincha amekengeuka kabisa. Tushatangulia kusema kuwa kukengeuka huku kwake kabisa kunatokana na mazingira alimokulia yasiyokuwa na mzazi wa kumthamini na wa kumwongoza katika mambo muhimu maishani. Kukengeuka kwake aidha kukaongezwa na elimu aliyoipata huko chuoni kama asemavyo Mayaka (keshatajwa).

Baadaye alipopatana na Yasmin, Garincha bado anaonyesha matatizo yake ya kutofuata itikadi za ndoa. Bado anaonyesha kutojali mamlaka ya wazazi kuhusu jambo la ndoa anapomwomba Yasmin uchumba. Yasmin, kama Eliza alivyofanya hapo nyuma, alionyesha wasiwasi wake na msimamo katika itikadi kuwa jambo la uchumba na ndoa kwa jumla lazima lipate baraka za wazazi, ila Garincha analipuuza jambo hili. Garincha amekengeuka kabisa kutoka kwenye mila na desturi zinazotawala jambo zima la ndoa;

"*Naomba tuoane… Jumamosi." Garincha alimwambia Yasmin.*

"*Hiyo barua imepokelewa lini? Hicho kishika uchumba kilitolewa na nani. Na mahari imetolewa saa ngapi mpaka tuoane hiyo Jumamosi? Au unanidhihaki?" (uk. 56)*

"Siwezi kuolewa bila idhini ya wazazi wangu." (uk. 57)

Kauli hii inaonyesha kuwa Yasmin bado anatilia maanani kanuni, desturi na mila zinazohusiana na ndoa. Anatambua mamlaka ya wazee wake maishani mwake. Ila Garincha kwa upande wake hazitilii maanani desturi hizo wala kuona umuhimu wa wazee kuhusishwa katika maamuzi hayo;

"*Hiyo itakuja baadaye, mimi siwezi kuleta utani kwa jambo muhimu kama kuoa. Nakwambia tutawaendea baada ya kuoana na sidhani kama watatukatalia." (uk. 57)*

Japo anakiri kuwa jambo la ndoa ni muhimu, kauli hii bado inaonyesha kuwa Garincha haheshimu itikadi zozote za ndoa. Hatambui umuhimu wa wazee katika jambo kama hili.

Garincha alipatana na Yasmin aliporudi likizo kutoka Uingereza. Tunaamini kuwa kuishi kwake Uingereza kulizidi kumkengeusha na mila za Kiafrika. Akawa hazitambui tena. Katika utamaduni wa Ulaya, kaida ya kulipa mahari hakuna tena. Siku hizi huko Ulaya hata lazima ya ndoa hakuna tena, muhimu ni kukaa pamoja na kuzaa. Hii ni athari nyengine ambayo Garincha alikumbana nayo kabla ya kupatana na Yasmin na athari zake ziko wazi. Hata anapoenda kukutana na wazazi wa Yasmin, anaonyesha kughadhabishwa sana na matusi ya babake Yasmin kiasi kwamba anafikia kumtusi. Watu hunyimwa wake kwa sababu ndogo kuliko hizi ila yeye hajali hata kumtusi mkwe mtarajiwa;

Garincha sasa alikasirika. Akasimama na mikono amejishika nyongani na huku akimwangalia Saad kwa macho yaliyoiva kwa hasira chini ya pumzi alisema, "Shenzi taipu. Kamuoe mwenyewe." Akafungua mlango na kuurudisha kwa nguvu. (uk. 97)

Mambo haya hayafanywi uswahilini, isitoshe hayafanywi na mtu yeyote ambaye anaheshimu wazazi na mamlaka yao. Hayafanywi na mtu ambaye anampenda vizuri msichana aliyeenda kumposa. Haifai kuchokoza mamba ilhali hujavuka mto, ila Garincha aliyafanya bila kujali. Hili linaonyesha kuwa Garincha amekengeuka. Hajali kukosana na kutusi watu waliomzidi umri. Haya yanatokana na elimu na malezi aliyopata. Katika *Kichwamaji* Kezilahabi anasema anavunjikwa na moyo kwa kuona wazee wanakimbia vijana. Hii ni baada ya mzee kuingia katika ofisi ya Manase alimotukanwa ikambidi atoke mbio ofisini. Haya yanaonyesha mbanduko wa vijana kutoka kwenye jamii zao.

Kushadidia haya, Wanjala (1980:22) anatoa maoni kuwa msomi Mwafrika anapotambua utamaduni wa 'bwana', hutaka kujitambulisha, kuoanisha na kumudu utamaduni huu mpya huku akikemea wake. Anaposhindwa, anarudi kwa utamaduni wake wa zamani. Vile vile kufanya hivi si rahisi. Mwisho anakataa na kukataliwa na pande zote - mashariki na magharibi na huu ndio ukengeushi. Garincha katika *Harusi ya Wendawazimu* ni mhusika anayeingiliana vizuri na maelezo haya.

4.5.6 Chris (Christopher Mbwana) afanya kinyume na ubatizo

Tangu mwanzo wa riwaya ya *Harusi ya Wendawazimu*, Chris amesawiriwa kuwa mtu anayependa anasa, pombe na wanawake hata walioolewa tayari kama Mariam aliyekuwa mke wa kwanza wa Musa. Anajihusisha na Eliza kimapenzi na kuwa na Zamda kama kimada wake. Huu ni uasherati na hakuna dini inayoruhusu ngono kiholela. Kwa Chris kujihusisha na ngono za kiholela namna hii inaonyesha kuwa amekengeuka, kwa sababu Chris alikuwa amebatizwa kanisani. Mhusika Shofeli anathibitisha hili kwa kusema yeye ni kama babake Chris kwa sababu ndiye aliyesimamia ubatizo wake;

> *"... Mimi nimekuja kwenye harusi. Christopher ni mwanangu, nilimsimamia katika ubatizo..."* (uk. 133)

Mfano huu wa Chris pia unapatikana katika riwaya ya *Kichwamaji* ambapo badala ya mhusika Kazimoto aliyekuwa msomi kuwa kielelezo chema kwa kakake mdogo Kalia, yeye Kazimoto ndiye anayechangia kumharibu kimaadili kwa kumtumia kuwafikia wasichana wake.

Pia Chris katika *Harusi ya Wendawazimu* ni msomi mwengine anayeonekana kukengeuka kimaadili. Anashiriki mapenzi na Mariam ambaye ni mke wa Musa. Anakuwa na kimada, Zamda na anakuwa na Eliza pia. Baada ya harusi yake na Zamda Chris bado anashiriki mapenzi na wanawake wote watatu. Huku ni kukengeuka kutoka

katika maadili ya dini yake ya kikristo inayokataza zinaa na ndoa mseto. Pia anakengeuka na maadili ya jamii inayomruhusu kuoa wake zaidi ya mmoja ila si kulala na wake za wenyewe wala vimada.

4.5.7 Zamda na Yasmin wanakengeuka kidini na kimaadili

Ulevi wa aina yoyote ile umeharamishwa katika dini ya kiislamu ambayo ndiyo dini ya akina Zamda na dadake Yasmin. Mwenyezi Mungu anasema katika Korani 2:219;

> *Wanakuuliza juu ya ulevi na Kamari. Sema: "Katika hivyo mna madhara makuu na (baadhi ya) manufaa kwa (baadhi ya) watu. Lakini madhara yake ni makubwa zaidi kuliko manufaa yake…"*

Si unywaji wa pombe tu ulioharamishwa katika dini ya kiislamu bali shughuli zozote zinazohusiana na pombe. Kuhusu hili, Mtume Muhammad (S.A.W) anasema katika *hadith sahih*. *Hadith* nambari 3674 katika *Sunnan Abu Dawood* na *hadith* nambari 3380 katika *Sunnan ibn Majah;*

> *"Mwenyezi Mungu ameilaani pombe, yule anayekunywa, yule anayeimimina (gilasini), yule anayeuza, yule anayenunua, yule anayeitengeza, yule anayetengenezewa, yule anayebeba na yule anayepelekewa."*

Hadith hii iko wazi kabisa kuhusu maswala ya pombe. Kwa mwislamu anayemcha Mwenyezi Mungu huwa si rahisi kujihusisha na anasa zozote zinazohusiana na pombe. Zamda na Yasmin kuwakaribisha Chris na Garincha nyumbani kwao kwa kuwanunulia pombe ni kinyume kabisa na mafunzo ya dini yao ya kiislamu. Huu ni ukengeushi. Zamda na Yasmini kwa kutenda haya wanaonyesha kuwa wamekengeuka kutoka kwa mafunzo ya dini yao. Yasmin anamwambia dada yake;

"*Na wewe Zamda usikae kama kinyago cha mmakonde, chukua shilingi elfu mbili katika mkoba wangu kawanunulie wageni bia, sijui mgeni wetu anatumia nini, kamwulize." (uk. 53)*

Tushaeleza msimamo wa dini ya kiislamu juu ya kushiriki mapenzi nje ya ndoa. Zinaa ni katika madhambi manne makubwa ambayo siku ya kiama yatampeleka mtu motoni moja kwa moja bila hata ya hesabu pindi yasipotubiwa. Mengine matatu ni kunywa pombe, kutowaheshimu wazazi na kuwa kiongozi mwovu. Uswahilini, watoto wa kike haswa hufungiwa ndani na kuchungwa sana ili wasiwaaibishe wazazi wao kwa kupatikana si bikra usiku wa harusi. Kulingana na desturi za uswahilini watoto wa kike hawaruhusiwi kutembea nje usiku sembuse kutembea na mwanamume wakati kama huo. Itikadi hizi zinaonekana kukiukwa na hata kupuuzwa na Zamda na Yasmin wanapoamua kwenda dansini na Chris na Garincha. Yasmin, anapoulizwa na Garincha iwapo shangazi lao hawezi kuwasema watakaporudi nyumbani usiku kutoka dansini, anasema;

"*Unasema nini? Hizi ni enzi za Katibu Kata siyo enzi za Akida na Mudir." (uk. 56)*

Anaposema haya, Yasmin anamaanisha kuwa zama wanazoishi si za kitambo. Mambo yamebadilika na mila kama hizo za kitambo za wanawake kutawishwa zimekwisha kupitwa na wakati. Huku ni kukengeuka kutoka kwa tamaduni za jamii na pia dini yake ya kiislamu inayokataza wanawake kutangamana na wanaume hasa faraghani. Mtume Muhammad (S.A.W) anasema:

Hawatakaa pamoja mwanamume na mwanamke faraghani isipokuwa Shetani ni wa tatu wao. (kutoka kwa Ahmad, Tirmidhi na Hakim).

Shetani hapa anachukuliwa kama kiumbe anayewalaghai na kuwashawishi wanadamu waingie katika maasi na kumwasi Mola wao. Basi mwanamume na mwanamke

wanapokuwa faraghani shetani naye huwa pale kuwashawishi watende maasi kama vile kuzini hata kama hawakuwa na nia hiyo. Ndio maana faragha ya wanawake na wanaume wasiohusiana kinasaba haifai katika dini ya kiislamu. Zamda na Yasmin kwenda dansini na wanaume na kuwa faragha nao ni kukengeuka kutoka mafunzo haya.

Tumetangulia kusema pia kuwa katika mila za uswahilini mwari angewaaibisha wazazi wake endapo atakuwa si bikra usiku wa harusi yake. Kitambo, kitanda cha maharusi kingetandikwa shuka nyeupe ili ile damu ya kuvunjwa ubikra ionekane, kisha ile shuka ingepelekwa kwa shangazi za bibi harusi na wangeshangilia wifi yao aliwalelea mwana vizuri. Utamaduni huu ulichukuliwa muhimu sana hasa na hao wanawali wenyewe kiasi kwamba endapo angehiari kufanya mapenzi kabla ya ndoa basi angeruhusu aingiliwe kinyume na maumbile ila asiharibiwe usichana wake (kuvunjwa ubikra). Dhana hii ni muhimu sana uswahilini kwa sababu pia imesisitizwa na dini kuwa msichana atakayeolewa bila kujihusisha na mahusiano yoyote ya kimapenzi (hasa ngono) nje ya ndoa basi atakuwa sababu ya wazazi wake kuingia peponi siku ya kiama. Kwa mapenzi ya dini na ya wazazi wao, wasichana wengi hujilinda wasifanye zinaa.

Hata hivyo, hivi sivyo hali ilivyo kwa Zamda na dadake Yasmin. Dada hawa wanaonekana kukengeuka kutoka kwa maadili haya ya jamii na mafunzo ya dini yao. Mbali na kucheza densi na pombe, Zamda na Yasmin wanashiriki mapenzi na Chris na Garincha nje ya ndoa;

Zamda… Ni yeye aliyekuwa kimada wa Chris. (uk. 50)

Saad, baba yao akina Zamda na Yasmin anakerwa na swala la wanawe kukaa nje usiku na hasa kwa jumla jinsi vijana wanavyofanya mapenzi kiholela;

“Wasichana gani hawa!... kama si umalaya ni nini? Msichana anayetarajiwa kuolewa asiwe nyumbani? Nilisema. Wako wapi? Wasichana wa siku hizi wala hawana kuolewa wala kuachika ni Malaya. Huo ndio uhuru tuliowaletea. Ndiyo manaa

wanathubutu kuimba kuwa kula na kulala na vijana ndio uhuru kamili wimbo gani huo…" (uk. 97)

Saad ni mzee, na tamaduni ambazo tumetangulia kuzitaja hapo juu bado anazijua na anazithamini. Ndio maana alipofika mjini kwa dada yake ilhali binti zake hawakuwa nyumbani alikasirika na kuziita tabia zao hizo za kuzurura ovyo na wanaume kuwa ni za kimalaya. Zamda na Yasmin kutenda matendo haya ya kuzurura usiku na wanaume kunaonyesha wamekengeuka kutoka kwa maadili ya jamii na mafunzo ya dini yao ya kiislamu.

Osore Miriam (2008) anasema Waafrika wanathamini wema na uovu na jambo hili limewafanya kuwa na kaida nyingi za kuongoza jamii… na kwao zinaa hushusha thamani ya mwanajamii… katika jamii kama za Waswahili ubikra huthaminiwa sana. Wasichana wanaotunza ubikra huchukuliwa wenye tabia nzuri… kwa Wakikuyu wasichana walifaa kupatikana bikra walipoolewa. Wale waliopoteza ubikra wao kabla ya harusi wakati mwingine ilibidi wadanganye ili wakubalike katika jamii.

Kauli hii ya Osore (keshatajwa) inaonyesha kuwa kulinda ubikra lilikuwa jambo la lazima katika tamaduni za Kiafrika. Zamda na Yasmin kushiriki katika ngono za kiholela ni kukengeuka kutoka kwa kaida hizi za jamii na za dini pia.

4.5.8 Eliza anajichanganya na wachumba wawili

Katika *Harusi ya Wendawazimu* Eliza ni msichana anayesawiriwa kukengeuka kimaadili. Kwanza anakubali uchumba wa Garincha. Hadi kuwa mchumba wa Garincha ni kuwa alijipendekeza kwake na kuhakikisha anamteka Garincha kwa urembo wake aliokuwa nao. Baada ya kukubali posa, Garincha anapata ufadhili wa kusomea Uingereza. Chris ambaye alikuwa rafiki ya Garincha akarudi kutoka Ujerumani alikokwenda kusoma. Bila kujua kuwa Chris na Garincha walikuwa marafiki, Eliza

akakubali posa kutoka kwa Chris pia. Akawa na wachumba wawili wakati mmoja. Kuwa na wanaume zaidi ya mmoja ni kinyume kabisa na maadili ya dini na ya kiafrika, sembuse wanaume hawa wawe wachumba wako. Ila Eliza anajipata na wachumba wawili.

Siri ilipofichuka uchumba na wanaume wote wawili ukavunjika. Eliza akakimbia kwa mwanamume mwengine, Jim Kichaa, aliyemteka bakunja amwoe. Baada ya ndoa, Jim Kichaa anashikwa na kufungwa, Eliza anabaki bila mume. Anarudiana na Chris aliyekuwa ashamwoa Zamda. Mwishowe, Eliza anabaki kuwa katika uhusiano usio wa halali na mume wa mtu. Hiki ni kinyume na maadili ya Kiafrika na hata dini. Eliza amekengeuka.

Kuhusu wahusika wa namna hii Mayaka (1991) anasema kuwa kinyume na matarajio ya wanajamii kuwa wasomi watakuwa na adabu njema na mfano mzuri wa kuigwa, matendo yao ni ya aibu. Hawaleti tumaini. Wanaishia kutengwa na jamii kwa sababu ya mtazamo wao wa maisha pamoja na vitendo vyao. Fikra zao zimekwama kwenye nia ya kuwagandamiza wanawake kwa upande wa wavulana. Wasichana wanajiachilia ovyo na kukosa uadilifu. Wanajitakia uhuru lakini unakuwa ni uhuru wa kukiuka mipaka ya maadili ya jamii. Kinachobainika ni ukengeushi wa ukosefu wa adabu. Maneno haya ni thibitisho kuwa matendo ya Eliza ni ya kikengeushi. Amekengeuka kimaadili.

4.5.9 Vijana katika mkesha wa harusi wamekengeuka kimaadili

Katika jamii za Afrika, ngono inafaa kuwa kitendo kitukufu na ambacho kinafaa kufanywa na watu waliooana pekee, ndio maana ikaitwa ‘tendo la ndoa’. Haifai kufanywa ila na waliooana. Katika sherehe ya mkesha wa harusi katika riwaya ya *Harusi ya Wendawazimu*, vijana waliohudhuria wanasawiriwa wakijihusisha katika tendo la ndoa kiholela. Si hivyo tu bali wanabadilishana wasichana. Kuzini na msichana

mmoja au mvulana mmoja kunaweza kuchukuliwa kama jambo la kawaida hasa katika enzi hizi za sasa. Ila kukusanyika chumba kimoja watu wengi mkifanya ngono na kubadilishana ni thibitisho kuwa vijana hawajakengeuka tu bali wanachukulia ngono kama mchezo wa kawaida. Huu ni ukengeushi mkubwa wa maadili ya dini na jamii;

Chumba cha bafu kilikuwa tayari kimejaa wavulana na wasichana wengine walikuwa wanabadilishana wasichana. (uk. 123)

Kubadilishana wasichana kunaashiria kuwa hata hao waliokuwa wakishiriki ngono hawakuwa wapenzi, ni watu waliokutana wakaamua wafanye ngono. Watu wanaopendana hawawezi kubadilishana wapenzi. Huwaonea wivu.

Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) ya Kezilahabi, tunakutana na wahusika vijana wanaopigwa hadi kufa kwa kupatikana wakifanya ngono kwenye kichaka karibu na sherehe za kitamaduni zinazoendelea. Mayaka (1991) anasema sababu kubwa ni kuwa hawa vijana waliudharau utamaduni na watu. Na kuwa kitendo walichokitenda vijana hao kikiangaliwa kwa jicho la kimagharibi si chochote cha kufikiriwa lakini katika utamaduni wa jadi ni kibaya mno.

Kauli hii ni thibitisho kuwa ngono za kiholela si jambo la kawaida katika jamii za Afrika na vijana kufanya hivyo ni kukengeuka. Kushiriki zinaa ni kosa kubwa kidini na kimaadili ya Kiafrika. Kuwa vijana katika mkesha wa arusi walibadilishana wanawake haswa ni ukengeushi mkubwa wa maadili.

4.5.10 Saad Mwendawazimu anakengeuka na dini

Tangu atambulishwe katika riwaya ya *Harusi ya Wendawazimu*, Saad Mwendawazimu amesawiriwa kuwa mtu mkali na mwenye misimamo mikali hasa ya kidini. Ni Saad yuyu huyu ambaye alithubutu kuzikataa posa za binti zake Zamda na Yasmin kwa misingi ya tofauti ya dini kati ya binti zake na wanaume waliotaka kuwachumbia- Chris

na Garincha. Hata hivyo, Saad Mwendawazimu baadaye anasawiriwa akibugia pombe kwa hasira katika mkesha wa harusi ya binti zake. Huku ni kukengeuka kutoka mafunzo ya dini yake. Tushatangulia kuonyesha msimamo wa dini yake ya kiislamu kuwa ulevi haujakatazwa tu, bali mtu yeyote anayejihusisha na pombe, kuanzia upanzi wa matunda kwa nia ya kutengeneza pombe amelaaniwa na Mwenyezi Mungu. Kwa kunywa pombe, Saad Mwendawazimu amekengeuka kutoka kwa mafunzo ya dini yake aliyosawiriwa kuishika thabiti hapo awali;

Saad Mwendawazimu alikuwa amekaa kwenye meza peke yake huku akiendelea kushambulia chupa ya 'John Walker' kwa hasira kama kwamba ndiyo ilikuwa imembeua. (uk. 119)

Mwandishi anaendelea kuonyesha kuwa Saad Mwendawazimu alikuwa bado anakunywa pombe;

Katika ukumbi, Bwana Saad, baba yao Yasmin na Zamda alikuwa anaendelea kunywa pombe kali ya 'John Walker'. (uk. 125)

Kwa matendo yake haya ya kunywa pombe, Saad Mwendawazimu amekengeuka kutoka katika maadili ya dini yake ya kiislamu.

4.5.11 Buda anakengeuka kimaadili

Buda alikuwa mwalimu wa shule ya msingi kwa miaka mingi. Alikuwa amefikia cheo cha mwalimu mkuu. Alikuwa tayari ashavuta umri kiasi. Kulingana na umri wake na heshima ya kazi yake kuna mambo ambayo alitarajiwa asiyafanye. Hata hivyo, Buda anasawiriwa akikengeuka na kuanza kushiriki katika mambo ambayo mzee kama yeye hayamfai. Isitoshe anayafanya na vijana wadogo ambao wengine aliwafunza shule ya msingi.

Siku ya harusi Buda anasawiriwa akishinikizwa na vijana wadogo kumliko kujiunga katika mchezo wao wa *The dance of silence.* Katika mchezo huu wachezaji walitakikana kuvua nguo zote isipokuwa chupi kwa wanaume na chupi na kanchiri kwa wanawake. Kunao walioona aibu wakaondoka hawakushiriki. Buda, japo aliona aibu mwanzoni alishinikizwa naye akavua nguo mbele ya watu;

Wachezaji mara walijidai kuchoka, wakajidai kuoga walianza kuvua nguo. Wavulana walibaki na chupi na wasichana walibaki na chupi na kanchiri. Wengi hawakuona aibu kwani walikuwa wamelewa au wameyazoea, walioona aibu na kugoma kuvua walizomewa wakavua au wakaondoka. Buda alizomewa akakubali kuvua na kushiriki kikamilifu. (uk. 150)

Taswira hii inamsawiri Buda akikengeuka na kushiriki katika michezo ya aibu na vijana ambao si wa rika lake, wakiwemo wanafunzi wake. Huku ni kukengeuka kimaadili. Na kukengeuka kwake hakukuishia pale harusini tu. Aliendelea kushiriki mapenzi na Nora aliyekuwa mwanafunzi wake na akakiri kuwa amekubali kujitia hamnazo na kuwekwa kimada na mwanafunzi wake kwa sababu huo ndio mtindo mpya japo hakuna mapenzi kati yao. Buda anasema katika dondoo hii;

"...Mbinu za kuishi ni nyingi hapa jijini, kama Nora ana uwezo wa kuniweka kimada kwa nini nisijitie hamnazo?" (uk. 160)

Mwanamume, hasa mzee kuwekwa kimada na mwanafunzi aliyemfunza –ambaye anafaa kuwa kama mwanawe ni kukengeuka kimaadili. Buda anaendelea;

"Nakwenda kwa Nora. Najua hanipendi lakini inamsaidia kumfikiria Garincha. Kwaheri." (uk. 151)

Hata wale kachala aliokuwa akinywa nao pombe walimshangaa na kumuuliza sababu ya kushiriki mapenzi na watoto wadogo ambao wengine walikuwa wanafunzi wake.

Buda alikiri kuwa mji ule ulimchanua ukamfunza mambo mapya na hayo ndiyo anayoyafuata;

"*Buda leo nataka utuambie ile kweli yako, kwa nini unatembea na watoto ambao wengine waliwahi kuwa wanafunzi wako?"* (uk. 159)

Swali hili, hasa kutoka kwa vijana wadogo kumliko Buda linaonyesha kuwa tabia aliyokuwa nayo ya kujihusisha kimapenzi na wasichana wadogo ambao hata wengine aliwafunza shule ya msingi haikuwa tabia ya kawaida Buda kuwa nayo. Ilikuwa kinyume kabisa na maadili ya jamii. Katika jibu lake Buda alijitetea kwa kukiri kuwa amekengeuka na mji ndio uliomkengeusha;

"Nilipohamishiwa hapa sikujua huu mji na kwa ujinga wangu mji umenichukua. Lakini nimejifunza… tangu siku hiyo nimekuwa mwanafunzi kwa kila namna. Najifunza ya kisasa, niliyojua mimi hayatumiki tena. Sasa hivi niko darasani najifunza…" (uk. 159) Buda amekengeuka. Hata vijana wanaona kuwa ni makosa kwa mtu kama yeye kuyafanya hayo ya kulala na wanafunzi wake ila yeye haoni makosa na anajitetea kwa kusema kuwa ndio anajifunza. Huku ni kukengeuka.

Kuonyesha kuwa tabia hii ya wazee kulala na wasichana wadogo kiholela ni kukengeuka, Mayaka (1991) anamtaja mhusika Deogratias katika riwaya ya *Rosa Mistika* kuwa wakati wake mwingi anautumia kutafuta wasichana na kuwapeleka katika sherehe za starehe. Vilevile anamtaja mwalimu mkuu wa chuo cha ualimu cha Morogoro Bw. Thomas anayekitumia cheo chake kama mwalimu mkuu ili kushiriki ukahaba na mwanafunzi wake Rosa. Mayaka (keshatajwa) anasema huyu ni kiongozi wa chuo ambaye anatarajiwa kutetea nidhamu na adabu njema kwa wanafunzi. Kinyume na hayo, yeye ni gwiji wa ukosefu wa nidhamu.

Kauli za Mayaka (keshatajwa) zinaonyesha kuwa tabia ya Buda kulala na wasichana wadogo aliowafunza si tabia inayotarajiwa kutoka kwake na jamii. Huku ni kuonyesha kuwa Buda amekengeuka kutoka kwa maadili ya heshima ya jamii aliyomo.

Buda ni mwalimu mkuu wa shule ya msingi. Anatarajiwa kutetea nidhamu na kuwafunza watoto na vijana namna ya kukabiliana na maisha kiuadilifu katika enzi hizi mpya za usasa. Ila kinyume na hayo yeye ndiye gwiji wa ukosefu wa nidhamu. Anaruhusu watoto wadogo wamwelekeze yeye mzee katika uasherati badala ya yeye mzee kuwarekebisha na kuwaelekeza vijana katika njia za heshima. Buda amekengeuka.

4.6 Utamaushi

Kwa mujibu wa mdhanaishi Sartre (keshatajwa), kwa kuwa mwanadamu hana uwezo juu ya masuala kama maumivu na mateso, anaweza kukata tamaa. Njia moja ya kuonyesha kukata tamaa ni kujitoa uhai mwenyewe.

Santosh Kumar Nayak (2018) anaeleza kuwa mwanadamu ni kiumbe kinachoweza kufikiria na kuwa na ndoto za kufikia malengo fulani maishani mwake. Ila ndoto hizi zinapokumbana na ukweli wa maisha zikaporomoka humchanganya mwanadamu. Kutokana na haya, mwanadamu anapojiua ni sawa na kukiri kuwa si muhimu kuendelea kuishi na kupambana na kweli ya maisha. Bila kukubali ukweli wa maisha, mwanadamu anakengeuka na kuwa mpweke. Anatamauka kwa kuuona ulimwengu kama pahali katili pa kuishi na mawazo haya ndiyo humfanya mwanadamu kutamani kifo na hatimaye kujiua.

Wahusika wafuatao wa riwaya za *Harusi ya Wendawazimu* na *Kitu Kidogo Tu!* wanasawiriwa wakikata tamaa na wengine kujitoa uhai.

4.6.1 Katoto wa Minane anatamauka na kujiua

Katoto wa Minane ni mhusika katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* ambaye alijitoa uhai kwa kujitia kitanzi kwa ugumu wa maisha. Katoto alikuwa mkimbizi aliyepewa hifadhi katika kijiji cha Mushule baada ya kukimbia vita vya wao kwa wao vilivyoangamiza familia yake yote huko nyumbani kwao Burundi. Tangu apewe hifadhi, Katoto wa Minane aliishi kwa matatizo siku zote. Maisha yake hayakuoneka yakiwa na maendeleo yoyote. Hakuwahi kuoa wala kuwa na uhusiano wowote. Matatizo haya ndiyo yaliyomfanya akakata tamaa ya kuendelea kuishi na hivyo akajitia kitanzi kama dondoo hii inavyodhihirisha;

> …*Katoto wa Minane alikuwa ananing'inia kwenye kamba huku kichwa chake kimeinama upande wa bega la kushoto.* (uk. 110)

Katika maisha hasa haya ya kibepari watu wamefanya tabia ya kuiweka maana ya maisha yao katika vitu wanavyovimiliki kama vile magari, majumba na biashara. Wengine ambao bado wanauthamini utu hueka maana ya maisha yao katika familia zao, hasa za nyuklia. Endapo kutatokea kitu chochote kitakachoangamiza mali zao au familia zao basi watu hawa huwa wamepoteza maana ya maisha kabisa na mara nyingi huishia kujitoa uhai. Kwao maisha yatakuwa hayana maana tena kwa kuondokewa na vitu walivyomiliki na kuvithamini.

Visa vingi vimeripotiwa vya watu kujitoa uhai kwa kuwapoteza wapenzi wao na hivyo kuona maisha yao hayatakuwa na maana tena kuishi bila wapenzi wao. Romeo na Juliet katika tamthilia ya *Romeo and Juliet* ya William Shakespeare (1597), ni mfano mzuri wa wapenzi wanaojitoa uhai kwa kuona hawawezi kuishi bila ya mwengine.

Aidha, visa vingi vimeripotiwa watu wakijitoa uhai kwa kushindwa kulipa mikopo waliyochukua kwa watu au benki. Katoto wa Minane alijasiria kuendelea na maisha jinsi yalivyo baada ya kupoteza familia yake yote, akitarajia kuwe na maendeleo ila

hayakuwa. Basi akaamua naye kujitoa uhai. Katika hotuba yake kwa wanakijiji, bwana mwenyekiti Petro anathibitisha hili;

"…Bwana katoto kajitoa roho mweyewe…" (uk. 116)

Kukata tamaa na kujitoa roho ni kati ya sifa moja kuu ya udhanaishi, hasa ugumu wa maisha na ubwege unapochangia kuchukua hatua hii.

Ezra Mose (2005) anamnukuu Emile Durkheim (1957) kwamba watu wengi hujiua katika jamii zinazosheheneza ubinafsi na tadi. Katika jamii hizi, kila mtu hujitahidi kivyake kuendeleza maisha yake na anaposhindwa, aghalabu kifo huwa suluhisho. Haya ni maelezo yanayoeleza vizuri hali ya Katoto wa Minane.

Tushatangulia kusema kuwa hata wale majirani wa Katoto wa Minane hawakuwa na hakika juu ya imani ya dini yake. Hakuwahi kuonekana kuwa na shughuli zozote za kidini. Bila shaka kama ilivyokuwa baada ya vita vya pili vya dunia, vita vya wao kwa wao huko Burundi vilivyoangamiza familia yake nzima vilimwathiri vikamkengeusha kama vilivyowafanya akina Sartre kule Ulaya. Hata hivyo, Katoto wa Minane alikuwa na matumaini ya kuyapa maisha yake maana kwa kuanza upya katika nchi mpya. Sivyo mambo yalivyokuwa kwa sababu alizidi kuteseka akashindwa hata kuoa. Tariq (2017) anamnukuu Nietzsche (1961) akisema kuwa matumaini ni aina mbaya kabisa ya uovu kwa sababu yanamzidishia mwanadamu muda wa kuteseka. Naye Katoto wa Minane hakupata natija yoyote katika matumaini yake ya kuanza maisha katika nchi nyingine. Aliteseka hadi akaamua kujiua.

Katika jamii za Kiafrika, mtu anapokufa huambiwa ameenda kupumzika. Kutokana na haya ni bayana kwamba Waafrika huchukulia kifo kama njia moja ya kuyakimbia matatizo ya ulimwengu kama vile maradhi sugu, na mja hupata kupumzika na dhiki za ulimwengu pindi anapoiaga dunia. Ndio maana katika jamii ya Waduruma mtu

anapokufa huambiwa akalale “pehoni”. *Pehoni* ni pahali penye upepo mwanana wa kuvuvia na mja huburudika anapojipumzisha kwenye makazi haya. Hali hii ya kuchukulia kifo kama pumziko pia inapatikana katika riwaya ya *Rosa Mistika*. Rosa anasawiriwa akifurahia baada ya kunywa sumu kuwa kifo kinamkaribisha. Anakishukuru kifo kwa kumwondolea dhiki ya kuishi duniani;

Rosa alifikiri kwanza kabla ya kunywa…Alikunywa maji yale... Aliona damu...'Asante. Kifo njoo upesi' alisema…'sasa ninakufa; ninakufa sasa. Maisha yangu yalikuwa magumu.' (uk.91)

Osore Miriam (2008) akizungumza kuhusu kifo hiki cha Rosa anasema; jinsi kifo cha Rosa kinavyosawiriwa kinaonyesha kuwa maisha ya Rosa yalikuwa magumu mno. Anakifurahia kifo akitumai kingempumzisha na ugumu wa maisha. Katika maisha yake yote Rosa hajawahi kuwa na faraja… Kezilahabi anayasema haya (kupitia kauli ya Rosa) kurejelea ile imani ya Kikristo kuwa mbinguni kuna raha kuliko duniani.

Hivyo, Katoto alijiua ili kwenda kupumzika dhiki zote za ulimwengu huu wa kibwege usiokuwa na maana yoyote. Hii ndiyo suluhu wanayotoa wadhanaishi kwa matatizo ya wanadamu katika ulimwengu huu.

4.6.2 Mahabusu anatamauka na kijiua

Mose (2005) anamrejelea Cruickshank (1958:40) anayemrejelea Albert Camus kwamba ni haki ya mtu kujiua ili kujiepusha na maisha magumu.

Katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* wapo wahusika wanaojipata jela kwa kuhusishwa na kifo cha Katoto wa Minane ambaye alijiua mwenyewe. Wahusika hawa wanasawiriwa wakikata tamaa na wengine kujiua. Kwa sababu kule rumande maisha hayaendelei, kila siku taratibu ni zile zile, ukiongeza na kunyimwa uhuru wa kutembea. Nayak (2018) akizungumzia swala hili la maisha kujirudia kila siku anamrejelea Camus akisema mbali na kuwa mwanadamu anaishi akiwa na matumaini kuwa maisha yana maana fulani, ila

kurudia nyendo zile zile kila siku: kulala, kuamka, kwenda kazini, kulala na kulala tena kila siku ya wiki kuna uwezekano mwanadamu akawazia kujiua kwa kujiuliza kama ni muhimu kwake kwendelea kuishi.

Siku nne baada ya mazishi ya Katoto katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* polisi ambao walikuwa wameitwa kwa takriban siku tatu wakisema hawangeweza kufika kwa sababu hawakuwa na usafiri hatimaye walifika kijijini Mushule. Wenyeji walipigwa fimbo kisha wakalazimishwa kuufukuwa mwili wa Katoto kwa kucha zao. Watu kumi na wawili walitiwa mbaroni akiwemo Abdu Shaaban, binamu yake Musa Nshomile kwa kosa la mauwaji ya Katoto. Ila kwa kuwa idara zote za serikali zilikuwa zimezorota na hata huko mahakamani hakukutolewa haki yoyote, washukiwa hawa waliishia kubaki rumande kwa miaka. Hata hivyo, watatu waliachiliwa, wawili wakakimbia na wanne wakafia jela. Kati ya hao waliokufa jela ni mahabusu mmoja ambaye alijitoa uhai baada ya kukata tamaa ya kesi yao kusikizwa na kuamuliwa kwa sababu hata faili zao zilisemekana kupotea. Abdu anasema;

"Mimi sijui, wala sijui nyenzo alizozitumia alizipataje. Ninachokumbuka siku za karibu na mwisho wake alianza kubadilika. Akawa hataki kusema na mtu, hata mimi mtuhumiwa mwenziye. Nakumbuka usiku wa siku ya mwisho aliniita akaniambia, "Abdu unajua nina mke na watoto watatu," akasema, 'ukijaaliwa kurudi nyumbani wape salamu hizi, salamu za mwisho. 'Nikamuuliza kwa nini alikuwa anasema hivyo, akanijibu kuwa usiku ule alitarajia kulala usingizi wa mwisho, usingizi usio na mwisho. Nilimkataza asiendekeze mawazo hayo. Kesho yake asubuhi alikutwa ananing'inia chooni." (uk. 124)

Hiki ni kifo chengine cha kujitia kitanzi na sababu ni ile ile kukata tamaa. Kwa sababu alianza kuonyesha ishara za kukata tamaa na maisha. Kama Abdu anavyosema kuwa mahabusu mwenzake alianza kubadilika akawa hataki kuongea na watu hata yeye Abdu,

waliokuwa watuhumiwa sawa. Tabia kama hii ni ya kuonyesha kukata tamaa kwa sababu hata katika riwaya ya *The stranger* ya Albert Camus (1946), mhusika Mersault alipohukumiwa kinyongo, siku chache kabla ya kunyongwa alionyesha kukata tamaa na maisha na akawa hataki hata kuongea na padre aliyekuwa akija kuzungumza naye akijaribu kumpa moyo.

Mayaka (1991) akichambua riwaya za Kezilahabi anasema mwandishi ameathiriwa na falsafa ya utamaushi kwa kiasi kikubwa. Haya yanabainika katika usawiri wake wa wahusika ambao wameonyeshwa kama waliokata tamaa. Kifo kimetolewa kama suluhisho la maisha ambayo yamekosa maana. Na katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* kifo ndio suluhisho aliyochukua huyu Mahabusu alipokata tamaa kwa maisha yake kukosa maana, haswa kwa kushikwa na kuwekwa kwa kosa asilolijua ndewe wala sikio. Isitoshe, haijulikani humo rumande angetoka lini. Haya yote yalimtamausha.

4.6.3 Abdu anatamauka baada ya kukaa rumande kwa miaka

Katika mazungumzo na binamu yake Musa Nshomile, Abdu anaonyesha kutamauka baada ya kuwa mahabusu na kusubiri kwa miaka kesi yake isikizwe na iamuliwe lakini haikuwezekana, kwa sababu faili ya kesi yao ilipotea. Alipoteza matumaini ya kuwachwa huru. Iko wazi katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* kuwa Katoto alijitoa uhai mwenyewe, ila kesi ikasingiziwa Abdu na wanakijiji wenzake kumi na mmoja kwa kuwa walihusika katika kuripoti kifo cha Katoto kwa polisi ambao walishindwa kufika mapema. Na pia kwa kuwa walihusika katika mazishi ya Katoto. Abdu anajua kuwa hana hatia yoyote kuhusiana na kifo cha Katoto ila kwa kuwa amekaa rumande kwa miaka mingi na hakuna mwelekeo wowote wa kueleweka kuhusu kesi yake, amekata tamaa na maisha na yuko radhi kukubali makosa na pia yuko tayari kutumikia kifungo au hukumu yoyote ile hata kama ni ya kunyongwa. Huku ni kukata tamaa na maisha jinsi yalivyo. Abdu anamweleza Musa;

"*Sidhani kama una lolote la kuweza kusaidia. Laiti faili ya kesi yangu ingepatikana ningekuomba usaidie katika kumwomba hakimu au jaji aitishe kesi mimi nikubali kosa, nitiwe hatiani nipewe adhabu na kuanza kutumia adhabu na kunyongwa." (uk. 124)*

Alipoulizwa na Musa kwa nini akubali adhabu ya kosa ambalo hakulitenda, Abdu anasema;

"*Bora kupewa adhabu kwa kosa ambalo hukulitenda kuliko kuwa katika jehanamu hii bila kujua utatoka lini au utakufa kwa ugonjwa gani. Kwa kukosa hewa, au kukosa maji au kukosa chakula, au kufa kwa kulawitiwa. Wengine wanakufa kwa kubakwa. Hebu, fikiria humu ndani tuna kijana mmoja ambaye alifikishwa mahakamani na kushitakiwa kwa kosa la kuiba nanasi. Hakimu alimuuliza kama anakubali kosa au la. Alikana kosa. Laiti angekubali angepewa adhabu miezi sita au sanasana mwaka mmoja. Lakini sasa tunaye humu zaidi ya miaka mitatu sasa. Wahalifu wazoefu wanamfanya bibi na huenda akafa kwa kulawitiwa." (uk. 124)*

Haya ni mawazo ya mtu aliyekata tamaa na maisha yake namna yalivyo na yuko tayari kwa lolote hata kama ni kifo ili aondokane na maisha hayo ya kujirejelea bila kubadilika. Mambo yote ambayo Abdu aliyaona mle rumande yalimkatisha tamaa. Hii ndio sifa kuu ya waandishi wa kidhanaishi. Kuwasawiri wahusika katika hali na mazingira ya mateso na kutamausha. Kadhia yote anayokumbana nayo jela inamtamausha Abdu.

4.7 Kuabudu mahitaji ya kimwili

Kwa vile binadamu yuko huru kufanya anachotaka, ni wajibu wake kushughulikia mahitaji yake ya kimwili kwa njia anayotaka yeye. Hivyo ni sawa mtu kushiriki katika matendo kama zinaa (ngono kiholela), ngono za jinsia moja, kuwa na wapenzi wengi,

kulewa n.k ili kukidhi mahitaji ya mwili wake. Kwa wadhanaishi, taasisi kama ndoa si muhimu alimuradi mtu anapata mahitaji ya mwili wake.

Tushatangulia kueleza kuhusu namna Sartre na Simone de Beauvior walivyoamua kutumia uhuru wao kufanya ngono kiholela bila kujali kuwa na mpenzi mmoja au kutulia ndoani. Kwao ilikuwa ni kusherehekea na kuutumia vilivyo uhuru waliojipatia kwa kudai “kifo cha Mungu”. Hata hivyo, kwa wale ambao bado wanamwamini Mungu na wana dini zao wanazozifuata, watakapoamua kushiriki mapenzi kiholela nje ya ndoa. Watakapoamua kujiingiza katika ulevi na anasa kwa kufuata matamanio ya nafsi zao, basi watakuwa wameamua kuabudu mahitaji ya nafsi zao na kwenda kinyume na dini na itikadi zinazowawekea mipaka.

Hadi kufikia karne ya ishirini, si dini tu zilizoshikilia imani kuwa mwanamke anapoolewa akiwa bikra, huchukuliwa kuwa mtu mwenye kujiheshimu na huthaminiwa. Tumetangulia kusema kuwa Uswahilini maharusi waliekewa shuka nyeupe ili kuthibitisha ubikra wa bibi harusi endapo kungekuwa na damu. Ilipokoseakana damu hii ilikuwa aibu sana kwa wazazi wa bibi harusi, hasa mamake, na ingesababisha kukosana na wifi zake. Wanawake wengi hutalikiwa usiku huo huo wa harusi wanapopatikana si bikra.

Katika jamii ya Waduruma itikadi kama hizi zilikuwepo pia. Bibi harusi, katika ndoa zilizofanywa kwa desturi na wala si kwa *pkwiya* (msichana kuibwa na kuwekwa kinyumba kinyume cha sheria) pia alitarajiwa kuwa bikra. Endapo angepatikana si bikra, shangazi zake mume wangechukua nazi wakaitoboa kisha wakaipeleka kwa akina mke kuwaonyesha kuwa mtoto wao walimpata akiwa ‘wazi’ tayari kama ile nazi. Hii pia ilikuwa aibu kwa familia ya bibi harusi. Jamii nyingi zimewacha hizi itikadi ila katika dini bado zinafuatwa na zinafaa kwendelea kufuatwa hadi siku ya kiama. Na kuna adhabu zilizowekewa wazinifu hapa duniani na pia siku ya kiama.

Watu wote wanaoamini dini hawafai kujihusisha na zinaa, endapo watafanya hivyo watakuwa wamekiuka mafunzo ya dini na kupatiliza zaidi mahitaji ya miili yao. Na hata wale ambao hawaamini dini ni vyema kuwa na mpenzi mmoja, ila ikiwa mtu atakuwa anazini na watu tofauti kwa kuvutiwa na maumbile yao pia huko ni kuabudu mahitaji ya kimwili. Kwa mwanamume na hata kwa mwanamke kuna sifa fulani wakiziona kwa jinsia nyengine huwatamanisha kufanya ngono nao. Kwa mfano wanaume wanapoona mwanamke mwenye umbo zuri, au makalio makubwa, au maziwa makubwa kifuani huwapa mshawasha wa kutaka kulala naye. Endapo atadiriki kulala na kila mwanamke atakayemvutia na akatumia pesa kuwashawishi, basi atakuwa anaendeshwa na shahawa zake kuliko akili yake. Huko ni kuabudu mahitaji ya kimwili kama inavyojitokeza:

4.7.1 Musa Nshomile anaishi na Irene bila ndoa

Kuhusu Musa na Irene, mwandishi anasema;

Kwanza, uhusiano wao ulikuwa wa mazungumzo, baadaye ukawa wa kutembeleana na hatimaye ulifikia hatua ya kutembea pamoja, mara walale kwa Irene mara kwa Musa. Ilipochosha waliamua kuishi pamoja. (uk. 4)

Mwanamume na mwanamke huamua kuishi pamoja ili kukidhiana mahitaji yao ya kimwili. Haya hufanywa kulingana na kanuni maalumu zilizowekwa kihalali, yaani ndoa. Vinginevyo wakishindwa kuvumilia hadi watakapofunga ndoa ni kuwa wameshindwa kudhibiti mahitaji ya miili yao na kuyawacha yawapeleke, huku ni kuabudu mahitaji ya kimwili. Katika dini, haya ni makosa kwa sababu Mungu wa kuabudiwa yuko na anasema binadamu asikurubie zinaa. Binadamu akishindwa kujizuia atakuwa hamwabudu Mungu tena ila anaendeshwa na mahitaji ya mwili wake.

4.7.2 Eliza ashiriki mapenzi na wanaume watatu

4.7.2.1 Eliza na Garincha

Kulingana na *Kamusi Elezi ya Kiswahili*, ashiki ni ‘uchu, tamaa, hamu au nyege ya mwanamume au mwanamke ya kutaka kufanya mapenzi au ngono’. Hivi ndivyo macho ya Eliza yalivyoonyesha alipomtembelea Garincha nyumbani kwake na kujaribu kujieleza hisia zake. Baada ya kuonyesha uchu huu Eliza na Garincha walishindwa kujizuia kupapasana na kulazana kwenye kochi, isingelikuwa ni siku ya kwanza kukutana katika mazingira haya basi jambo hili lingesababisha ngono. Hata hivyo, haukupita muda mrefu Eliza na Garincha wakaanza kulala pamoja kimapenzi. Mwandishi anasema;

Eliza aliinua macho na kumuangalia Garincha usoni kwa macho maang’avu. Halafu alifanya kitu cha ajabu sana: kwa ghafla alitupa leso na mkoba wake chini na haraka alimkumbatia Garincha kwa nguvu, uso wake akauegemeza kwenye bega la Garincha huku akitaja jina lake tena na tena kama mtu aliyepagawa, alipotulia alirudisha kichwa chake nyuma kidogo na kumwangalia Garincha usoni. Macho yao yalikutana, macho yaliyoonyesha ashiki zaidi kuliko mapenzi.

Eliza alibandika midomo yake kwenye midomo ya Garincha. Busu hili lilimshika Garincha ghafla bila kutegemea. (uk. 16)

Huku ni kuabudu mahitaji ya kimwili. Mwandishi anaeleza vizuri jinsi miili yao ilivyokuwa ikichemka kwa ashiki. Ijapokuwa baada ya wiki tatu tu Garincha alikuwa tayari kwenda kumchumbia Eliza kwao Mbinga, ila kama isingekuwa kuabudu mahitaji ya kimwili wangesubiri hadi waoane kabla hawajaanza kulala pamoja. Kwa sababu dini na mila za Kiafrika zote zinapinga zinaa, ila wanaifanya hivyo hivyo.

4.7.2.2 Eliza na Chris

Baada ya mchumbawe Eliza, Garincha, kusafiri kwenda Uingereza kusoma, rafiki yake mkubwa, Christopher alirudi Tanzania kutoka Ujerumani alikokwenda kusoma. Chris alipoamua kutafuta mchumba alipatana na Eliza na wakawa katika uhusiano wa mapenzi;

Eliza naye alimpa Chris pendo la huba. Chris akawa anaona fahari kuonekana kwa watu akiwa na Eliza. (uk. 33)

Wakati Chris akichukulia uhusiano huo kwa uzito na hata kutarajia ndoa, Eliza alikuwa katika uhusiano huo kwa ajili ya kustarehe na kukidhi mahitaji ya mwili wake kwa kuwa mchumba wake alikuwa mbali. Hakusema lolote kuhusu kuchumbiwa kwake akitarajia wakati Garincha atakaporudi mahusiano yake na Chris yangekuwa yaliisha kitambo. Hii ndiyo sababu Chris alipomwomba uchumba lilikuwa swala zito kwake;

Ombi hili lilimpiga Eliza ghafla kama radi. Hakuwa ameliwazia. Kwanza alikuwa anamwona Chris kama mtu mpenda starehe na uhusiano wao, kama wasemavyo, ukiwa wa 'pastime', hakuwa anawazia kuwa Chris angewazia jambo la kumuoa. Alipoombwa uchumba hakutoa jibu, aliomba muda alitafakari. Na kwa siku kadha alisumbuliwa na dhamira yake. Hakujua afanyeje. Kumkatalia ilikuwa ni kukatisha raha aliyokuwa akiipata, kumkubalia ilikuwa ni kumkana Garincha ambaye licha kuwa alikuwa tayari ameisha toa kiasi kikubwa cha mahari, vilevile alikuwa na huduma zake ambazo Eliza angejuta kuzipoteza. Yote haya aliyaweka kwenye mizani na kuyapima mwisho aliamua kukubali ombi la Chris lakini hakutaka kuvunja uchumba na Garincha, hivyo akajikuta ana wachumba wawili kwa wakati mmoja. (uk. 34)

Dondoo hii inathibitisha wazi kuwa Eliza alikuwa katika uhusiano na Chris ili kustarehe na kukidhi mahitaji ya mwili wake. Kwanza aliingia katika uhusiano na Chris kwa nia ya ku-*pastime* tu na kujistarehesha. Kitu ambacho angekikosa kwa kukatisha uhusiano

wake na Chris kwa kukataa ombi lake la uchumba kwa sababu ya Garincha ambaye alikuwa mbali. Ili aendelee kustarehe na kupata raha alizozipata kwa Chris ilibidi akubali uchumba wake. Aidha, hakutaka kuvunja uchumba na Garincha kwa sababu kama inavyosema dondoo ni kuwa Garincha alikuwa na huduma zake ambazo Eliza angejuta kuzikosa. Kwa hivyo kwa kuabudu mahitaji ya mwili wake Eliza alijikuta akiwa na wachumba wawili ambao walikuwa marafiki wakubwa. Kuabudu mahitaji ya kimwili kulimfanya Eliza akakosa ndoa na harusi ambazo alipanga kuzionea fahari. Mtaka yote hukosa yote.

Katika kujitetea matendo yake ya kumsaliti Garincha, Eliza anafikiria na kujisemea kuwa uaminifu ndo jambo zuri la kufanywa kwa wapendanao ila anakiri kuwa mwili ni dhaifu;

Moyo ungetaka uwe mwaminifu lakini mwili ni dhaifu. (uk. 39)

Hii ni thibitisho kuwa yale anayoyafanya Eliza ni kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya mwili wake ambao ni dhaifu hauwezi kuvimilia kwa muda bila starehe hizo.

Baadaye, katika mkesha wa harusi, mbali na kuwa Eliza alihudhuria sherehe akiwa na mchumba wake mpya- Jim Kichaa ambao pia walikuwa waoane siku iliyofuata, aliamua kufanya mapenzi na Chris. Alimwambia Chris;

"Twende bafuni najua ilipo, twende nkakupe 'one for the road'." (*uk. 119)*

Baadae walikutana kweli kuzima ashiki zao;

Eliza naye alikuwa amemvuta Chris na kumpeleka bafuni na kumlaza ndani ya beseni la bafu. (uk. 123)

Huku ni kuabudu mahitaji ya kimwili. Eliza asingeyafanya haya kama asingekuwa bado anamtamani Chris, na Chris asingekubali kama isingekuwa matamanio yake kwa Eliza.

4.7.2.3 Eliza na Jim Kichaa

Baada ya kukorofishwa na Chris na Garincha kwa kuwaendea kinyume wote wawili, Eliza aliamua kumgeukia Jim Kichaa aliyekuwa akimpuuza na kumwona hafai siku zote. Hata hivyo, badala ya kuzungumza naye tu kuhusu nia yake ya kutaka Jim amwoe, Eliza anaamua kutumia mwili wake kama kigezo cha kumvutia Jim katika mpango wake huo. Alifanya mapenzi na Jim kwanza kabla ya kumwambia nia yake hiyo. Eliza anasawiriwa kutumia mbinu hii ili kupata harusi yake aliyoikusudia badala ya kutulia na kujipanga tena na maisha.

Eliza aliegemeza mwili wake kwenye mwili wa Jim, Jim naye alitazama saa yake ambayo alikuwa hakuvua kabla ya kufanya mapenzi na kuwaza kwa mshangao kidogo kuwa ilibidi yule msichana aanze safari ya kurejea nyumbani kwao.

"Eliza lazima uende sasa, nyumbani, watakuwa wanakutafuta." Jim Kichaa alisema kwa sauti ya kusikika.

Ghafla, Eliza alijichomoa toka kwa Jim, akamwachilia huku akinyoosha mikono yake kiasi kwamba mkono wake wa kulia uligusa zulia hapo sakafuni toka kwenye kochi ndefu. Hapo ndipo Jim na Eliza walipokuwa kwa muda wa saa nne hivi zilizopita. Walipoingia ndani walishikana, wakavurugana, wakihema na kubusiana mpaka wote walipolala, sasa baada ya uchovu, walikuwa bado wamekumbatiana ili wasianguke toka kwenye kochi nyembamba.

"Aise Jim," Eliza alisema huku akisimika mguu wake sakafuni. "Uliwahi kuniambia kuwa unanipenda sana?"

"Hilo nililisema na kadri ninavyokuona ndivyo nazidi kukupenda zaidi na zaidi," alisema Jim. Eliza aliinama akaanza kupekua nguo akitafuta nguo yake. (uk. 82)

Mbali na kuabudu mahitaji ya mwili wake, Eliza haogopi kuutumia mwili wake kama chambo cha kujitimizia mahitaji yake mengine. Anasawiriwa akimzuzua Jim Kichaa

kwa kumpa ngono ili kumshawishi amwoe kwa masharti yake ili aweze kutimiza ndoto yake ya kufanya harusi kubwa zaidi Tanzania. Hii ni sifa ya wadhanaishi, kutojali mbinu anazotumia almuradi mtu apate matokeo. Kutokuwa na mipaka kati ya jema na baya. Kwa wadhanaishi wasioamini Mungu kama Sartre (keshatajwa) hakuna kigezo cha kupimia wema au ubaya. Eliza pia anasawiriwa bila mipaka hii anapotaka kukidhi mahitaji ya mwili wake;

"Jim mpaka kipindi hiki sioni jinsi ninavyoweza kuendelea kuishi, ndiyo maana nimekuja hapa kukuaga, na hicho ulichopewa ndiyo kwaheri yako nakwenda zangu kujipa sumu, tayari ninayo katika mkoba wangu." (uk.83)

Kwa Jim Kichaa, Eliza ni msichana aliyemtamani zamani, asingeweza kumwacha aende kujiua wakati amepata alichokuwa akikitaka kwa miaka mingi. Mzungu huu ulifaulu kwa Jim Kichaa. Huko ni kuabudu mahitaji ya kimwili.

4.7.3 Garincha asaliti uchumba kwa kuwa na Fay Parker

Huko Uingereza alikoenda kusoma Garincha, katika riwaya ya *Harusi ya Wendawazimu*, alianza uhusiano wa kimapenzi na msichana wa Kiingereza kwa jina Fay. Kama mchumba wake, Eliza, Garincha anashindwa kuvumilia kuwa mbali na mpenziwe na kuanza uhusiano wa kimapenzi na msichana wa Kiingereza;

Fay Parker alikuwa msichana wa Kiingereza aliyekuwa akitembea na Garincha siku zile. (uk. 38)

Huku pia ni kuabudu mahitaji ya kimwili kwa sababu, kuwa katika uhusiano huo na Fay Parker alikuwa anamsaliti mchumba wake, Eliza aliyemwacha Tanzania, japo naye Eliza alikuwa akimsaliti Garincha na rafiki yake Chris. Wote wawili wanasawiriwa wakishindwa kuvumilia kujitunza na kuanza mahusiano mengine.

4.7.4 Chris ashiriki mapenzi na wanawake watatu

Tushatangulia kusema kuwa katika riwaya ya *Harusi ya Wendawazimu* Chris alikuwa amekengeuka kwa kufuata starehe na mahitaji ya mwili wake. Chris haheshimu mahusiano yake yoyote. Alikuwa na Mariam mke wa Musa. Akawa na Eliza na akawa na Zamda kama kimada. Hata baada ya ndoa na Zamda Chris hakukaa kwake akatulia. Kwa kuwa Jim Kichaa alikuwa amefungwa na Eliza akawa hana mume, Chris alihamia kwa Eliza na akapuuza kabisa ndoa yake na Zamda. Aidha akawa bado anaenda kwa Mariam (ambaye sasa alikuwa mtalaka wa Musa) kila Jumapili kukandwakandwa. Isingekuwa kwa matamanio kwa Eliza, Chris asingeisaliti ndoa yake na kwenda kwa Eliza wala kwa Mariam kukandwakandwa;

"… *Siku hizi Chris anakwenda kwa Zamda kubadili nguo labda na kufoka ili asisahaulike kama yeye ndiye mwenye nyumba. Siku zote utamkuta kwa Eliza, Jumapili kwa Mariam akikandwakandwa." (uk. 158)*

Chris anayafanya yote haya kwa ajili ya kustarehesha mwili wake. Hatambui ndoa yake ila anaendeshwa na matamanio aliyonayo. Hata huko kwa Mariam anakokandwa pia hulala na huyo Mariam. Huku ni kuabudu mahitaji ya kimwili.

4.7.5 Mariam (mke wa Musa) anamsaliti mumewe, na dini yake

Katika *Harusi ya Wendawazimu,* Mariam, mke wa Musa ambaye ni mama wa makamo, anasawiriwa akishiriki katika uhusiano wa kimapenzi na Chris nje ya ndoa. Huku ni kuabudu mahitaji ya kimwili. Kwa sababu dini ya Kiislamu iko wazi kuhusu zinaa;

"*Wala msikaribie zinaa. Hakika hiyo (zinaa) ni uchafu (mkubwa) na njia mbaya (kabisa).* (*Kurani 17:32*)

Lakini ili kukidhi mahitaji ya mwili wake, Mariam anaenda kinyume na mafunzo ya dini yake na kushiriki zinaa na Chris. Mwandishi anasema;

Mariam, mke wake (Musa) wa kwanza, alikuwa amebaki mke wa jina tu, na nyumbani kwake Musa alikuwa halali tena. Chris ndiye aliyekuwa mpenzi wake na alimhudumia kimwili. (uk. 25)

Kuwa Chris ndiye aliyekuwa akimshughulikia mahitaji yake ya kimwili kama isemavyo dondoo ni wazi kuwa Mariam aliyafanya hayo ya kuzini kwa sababu ya kupatiliza mahitaji yake ya kimwili. Badala ya kujikita na mafunzo ya dini yake ya kusubiri wakati wa shida kama hivi, au kuitisha talaka ili akaolewe na mume mwengine atakayemtimizia mahitaji ya mwili wake kwa njia halali, Mariam anaamua kufuata matamanio ya mwili wake na kujihusisha na zinaa;

Chris aliangalia uso wa Mariam, akamwangalia matiti, tumbo na miguu ilkuwa imepanuliwa juu yake, mavazi yake yote yalikuwa chini, Chris hangekataa. Mariam alianza kufanya kazi, alipoanza kuhema na kulilia mapenzi mlango uligongwa… (uk. 26)

Wakati wa kitendo hiki, Musa amabye ni mumewe Mariam aliwafumania. Chris alikimbia na Mariam akabaki akipigana na Musa. Katika sherehe ya mkesha wa harusi Mariam alitokea tena akimtaka Chris waendelee na uhusiano wao kwa kuwa ashapata talaka yake. Mbali na kuwa alikuwa na harusi siku iliyofuata, Chris alimkubalia ombi hili;

“Utaendelea kuwa unakuja kwangu kila Jumapili nimeishapata talaka,” alisema Mariam.

“Nitakuja,” alijibu Chris. (uk. 113)

Hata baada ya arusi, Chris aliendelea kwenda kwa Mariam kila Jumapili kukandwa mwili. Kabla ya Mariam kupewa talaka na Chris kuoa, kukandwa huku kuliishia na ngono ambayo ilimridhisa Musa hata mwenyewe akakiri wasingefumaniwa wala asingewahi kufikiria kuoa;

Alimwona Mariam, akajisemea kuwa kama haingekuwa kufumaniwa kwake mwanamke yule labda hangeamua kuoa. (uk. 113)

Chris alimwambia Mariam angeendelea kwenda kwake hata baada ya ndoa yake, na hivyo ndivyo alivyofanya kila Jumapili;

"…*Siku zote utamkuta kwa Eliza, Jumapili kwa Mariam akikandwakandwa." (uk. 158)*

Haya yote Mariam aliyafanya ili kukidhi mahitaji ya mwili wake, hasa ya mapenzi. Kwa kufanya haya, aliyapuuza mafunzo na mahitaji ya dini yake inayokataza zinaa na akafuata mahitaji ya mwili wake. Huku ni kuabudu mahitaji ya kimwili.

4.7.6 Chris na Garincha wanastarehe na wanawake

Katika *Harusi ya Wendawazimu,* baada ya kugundua kuwa Eliza amewacheza shere, Chris na Garincha walikosana karibu kupigana. Walipotuliza hasira waliamua kwenda kujistarehesha ili kujisahaulisha waliyofanyiwa na Eliza. Katika kujistarehesha huku, Chris anapendekeza wakachukue wasichana wa *pastime* ili wasiwazie sana kumhusu Eliza. Huku pia ni kuabudu mahitaji ya kimwili. Wanashindwa kukaa na kufikiria hatma ya yaliyowakuta wanaona njia bora ni kujistarehesha na vimada. Chris anasema;

"*Tutafute warembo wa 'pastime'. Itasaidia kutowazia sana juu ya Eliza. Kama hutajali kuna msichana mmoja Kinondoni. Yeye ni kimada wangu wa siku nyingi, anaishi na mdogo wake, ambaye pia anafaa. Tunaweza kwenda nao, yumkini wakatufariji na kutupa burudani." (uk. 49)*

Garincha aliunga mkono wazo hili, huku ni kuabudu mahitaji ya kimwili kwa wote wawili.

4.7.7 Nora (mama huruma) na ngono za kiholela

4.7.7.1 Nora na Garincha

Katika *Harusi ya Wendawazimu,* kwenye mkesha wa harusi, Nora alimtaka Garincha wafanye mapenzi wakati Garincha akijiandaa kufanya harusi siku iliyofuata. Garincha naye hakupinga wazo hili na wakaishia kufanya mapenzi katika chumba cha Nora. Nora alisema;

"*Lazima leo nikuazime kwa mara ya kwanza na ya mwisho… ikifika saa saba na nusu uingie chumbani kwangu nitakukuta. Chumba changu ni cha tatu toka msala upande wa kulia. Ukiingia ufunge na ufunguo uko katika mfuko wa koti lako. Mimi nitagonga mara tatu ndipo ufungue." (uk. 113)*

Ilipofika saa saba Nora anamkumbusha Garincha kuhusu miadi yao wakati wakisakata ngoma pamoja;

"*Ni wakati wa kwenda chumbani mwangu, uende nitakukuta usinitie ashiki halafu ukaniwacha vivi hivi." (uk. 119)*

Nora alikuwa ashapandisha ashiki na alimhitaji Garincha aizime hamu yake ile. Huku ni kuabudu mahitaji ya kimwili. Hajali kulala na mwanamume aliyebakisha siku moja tu kufunga ndoa. Na baadaye walikutana wakajamiiana.

Garincha alikuwa katika chumba cha Nora, na Nora mwenyewe alikuwa ndani amemkaa juu.

Naye Zamda alitangatanga nyumba nzima mpaka alipofika chumba cha Nora ambapo alihisi kama alisikia mtu akililia mapenzi. Alisogea karibu zaidi na kuweka sikio lake kwenye mlango. Sasa aliwasikia vizuri, wakihema na kulilia mapenzi. Alibaki kwenye mlango kama mbwa abakivyo kwenye kaburi alimozikwa bwana wake. Mwisho vitendo vyao ndani vilianza kuathiri mwili wake, akawashwawashwa na mwisho kuchemka kama vile naye alikuwa akishiriki mapenzi na mwanamume asiyeonekana.

Hata mpaka walipomaliza kitendo kile ndani naye akajisikia kama michirizi ya barafu ilikuwa ikipita mwili mwake, mwisho alitulia na akili kumrudia. Aliporudiwa na akili alitafuta chupa tupu akasimama nayo mlangoni akisubiri kugonga yeyote atakayetoka mle ndani. Baada ya muda mrefu wa kusubiri, mlango ulifunguliwa na Garincha alitoka. Zamda alinyanyua chupa kugonga lakini alipoona kuwa mtu mwenyewe alikuwa Garincha aliachia chupa ikadondoka na yeye aliondoka pale haraka. (uk. 123)

Nora alichojali ilikuwa kuzima moto wa mapenzi aliokuwa nao. Nora hamu yake kubwa ilikuwa kwa Garincha. Siku ya harusi alijaribu tena kumwomba kutoka mikononi mwa Yasmin na akakoswa chupa ya bia kwa sababu hiyo. Hata hivyo Nora hakuishia hapo. Japo uchu wake ulikuwa wa Garincha, baadaye alimchukua Buda ambaye alikuwa mzee na mwalimu wake wa shule ya msingi. Yote haya ili kuzima hamu yake ya mapenzi.

4.7.7.2 Nora na Buda

Nora anasawiriwa kama mwanamke ambaye hawezi kuvumilia ashiki zake na yuko tayari kulala na mtu yeyote. Asubuhi iliyofuata baada ya harusi, Buda alijipata chumbani mwa Nora na wala Nora hakuonyesha kama yaliyotendeka kati yake na mwalimu wake wa shule ya msingi yalitendeka kwa sababu ya ulevi. Alionyesha kuridhika kuwa walilala pamoja, hata pale mwalimu Buda alipoonyesha kuwa na wasiwasi na kukerwa na mambo hayo. Hii inaonyesha kuwa Nora ni mwanamke anayeabudu mahitaji yake ya kimwili na hajali kulala na mwanamume yeyote ili kukata kiu yake ya mapenzi;

Buda alitingisha kichwa. Msichana aliamka bado akiwa uchi alimletea vidonge vya 'asprin' na gilasi ya maji. Alitafuna vidonge na kunywa maji…

Msichana alimsogelea karibu akaweka mikono yake shingoni mwa Buda huku akiruhusu pua zao zigusane. Hiki ndicho kitu Buda hakutaka. Msichana alinuka bia. Makalio na matiti yake yalikuwa makubwa mno na hayakuvutia sasa. Aliuliza swali lao la kawaida;

“Tutaonana lini tena?”

“Nitakupigia simu kesho. Nipe namba yako ya simu.”

Aliiandika kwenye ganda la kiberiti, lakini hakuandika jina lake.

“Na jina lako linaandikwaje?”

“Unanikumbuka, ulinifundisha magomeni nikiitwa Kijakazi lakini siku hizi naitwa Nora,” Yule msichana alisema.

“Lazima niende sasa.”

“Sawa,” Nora alisema huku akitabasamu. Ilibidi ampe busu ya alamsiki. Alitaka kumbusu kwenye shavu lakini msichana aligeuka haraka na kumpa midomo. Harufu yake haikuwa nzuri na rangi aliyopaka midomo ilikuwa imekaukana mdomo ulikuwa kama mpira. (uk.152)

Maelezo haya yanamsawiri Nora akifurahia makutano yao na angependa waonane kwa kitendo kama hicho tena ingawa Buda alipoonyesha kukirihishwa na matendo yake Nora. Kwanza hakujali kuwa yuko uchi mbele ya Buda na kisha akawa anajipeleka akitaka mabusu kwa midomo ya Buda. Matendo haya yote yanaashiria kuwa kwa Nora kulala na Buda na kuamka naye siku ile hakukuwa ajali tu bali ni kitu alichokitaka na angependa kiendelee kutokea. Mahusiano yao haya yaliendelea. Ijapokuwa hayakuwa kati ya Nora na Buda pekee. Buda anasema;

“*…Hata sisi tunaotembea naye tunafanya hivyo kwa niaba ya Garincha. Akiwa anatembea na mwanamume siku hizi lazima afunge macho na kujiaminisha kuwa amelala na Garincha la sivyo hakuna lolote litakalotokea. Hata mchezo ukifika kilele chake utaskia anamwita, ‘Ohoo asante Garincha.” Imekuwa hivyo kwa mara zote hizo tumetembea.” (uk. 155)*

Kulingana na kauli hii ya Buda, Nora hakuwa na mwanamume mmoja pekee, na raha yake ilikuwa ni kupata starehe ya mwili wake.

4.7.8 Mama John (mke wa Buda) anavunja ndoa yake kwa uasherati

Katika *Harusi ya Wendawazimu,* Buda alishindwa kukodi nyumba yenye nafasi kubwa ya kuwatosha yeye na wanawe hivyo wakaishia kukaa chumba kimoja. Watoto walipokuwa na kuanza kutambua mambo ilikuwa muhali kwa Buda na mkewe kujamiiana tena kwa sababu wana walikuwa macho na wangewasikia. Kwa sababu hii mkewe Buda alianza kutoka nje ya ndoa kutembea na mwanamume mwengine ili kukidhi mahitaji yake ya kimwili aliyoyakosa kwenye ndoa yake. Kutofanya ngono ilikuwa shida kwa wote wawili. Buda hakufanya tendo la ndoa na mkewe aidha, ila kwa kuabudu mahitaji ya kimwili mkewe Buda aliamua kutembea na mwanamume mwengine na akaanza kumdharau mumewe. Tamaa za kukidhi mahitaji ya mwili zilifanya ndoa yake ikavunjika. Kama isingekuwa kuabudu mahitaji ya mwili wake angevumilia kama mumewe ili kuishikilia ndoa yao wakalea wana wao hadi pale ambapo maisha yangekuwa mazuri. Au pengine wangetafuta mbinu mbadala pamoja kukidhi mahitaji yao. Mke wa Buda kuamua kuitoa ndoa yake kafara ili kukata kiu yake ya mapenzi ni thibitisho tosha ya kuabudu mahitaji ya kimwili. Buda mwenyewe anaeleza;

“Kushindwa kupata nyumba ya vyumba viwili kuliniharibia mambo. Tulipokosa kufanya mapenzi mke wangu akawa mwendawazimu. Haikuchukua muda nikagundua kuwa alikuwa anatembea na mwanamume mwingine. Mambo yakaanza. Ikawa mimi sifai. Chumba chetu kidogo kikageuka kama jukwaa la ndondi.

Angebubujikwa na matusi, angeniita hanithi na matusi mengi. Na mimi, kwa hasira, ningemvamia na kumpiga kama vile nagombana na mwanamume mwingine. Mwisho niliona kuwa ningeua. Ilibidi aende.” (uk. 138)

Kwa kuwa mama john aliamua kutoa ndoa yake kafara na kushiriki matendo ya kukidhi haja zake za kimwili, huko ni kuabudu mahitaji ya kimwili.

4.7.9 Eva auza mwili kujikimu

Eva ni kimada wa Kachala mmoja mteja wa pale mkahawani DDC. Pia ni mwajiriwa hapo. Eva anakiri sababu ya kutembea na kachala yule ni kuwa ndiye anayemkidhi mahitaji yake yote, kwa sababu mshahara wake wa pale DDC haumtoshi. Eva amekubali kuwa kimada ili apate mahitaji yake na anadhihaki kuwa ndoa yao ilifungwa na 'sudi', kumaanisha kuwa hawajaoana ila ameridhika na hali ilivyo almuradi anapata mahitaji yake;

"Kachala ndiye mwajiri wangu, hapa DDC najishikiza tu, kachala ndiye kitegauchumi changu, ndiye njia pekee ya kupata ugali, kulipa kodi ya nyumba, kuvaa hata kuwatunza watoto wangu. Yeye ndiye mume ndoa yetu ilifungwa na sudi." (uk. 161) Ugumu wa maisha umemfanya Eva kujitia hamnazo na kukubali kuishi kama kimada bora anatimiziwa mahitaji yake na wanawe. Ni kuabudu mahitaji ya kimwili.

4.7.10 Kachala msimulizi wa kisa ananunua ngono

Kachala huyu aliifanya kuwa tabia yake kulipa hawara wa pale DDC ili awe naye kimapenzi. Huku pia ni kuabudu mahitaji ya mwili. Kama sivyo angesubiri kupata mke au hata mchumba kuliko kulipa hawara ili amtimizie mahitaji ya kimwili;

Na mimi nilifanya hima nikamwita msichana aliyekuwa meza jirani. Alipofika nilimbusu kwenye mkono, nikachomoa noti ya shilingi elfu moja toka mfukoni nikampa. Aliikunja na kuiweka ndani ya sidiria huku akiuliza,

"Kwangu au kwako? Kama ni kwangu basi ongeza elfu nyingine."

Nilimpa. Nikamgeukia Buda nikasema,

"Muda unakwenda, inabidi kujihami." (uk. 159)

Baadaye alimtafuta yule msichana akapewe alicholipia;

Mimi nilichukua chupa yangu ya bia nikaondoka pale na kuanza kumtafuta bibi yule niliyempa shilingi elfu mbili. (uk. 161)

Huku ni kuabudu mahitaji ya kimwili. Mtu kutumia njia yoyote awezayo ili kuhakikisha anakidhi mahitaji ya mwili wake hata kama njia hiyo inamweka kwenye hatari ya kuambukizwa magonjwa ya kuambukiza kama ya zinaa. Ama njia itakayoshusha hadhi yake katika jamii, huko ni kuabudu mahitaji ya kimwili.

4.8 Utupu wa maisha/ ombwe/ ubatili

Mwanadamu si chochote. Kulingana na wadhanaishi, hakuna hata falsafa moja inayoweza kueleza mwanadamu ni kitu gani. Na zaidi, kifo kinapokuja humfuta mwanadamu akawa hayupo tena, kukabaki utupu. Kabla ya kuzaliwa mwanadamu huwa kuna utupu na baada ya mauko yake huwa kuna utupu. Mwanadamu huwako katikati ya utupu.

Aidha, aina nyengine ya utupu/ubatili inajitokeza pale ambapo mwanadamu anang'ang'ana kuyapa maana maisha yake. Katika juhudi hizi ndipo mwanadamu anapogundua maisha si chochote na hakuna maana yoyote inayoweza kutokana na maisha haya yasiyokuwa na maana. Atafanya juhudi zake zote kuyapa maisha maana ila mwishowe atagundua maisha hayana maana, na kama ipo basi si ya kudumu. Mwanadamu hatabaki katika umbile lake la kawaida kila wakati.

Usawiri wa wahusika wafuatao kutoka riwaya hizi mbili ni wa kuonyesha ombwe/utupu katika maisha ya mwanadamu;

4.8.1 Musa Nshomile anashindwa kuyapa maisha yake maana (anatoweka)

Katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* Mwandishi anatuchorea taswira ya matatizo yanayomkumba Musa katika safari yake tangu punde tu alipotua Tanzania hadi mwisho. Musa ambaye ni msomi wa uzamifu alikuwa na matarajio makubwa ya kupata kazi nzuri na kuheshimiwa kwa ajili ya mafanikio yake katika elimu. Sivyo ilivyokuwa.

Kwanza alidharauliwa kwa elimu yake aliyotarajia impe cheo miongoni mwa Watanzania. Hali hii inaonyesha ubatili wa maisha. Musa alidhani ameyapa maisha yake maana kwa usomi wake, ila jamii ikamkumbusha kuwa yote hayo si chochote ila ubatili. Elimu yake haina maana yoyote. Na maisha yake hayana maana yoyote. Matusi yafuatayo ni dhirihisho la jambo hilo;

"Ulikwenda kote huko, ukakaa miaka yote saba, hakuna chochote ulichokileta isipokuwa vyeti! Miaka yote saba unatuletea ujinga wa karatasi!... Nani anataka ujinga wa vyeti katika nchi hii? Bila dola, bila 'pick-up', rafiki yangu, utateremshwa daraja kama wafanyavyo katika ligi ya kabumbu." (uk. 18)

Musa anasawiriwa akipitia matatizo tangu atue Tanzania. Kila kitu alichojaribu kufanya hakiwezekani. Anashindwa hata kupata gari la kumpeleka hoteli alikokodisha hadi anapopata msaada kwa rafiki yake wa kitambo Mujuni, aliyemsafirisha hadi hotelini kwake. Mbali na elimu yake yote hadi uzamifu, Musa anaporudi Tanzania si chochote. Anadharauliwa na kupitia matatizo mengi hata kuliko wale ambao hawakusoma ila wana magari ya *pick-up.*

Huko mjini Musa anashindwa hata kupata nyumba ya kukaa. Alijaribu kuishi bila mke, hili likawa kikwazo kwake kupata nyumba. Akajaribu kujisingizia kuwa na mke ili apate nyumba ila pia hili likawa kikwazo kwake kupata nyumba. Alipoona maisha yamempokea vibaya mjini akaenda kijijini angalau apate faraja ya kuona familia yake, hili pia lilizidi kumkatisha tamaa. Familia yake haipo, shangazi lake aliyemlea alikufa na binamu yake yuko rumande. Maisha yake yanazidi kukosa maana.

Baadae Musa anashikwa na Malaria kali ambayo nusura imuuwe. Maradhi haya yanamfanya atanabahi kuwa maisha si chochote ila utupu. Na maisha yanaweza kumkatikia mtu wakati wowote. Kwa bahati anahudumiwa na Stella, bintiye Mwalimu Tadeo hadi kupona. Kitendo hiki kinamfanya Musa kutambua kuwa mtu ni utu na

maana ya maisha inapatikana kwenye upendo katika familia. Anajaribu kuitafuta maana hiyo mpya ila bado haipati kwani posa yake kwa Stella haikubaliwi moja kwa moja. Hili nalo linazidi kuyakosesha maisha yake maana.

Anaamua kwenda rumande kuonana na binamu yake, Abdu. Huko Abdu anamsimulia kadhia nyengine ya maisha yake inayozidi kumkatisha Musa tamaa. Haswa pale alipomuuliza Abdu angeweza kumsaidia vipi ila Abdu akamjibu kuwa hawezi kutoa msaada wowote. Hili lilizidi kumtamausha.

Hizi zote zilikuwa juhudi za Musa kujaribu kuyapatia maisha yake maana. Ila hakuna maana yoyote anayopata isipokuwa utupu. Shangazi lake alikufa na mji wao umebaki nyasi tu, binamu yeke amefungwa, shule aliyosomea haina tofauti na magofu, mke anayemtaka hampati. Hakuna kinachoendelea katika maisha yake ila utupu.

Baada ya matatizo yote aliyopitia Musa na yote aliyoyashuhudia, na yale ya kusimuliwa kama ya binamu yake Abdu, Musa hatimaye anasawiriwa akikata tamaa. Alifikiria kurudi tena Uingereza akaendelee na maisha yake na Irene;

Wazo la jana yake, wazo la kuikimbia nchi lilimjia tena. Taswira ya maisha ya Ulaya ilikuwa mbele yake. Aliiona Manchester, alimwona Irene. Mara alifikia uamuzi. Angekwenda kuishi Ulaya. (uk. 127)

Haijulikani kama alisafiri kurudi Ulaya kwa Irene au alijiua, ila alitoweka Tanzania. Juhudi zake zote hazikusaidia kuyabadilisha maisha yake na kuyapa maana aliyokusudia mwenyewe haswa kwa matumaini aliyokuwa nayo baada ya kusoma hadi kupata shahada ya uzamifu. Maisha ya Musa yanasawiriwa yenye utupu na ubatili. Hakuna chochote kinachoendelea cha kuyapa maisha yake maana. Kilele cha utupu huu ni pale Musa anapotoweka, hajulikani alipo na hakuna anayejali;

Kwenye ubao wa matangazo wa Makao Makuu ya Wizara ya Ujenzi alisimama msichana aliyeshikilia picha ya mgombea urais. Alikuwa akitafuta sehemu ya

kuibandika. Ubao ule ulikuwa umejaa matangazo. Mara pale kwenye ubao aliona karatasi iliyoonyesha picha ya Musa na maelezo ya kupotea kwake. Yule msichana aliibandua karatasi ile na kuichana vipandevipande. (uk. 128)

Hata baada ya Musa kupotea watu hawakujali na maisha yaliendelea tu kana kwamba kulikuwa hakuna lolote lililotokea. Hakuna anayejali kupotea kwake. Huku ni kuonyesha kuwa maisha hayana maana yoyote na kuwa matatizo ya mtu ni yake binafsi, wengine hayawahusu.

Elijah Guerra (2019) akichambua dhana ya utupu katika riwaya ya Cormac McCarthy, *Suttree,* anasema, *Arnold explains, "Suttree attempts to excuse his failures by insisting on the insignificance and 'nothingness' of life" (60), as when he is talking with the sheriff after his son's funeral and says "no one cares. It's not important" (Suttree 157).*

Arnold anaeleza kuwa, "Suttree anajaribu kusingizia kukosa maana na utupu wa maisha anapofeli katika majukumu yake" (60), kwa sababu anapozungumza na askari baada ya mazishi ya mwanawe anamwambia hakuna anayejali. Si muhimu" (Suttree 157). (T.Y)

Ni kama vile anavyofanyiwa Musa, ameng'ang'ana kuishi maisha yake vizuri ila amefeli. Anapotoweka hakuna anayejali, kwa sababu si muhimu. Huku ni kuonyesha utupu wa maisha. Musa ametoweka, na kilichobaki kumhusu ni utupu.

4.8.2 Isaya Omulangi anahubiri uduni wa binadamu

Isaya Omulangi ni mhusika katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* Baada ya mazishi ya Katoto wa Minane ni yeye aliyeamua kusomea umati mahubiri kutoka katika Bibilia ili wakayatafakari. Kifo hutumiwa sana na waumini kumwonya mwanadamu dhidi ya kujigamba na kujitapa kwa sababu maisha si chochote na mwisho wake ni kifo, kutumbukizwa kaburini (kwa wasiochomwa) ukarudi kwenye mchanga ulioukanyaga

kwa majigambo. Katika mazishi ya Katoto, Isaya Omulangi alipata fusra nzuri ya kuwakumbusha watu kuwa mwanadamu si chochote, hana tofauti na mnyama na kwa ajili hii maisha yake si chochote ila utupu:

"Basi kama hakuna ubaya," Bwana Isaya alisema. "Naomba tuanze kusoma neno la Mungu katika kitabu cha Mwanzo 3:17-19"

Alianza kusoma:

"Akamwambia Adamu, kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nilikuagiza, nikisema usiyale; ardhi imelaaniwa kwa ajili yako: kwa ungungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako; michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni; kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi." (uk. 117)

Alipomaliza kusoma akasema, "Hilo ni neno la Mungu toka Kitabu cha Mwanzo. Sasa tusome katika Kitabu cha mhubiri 3:19-22." ...Alisoma:

"Kwa maana linalowatukia wanadamu linawatukia wanyama; jambo moja lawatukia; anavyokufa huyu ndivyo anavyokufa huyu; naam, wote wanayo pumzi moja; wala mwanadamu hana kitu cha kumpita mnyama; kwa maana yote ni ubatili. Wote huenda mahali pamoja; wote hutoka katika mavumbi; na hata mavumbini kurudi tena. Ni nani ajuaye kama roho ya binadamu huenda juu na kama roho ya mnyama huenda chini?"

Alipofika hapo hapo akafunga kitabu chake na kukiweka kwapani, kisha akasema, "Ndugu zangu twendeni nyumbani tukitafakari hili neno; vumbini tulitoka, vumbini tutarudi tena; Ni nani ajuaye kama roho ya binadamu huenda juu, na kama roho ya mnyama huenda chini? Twende tunalitafakari." (uk. 118)

Katika nukuu zote hizi, uduni wa mwanadamu umesisitizwa. Mwanadamu si chochote ila mavumbi na mwisho wake ni kurudi mavumbini. Halafu mwanadamu anazidi kudunishwa kwa kuwekwa daraja moja na mnyama. Kujienua kote mwanadamu anaambiwa hana tofauti na mnyama. Hili ni kuonyesha kukosa maana kwa maisha ya mwanadamu na ubatili wa maisha yake. Kwa sababu mnyama kazi yake ni kula, kulala na kuzaa. Mwanadamu naye anaonyeshwa utupu wa maisha yake kwa kuambiwa kuwa yote anayojaribu kuyafanya katika maisha yake ni batili, na hayamtofautishi yeye na mnyama. Isaya naye anasisitiza haya kuwaambia wanakijiji waende wakatafakari kuwa mwanadamu anatokana na mchanga na atarudi mchangani, na kuwa si tofauti na mnyama. Haya ni mawazo ya wadhanaishi kuonyesha utupu wa maisha kwa kuyaondolea maana.

Kezilahabi (1974) naye anashadidia mawazo haya pale mhusika Kazimoto anapojiua kwa kutopata tofauti kati yake na wanyama; *Nimejiua. Siwezi kuendelea kuzaa kizazi kibaya. Pia sikuona tofauti kati yangu na mdudu au mnyama. Akili! Akili! Akili· ni nini? (uk. 217)*

Sayyid Abdalla bin Ali bin Nassir katika *Al-Inkishafi* naye anaonyesha utupu wa maisha kwa kurejelea utawala wa Pate uliosifika kwa utukufu, utajiri na kujitapa sana. Yeye anatumia mfano huu kuiusia nafsi yake kutokuwa na kiburi wala kuringa kwa uhai alio nao kwa sababu mwanadamu si chochote, utukufu wake huisha na kukabaki utupu wa milele. Anarejelea wazazi wake waliokufa pia kusisitiza dhana hii ya utupu. Anarejelea kuzeeka kwake pia. Anarejelea watawala, wafalme na mitume waliosifika kwa utukufu wao ila sasa hakuna chochote kilichobaki kuwahusu ila utupu usiokoma;

Au enga vumbi la muangaza,

Wakati wa yua likitepuza;

Mwenda kulegema akilisoza

Asione kitu ukishishiye. (ubeti wa 15)

Au enga meto limetukapo

Wakati wa yua lilinganapo;

Mwenye nyota hwamba, "Ni mai yapo!

Kayakimbilia akayatwaye. (ubeti wa 16)

Suu ulimwengu uutakao,

Emale ni lipi upendeyao?

Hauna dawamu hudumu nao,

Umilikishwapo wautendaye? (ubeti wa 31)

Hakuwa mtumi Suleimani,

Maliki wa insi na ajinani;

Ulimfutuye ukamukhini,

Akiwa mwengine, wamtendaye? (ubeti wa 32)

Beti hizi ni mifano mizuri ya kuonyesha utupu wa maisha. Kwanza ulimwengu unalinganishwa na mazigazi, unalaghai tu lakini hakuna chochote. Mwanadamu katika mbio zake zote anazokimbia ulimwenguni zinaishia kwenye utupu. Kwa sababu ulimwengu wenyewe ni utupu. Hata wale waliosifika kwa utukufu wao kama mtume Suleimani, ulimwengu "ulimfuta" ukabaki utupu. Hivyo, Isaya anaposema watu watafakari kuhusu maisha na mwisho wao usio tofauti na wa mnyama, anarejelea utupu wa maisha.

4.9. Kihitimisho

Katika sura hii, sehemu zote mbili za malengo ya utafiti zilishughulikiwa. Kwanza vilitambuliwa vipengele vyote vya udhanaishi vinavyojitokeza katika riwaya hizi mbili zilizokuwa zikitafitiwa: *Kitu Kidogo Tu!* na *Harusi ya Wendawazimu.* Vipengele hivi ambavyo ni uhuru, swala la Mungu, ukengeushi, utamaushi, kuabudu mahitaji ya kimwili, kifo na utupu vilidadavuliwa kwa kina. Hili lilitimiza sehemu ya kwanza ya malengo ya utafiti.

Baada ya vipengele hivi vya udhanaishi kutambuliwa na kufafanuliwa, matendo na maneno ya wahusika mbalimbali yaliyoonyesha sifa za vipengele hivyo yalichanganuliwa chini ya kila kipengele mtawalia. Kwa kufanya hivi, sehemu ya pili ya malengo ya utafiti huu ilitimizwa.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1. Kitangulizi

Hii ndiyo sura ya tano na ya mwisho ya utafiti huu. Katika sura hii, muhtasari wa utafiti huu umetolewa. Aidha, utafiti huu unahitimishwa na mapendekezo yanatolewa kwa tafiti za baadae zitakazojihusisha na riwaya hizi mbili za *Kitu Kidogo Tu!* na *Harusi ya Wendawazimu.*

5.2. Muhtasari

Utafiti huu ulinuia kuchunguza maneno na matendo ya wahusika katika riwaya mbili za Thomas Kamugisha- *Kitu Kidogo Tu!* na *Harusi ya Wendawazimu* kwa misingi ya nadharia ya udhanaishi. Utafiti uliongozwa na malengo mawili ambayo ni: Kubainisha vipengele vya udhanaishi vinavyojitokeza katika riwaya hizi mbili na kueleza jinsi vipengele hivyo vinavyojitokeza katika matendo na maneno ya wahusika. Vipengele vya udhanaishi vilivyobainika katika riwaya hizi ni:

Uhuru wa mtu binafsi

Hiki ni kipengele cha udhanaishi kinachoweka mbele uhuru wa mtu wa kujiamulia mambo yake bila kufungwa na kaida za dini au jamii. Aghalabu mtu hupitia migogoro ya kinafsi na ya kijamii anapojitafutia uhuru huu. Katika riwaya hizi mbili tulipata wahusika kama Zamda ambaye alikosana na babake aliyejaribu kumzuia kuolewa na kijana aliyempenda kwa kutumia kigezo cha tofauti ya dini. Zamda alisawiriwa kama mhusika aliyeridhia kukosana na familia ili kujitafutia uhuru wake. Ni sifa kuu ya udhanaishi.

Swala la Mungu

Hiki pia ni kipengele cha kidhanaishi kinachojadili uwepo au kutokuwepo kwa Mungu mwenye nguvu zote na muumba wa vyote. Wadhanaishi kama Nietzsche na Sartre wanashikilia kuwa hakuna Mungu na kuwa mwanadamu yuko huru kujiamulia na kufanya anavyotaka bila kujali kuulizwa chochote na Mungu siku ya kiama. Kunao wadhanaishi kama Kierkegaard wanaoshikilia kuwa mwanadamu ni kikaragosi cha nguvu zilizomuumba kwa hivyo anafaa kuishi kwa kuridhisha nguvu hizi ili apate utulivu wa kiroho, kwa kujua kuwa maisha yake yana maana ijapokuwa haijui yeye mwenyewe. Katika riwaya hizi kuna wahusika kama Musa Nshomile ambao wanaonyesha kupata imani ya Mungu ili kuyapatia tena maana maisha yao mambo yalipokuwa magumu. Musa, mbali na kisomo chake cha uzamifu, anateseka hadi kupoteza matumaini maishani. Hata hivyo, anarudi katika imani ya dini akitarajia Mungu atamwongoza na kuyapa maisha yake maana tena. Aidha kuna wahusika kama Mzee anayezungumza na Musa Nshomile katika gari la kwenda Bukoba. Mzee anaonyesha kukejeli uwepo wa Mungu na uwezo wake juu ya maisha ya mwanadamu ambayo yalionekana kutokuwa na maana kwa ugumu wake.

Kifo

Kulingana na wadhanaishi, juhudi za mwanadamu za kujitafutia maana katika maisha huishia katika mvunjiko wa juhudi hizo, yaani kwa kufa. Kifo ndicho kikwazo cha uhuru unaotafutwa mwanadamu. Udhanaishi unashughulikia maswala kama fadhaa, uchovu, pekecho, maradhi na majanga ya kiasili kama radi na mitetemeko ya ardhi, ambayo humwangamiza mwanadamu na hana uwezo juu yavyo. Haya yanapotokea huweza kusababisha kifo cha mwanadamu na kuvunja juhudi zake zote za kujitafutia maana ya maisha yake. Katika riwaya hizi kuna majanga yanayosababisha vifo vya halaiki. Katika *Kitu Kidogo Tu!* wazazi na ndugu wa Musa Nshomile wanaangamia kwa

mkurupuko wa maradhi ya malale ilhali katika *Harusi ya Wendawazimu* familia ya Garincha inaangamia kwa mkurupuko wa maradhi ya kipindupindu. Juhudi za Zainab, shangazi lake Garincha kumlea na kuhakikisha amepata elimu baada ya wazazi wake kuangamia nazo zinaangamia kwa kifo cha Zainab anayekufa Garincha akiwa darasa la saba. Ilibidi serikali imsomeshe Garincha hadi amalize shule.

Ukengeushi

Mwanadamu anapotafuta uhuru wake hujipata amekengeushwa na jamii, dini, Mungu na pia hata nafsi yake. Ukengeushi huu ndio usababishao mgogoro na familia na nafsi pia. Wahusika kama Zamda anapitia migogoro hii na babake alipojaribu kutafuta uhuru wake wa kujiamulia kuolewa na Mkristo ilhali yeye ni Mwislamu, kinyume na mafunzo ya dini na tamaduni za jamii. Kuna wahusika wengine kama Saad Mwendawazimu anayekengeuka na maadili ya dini yake ya Kiislamu yanayokataza unywaji wa pombe. Yeye anasawiriwa akibugia chupa za *johny walker* mbali na kuwa hapo mwanzoni alikuwa na msimamo thabiti katika mafunzo ya dini. Kuna wahusika kama Musa Nshomile anayekengeushwa na tabia yake na kuanza kutoa hongo na kudanganya ili kuingiliana na maisha ya Tanzania aliyoikuta. Hizi zote ni sifa za ukengeushi.

Utamaushi

Hiki ni kipengele cha kidhanaishi kinachoonyesha mwanadamu kukata tamaa pale ambapo juhudi zake za kujitafutia maana ya maisha yake zinaposhindwa kumpa maana anayoitafuta. Udhanaishi unamtaka mwanadamu kutambua mipaka yake ya kimaumbile, bila hivyo ataishia kukata tamaa kwa juhudi zake kutozaa matunda. Anapofikia kukata tamaa, mwanadamu anaweza kufanya uamuzi pekee alio na uwezo nao katika maisha yake, kujitoa uhai. Katika riwaya zote hizi mbili kuna wahusika wanaojitoa uhai kwa kukata tamaa baada ya maisha yao kukosa maana kwa mateso ya muda mrefu. Kwa mfano, katika *Kitu Kidogo Tu!* Katoto wa Minane anakimbia vita vya wenyewe huko

kwao Burundi vinavyoangamiza familia yake. Maisha yake hayaonekani kuendelea anapofika Tanzania na hatimaye anajitia kitanzi. Kutokana na kifo chake, wahusika wengine wanashikwa na kufungwa bila kufunguliwa mashtaka. Mahabusu wengine wanaishia kujitia kitanzi kwa kukata tamaa. Abdu, binamu yake Musa Nshomile naye hatimaye anakata tamaa na anamweleza binamu yake kuwa yuko tayari kukubali mashtaka ya mauaji japo hakuyafanya. Yuko tayari kutumikia kifungo au adhabu yoyote hata kama ni ya kifo. Wamekata tamaa wote. Hii ni sifa ya udhanaishi.

Kuabudu mahitaji ya kimwili

Kuabudu mahitaji ya kimwili ni kuishi bila mipaka yoyote inayofungamana na kuulinda mwili kutokana na matendo kama ngono za kiholela. Mtu anapoweka mbele anasa na kutojali kuhusu majukumu yake mengine ya kujilinda, kulinda heshima yake au familia yake basi anaabudu mahitaji ya mwili wake. Kwa wadhanaishi wasioamini Mungu hili ni sawa ila kwa wanaoamini Mungu kama Kierkegaard hili si sawa. Kuna wahusika kama Eliza katika *Harusi ya Wendawazimu* anayejikuta na wachumba wawili katika juhudi zake za kustarehe na kukidhi mahitaji ya mwili wake. Yeye mwenyewe anakiri na kusema kuwa mwili wake ni dhaifu asingeweza kumsubiria mpenziwe, Garincha aliyekwenda Uingereza kusoma. Kuna wahusika wengine kama Mama John- mke wa Buda anayeivunja ndoa yake kwa kukosa kufanya ngono kwa muda mrefu na mumewe. Nyumba yao ya chumba kimoja na watoto mumo isingewaruhusu kukidhi mahitaji hayo ya kimwili. Huku ni kuabudu mahitaji ya kimwili na ni sifa ya kidhanaishi.

Utupu wa maisha/ ombwe/ ubatili

Mwanadamu si chochote, kabla yake hakukuwa na chochote na baada ya kifo chake hakutakuwa na chochote kinachomshughulisha moja kwa moja. Hakuna nadharia inayoeleza mwanadamu ni nini na matendo yake yote si chochote ila ubatili. Mwanadamu amezungukwa na utupu, na hata anapokufa maisha yataedelea kana

kwamba hakuna kilichotokea. Katika *Kitu Kidogo Tu!* mhusika Musa Nshomile anatoweka na hakuna anayejali. Pale picha yake ilipobandikwa kutangaza kupotea kwake, msichana mmoja anaibandua, anaitupa kisha anabandika picha ya mgombea urais. Musa si chochote tena, hakuna anayejali kutoweka kwake. Kilichosalia kumhusu ni utupu usiokoma.

Hivi vyote tulivyoeleza ni vipengele vya kidhanaishi vinavyojitokeza katika matendo na maneno ya wahusika wa riwaya hizi mbili. Malengo ya utafiti yalitimia.

5.3. Hitimisho

Utafiti huu umemwezesha mtafiti kuhitimisha kuwa Thomas Kamugisha ni mwandishi wa kidhanaishi kwa sababu katika maandishi yake vipengele vya kidhanaishi vimejitokeza waziwazi. Tofauti na wadhanaishi kama Kezilahabi ambaye maandishi yake mengine kama *Nagona* na *Mzingile* ni riwaya za kifaslsafa na zinazungumzia moja kwa moja maswala ya kidhanaishi na mijadala yake kama vile maana ya maisha, uwepo wa Mungu n.k. Kamugisha yeye ameyasawiri maisha namna yalivyo. Katika riwaya hizi zake, Kamugisha amezungumzia maisha ya kawaida kama yalivyokuwa katika nchi ya Tanzania maika michache baada ya kupata uhuru. Hata hivyo, amezungumzia maswala muhimu ya kidhanaishi kwa njia ambayo si moja kwa moja ya kifalsafa.

Kwanza, katika riwaya zote mbili kulikuwa na maafa ya halaiki kutokana na magonjwa ya kuambukiza, malale na kipindupindu, yaliyoangamiza watu kwa halaiki. Hii ni sifa moja ya kidhanaishi. Akaonyesha kuwa maisha hayana maana. Mwanadamu hana uwezo wa matukio mengine katika maisha na hawezi kuzuia kifo chake anapokumbwa na majanga. Aidha, Kamugisha amesawiri wahusika wakikengeuka kama Buda na Saad Mwendawazimu. Akasawiri wahusika kama Zamda wanaotafuta uhuru na hawajali mtu yeyote wakiwemo wazazi wanaojaribu kumpimia uhuru wa maamuzi yake. Aidha, amesawiri wahusika wanaoamua kukana uwepo wa Mungu kwa matatizo

yanayowakumba na wale ambao bado wameishikilia imani ya Mungu na tumaini kuwa Mungu atawaondolea matatizo yao. Amesawiri wahusika kama Katoto wa Minane na mahabusu wanaokata tamaa na kuamua kujiua. Hili ni swala la msingi la udhanaishi.

Katika riwaya hizi mbili, mwandishi amesawiri jamii na matatizo wanayopitia kama binadamu. Hakujaribu kuonyesha tumaini wala mwelekeo wowote ila ametusawiria tu jinsi maisha yalivyokuwa kwa Watanzania miaka michache baada ya uhuru. Kutokana na utafiti huu, tunaweza kusema riwaya hizi mbili za Kamugisha ni za kidhanaishi kwa sababu udhanaishi ni nadharia inayoshughulikia maswala kuhusu maisha. Kamugisha naye ni mwandishi anayejihusisha zaidi na maswala yanayohusu maisha na matatizo yake.

5.4. Mapendekezo

Utafiti huu umeshughulikia maswala ya kidhanaishi pekee katika riwaya hizi mbili za Kamugisha. Katika maelezo ya jalada ya nyuma ya riwaya ya *Kitu Kidogo Tu!* mhariri anasema, *Thomas Kamugisha ni mwandishi mwenye ujasiri na ukwasi katika kuvisuka visa vya fasihi. Matumizi ya kebehi na kejeli ni baadhi ya mbinu alizojaaliwa*. Mtafiti mwengine anaweza kutafiti kuhusu mbinu za lugha na mbinu za uandishi na jinsi mwandishi alivyozitumia kuwasilishia kazi zake.

Aidha, utafiti mwengine unaweza kufanywa kuhusu jinsi elimu ya magharibi ilivyochangia katika ukengeushi wa maadili na kusababisha tabia za kiasherati kama ilivyokuwa katika *Harusi ya Wendawazimu.* Anaweza kuangalia pia jinsi elimu hiyo ilivyoathiri vijana wakataka kutafuta uhuru wao wa kufanya mambo yao bila kuingiliwa na wazee.

Aidha, kwa kuwa riwaya hizi hazijatafitiwa sana, utafiti mwengine unaweza kufanywa ukiongozwa na nadharia nyengine kama nadharia ya uhalisia au nadharia ya Ubuntu

kuchanganulia namna maisha yalivyokuwa katika Tanzania inayozungumziwa katika riwaya hizi mbili. Kamugisha ni msomi wa sosholojia, bila shaka uandishi wake umeathiriwa na elimu hii ya sosholojia aliyoipata. Mtafiti mwengine anaweza kutafiti akiegemea nadharia ya sosholojia.

Kwa kuwa utafiti huu umegundua kuwa hizi riwaya mbili za Kamugisha ni za kidhanaishi, mtafiti mwengine anaweza kulinganisha udhanaishi wa Kamugisha na wa Euphrase Kezilahabi ambaye anatambulika kwa udhanaishi wake katika fasihi ya Kiswahili. Kazi za Kezilahabi kama *Nagona* na *Mzingile* ni za kifalsafa na mara kwa majadiliano ya kidhanaishi hupatikana, tofauti na riwaya za Kamugisha. Utafiti linganishi au linganuzi wa kazi za hawa waandishi wawili pia unaweza kufanywa.

Hatimaye Kamugisha ana riwaya ya tatu ambayo hatukuishughulikia. Mtafiti mwengine anaweza kuishughulikia na riwaya hii ili tuzidi kuuelewa zaidi mchango wa Kamugisha katika fasihi ya Kiswahili.

MAREJELEO

Abbagnano, N. (2020, October 20). Existentialism. *Encyclopedia Britannica.* https://www.britannica.com/topic/existentialism. Accessed on 8th of June 2020.

Akinpelu, J.A. (1981). *An Introduction to Philosophy of Education.* London: Macmillan Publishers Ltd.

Al-Farsy, A. S (1969). *Qurani Takatifu.* Nairobi. Islamic Foundation.

Bakewell, S. (2016, March 4). Think big, be free, have sex … 10 reasons to be an existentialist. *The Guardian.* https://www.theguardian.com/books/2016/mar/04/ten-reasons-to-be-an-existentialist. Accessed on 8th of June 2020.

Bennett, M. (2011). *Reassessing the Theatre of the Absurd*. New York: Palgrave Macmillan.

Brown, C. (1969). *Philosophy and The Christian Faith*. London. Intervarsity Press.

Camus, A. & Gilbert, S. (1954). *The stranger*. New York: Vintage Books.

Charlesworth, M. (1975). *The Existentialists and Jean-Paul Sarte.* London: George Prior Publishers.

Chiduo, E.F.K., Habwe, J., Chimerah, R., Kaoneka, M., Yahaya, R. na Attas, A. (2016). *Kamusi Elezi ya Kiswahili.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1978). *Historia ya Kiswahili.* Nairobi. Oxford University Press.

Doody, M. A. (1996). *The True Story of the Novel*. New Brunswick. NJ: Rutgers University Press.

Elbe, I., & Blumenfeld, J. (2020). The Anguish of Freedom: Is Sartre's Existentialism an Appropriate Foundation for a Theory of Antisemitism? *Antisemitism Studies, 4*(1), 48-81. doi:10.2979/antistud.4.1.03

Esslin, M. (1974). *The Theatre of the Absurd.* London: Methuen.

Guerra, E. (2019). Nothingness is not a curse: Suttree's Absurd Revolt. *The Cormac McCarthy Journal, 17*(2), 148-170. Retrieved February 8, 2021, from https://www.jstor.org/stable/10.5325/cormmccaj.17.2.0148

Hitchens, W. (1972). *Al-Inkisafi: The Soul's Awakening.* Nairobi. Oxford University Press.

Hough, G. (2018). *An essay on Criticism*. London: Gerald Duckworth and Co ltd.

Iqbal, A.S. (2015 February 12). *Shaytan is the third between a Man and Woman meeting in secret.* The Milli Gazette. http://www.milligazette.com/news/11703-shaytan-is-the-third-between-a-man-and-woman-meeting-in-secret. Accessed on 8th, June 2020.

Kamugisha, T. (1980). *Harusi ya Wendawazimu.* Dar es Salam. MBP Enterprises.

Kamugisha, T. (2000). *Kitu Kidogo Tu!* Dar es Salaam. MBP Enterprises.

Kamugisha, T. (2004). *Safari ya Mwalimu Katoto.* Dar es Salam. Heko Publishers.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichwamaji.* Dar es Salaam: East African Pub. House.

Kezilahabi, E. (1988). *Rosa Mistika.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (1983). Utunzi wa Riwaya na Hadithi Fupi. Katika *Fasihi: Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III.* Dar es Salaam: TUKI.

Kezilihabi, E. (1990). *Nagona.* Dar es Salaam. Dar es salaam University Press.

Kezilahabi, E. (1991). *Mzingile.* Dar es Salaam. Dar es salaam University Press.

Khamis, S. (1983). Hatua Mbalimbali za Kubuni na Kutunga Riwaya. Katika *Fasihi: Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III*. Dar es Salaam: TUKI.

Khamis, M.A.S. (2008). Nadharia, Ubunifu, Uchambuzi na Taaluma ya Kiswahili. Katika *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na lugha za Kiafrika*. Nairobi; Moi University Press. Uk. 3-23

Kierkegaard, S. (1983). *Fear and Trembling*. (Tr. Howard V. hong and Edna H. Hong.) Princeton: Princeton University Press.

Kombo, K. na Tromp, A. (2006). *Proposal and Thesis Writing. An Introduction.* Nairobi: Pauline Publishers.

Kothari, R.C. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques.* New Delhi: New Age Publishers Limited.

Kumar, R. (1999). *Research Methodology: A step-by-step guide for beginners.* New Delhi: SAGE Publications India Pvt Ltd.

Macquarrie, J. (1972). *Existentialism.* London: Hutchinson of London.

Makoyo, M. S. (2014). "A critique of Christian Education for Self Reliance in Kenya in light of Existentialism". Tasnifu ya uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Mayaka, G. (1991). "Ukengeushi wa Wasomi katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi. Tasnifu ya Uzamili". Chuo kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Migiro, N. (2012). "Motifu za Usufi katika Utenzi wa 'Kiokozi cha Banati'". Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Mose, E. (2005). “Taashira za Kifo katika Tamthilia za ‘Mukwava wa Uhehe’, Amezidi, Kilio Cha Haki’ na ‘Visiki’”. Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Mungah, C. (1999). “Dhana ya Maisha katika Novela mbili za Euphrase Kezilahabi: ‘Nagona’ na ‘Mzingile’”. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Musau, P. (1995). Kezilahabi na Thomas Hardy: Sarafu kwa ya Pili? Katika Kioo *cha Lugha, juzuu 1, Na. 2*. TUKI. Kur. 62-66

Mwanjala, S.M. (2011). “Dhana ya Maisha Katika Riwaya Mbili Za E. Kezilahabi”. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa).

Nasimiyu, M. C. (2016). “Athari ya Mazingira ya Kihistoria na Kijamii katika Uwasilishaji wa Maudhui ya Dhifa (E. Kezilahabi)”. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Nanjala, W. C. (2015). “Mgongano wa Tamaduni katika Hadithi Fupi za Kiswahili”. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Nayak S. K (2018). Pedagogical Suicide, Philosophy of Nihilism, Absurdity and Existentialism in Albert Camus’ The Myth of Sisyphus and Its Impact on Post-independence Odia Literarure. Katika *IJTSRD*. Volume 2 issue 3, Pg 812-829

Nietzsche, F. (1974). *The gay science*. (W., Kaufmann, Trans). NY: Vintage books. Randon Hse, Inc. Original work published in 1882.

Nietzsche, F. (2003). *The Genealogy of Morals*. (Translated by Horace Barnett Samuel).

New York: Courier Dover Publications. Original work published in 1887.

Njogu, G. W. (2014). “Fumbo la Uhai na Kifo katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi

‘Nagona’ na ‘Mzingile’”. Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Njogu, K. (1997). *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*. Nairobi: Nairobi University Press

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation Ltd.

Ohly, R. (1981). *Aggressive Prose.* Dar es Salaam: TUKI.

Osore, M. (2008). “Defamiliarization in the Novels of Euphrase Kezilahabi and Said Ahmed Mohamed”. Tasnifu ya uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Powell, R., & Connaway, S. (2004). *Basic Research Methods for Librarians* (5th Ed). London: Sage Publications Inc.

Poyi, C. J. & Wandera-Simwa, S. (2020). Usawiri wa ukombozi katika diwani ya Euphrase Kezilahabi ya ‘Kichomi’: mtazamo wa kidhanaishi. Katika *Editon Cons. J. Kiswahili,* 2(1), 110-109.

Poyi, C. J. (2021). “Uchanganuzi wa Suala la Ubwege katika Diwani ya Kichomi”. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Laikipia (Haijachapishwa).

Rettová, A. (2016). Existentialism and Swahili Literature. Katika *Abdilatif abdalla: Poet in Politics.* Dar-es-Salam. Mkuki na Nyota, 109-122.

Rono, P. (2013). “Uhakiki wa Kimaudhui na Kifani wa Kidagaa Kimemwozea”. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Ruhumbika, G. (1983). Tafsiri za Fasihi za Kigeni katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili. Katika *Fasihi: Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III.* Dar es Salaam: TUKI.

Sartre, J.-P. (1956). *No Exit, and three other plays*. New York: Vintage Books.

Sartre, J-P. (1965). *Being and Nothingness* (B. Hazel Trans). New York. Citadel Press. Original work published in 1945.

Sartre, J-P. (2007). *Existentialism is humanism.* (M., Carol Trans). New Haven: Yale University Press. Original work published in 1945.

Searle, C. (2012). *Researching Society and Culture.* London: Sage Publications Ltd.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi.* Dar es Salam: Press and Publicity Center.

Shakespeare, W. & Durband, A. (1985). *Romeo and Juliet*. Hauppage, NY: Barron's.

Tariq, U. (2017). "Exploring Existentialism in Postcolonial Literature through Salman Rushdie's 'Midnight's Children'". Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Greenwich- bewa la Karachi, Pakistani (Haijachapishwa).

Vilem, R. (2007). Kazimoto and Meursault: "Brothers" in despair and loneliness. Comparing Kezilahabi's Kichwamaji and Camus' L'etranger. *Swahili Forum.* 135-151.

Wafula, R. (1999). Mtindo wa Majaribio katika *Amezidi. Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, R. & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. (1997). Contemtus Mundi and Carpe Diem Motifs in Kezilahabi's works. Katika *Kiswahili juzuu 60.* Dar es-salaam. TUKI. UK. 15-24

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*, Nairobi: Phoenix Publishers limited.

Wamitila, K. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Publications Limited.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia,* Nairobi: Focus publications Ltd.

Wanjala, C. (1980). *For Home and Freedom*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

MAREJELEO YA MTANDAONI

Riwaya. (2019, March 26). In *Wikipedia.* https://sw.wikipedia.org/wiki/Riwaya

Existentialism. (2020, May 12). In *Wikipedia.* https://en.wikipedia.org/wiki/Existentialism

Meaning of life. (2020, May 12). In *Wikipedia*.https://en.wikipedia.org/wiki/Meaning of_life

VIAMBATISHO

Cheti cha maadili ya utafiti

NACOSTI ACCREDITED

ERC/MA/006/2020

Pwani UNIVERSITY

ETHICS REVIEW COMMITTEE

ACCREDITTED BY THE NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION (NACOSTI, KENYA)

CERTIFICATE OF ETHICAL APPROVAL

THIS IS TO CERTIFY THAT THE PROPOSAL SUBMITTED BY:

ABDULAH M. CHIMERAH

REFERENCE NO:
ERC/MA/006/2020

ENTITLED:
Uchanganuzi wa udhanaishi katika wahusika na uhusika wao katika riwaya za Thomas Kamugisha: Kitu Kidogo tu na harusi ya wendawazimu

TO BE UNDERTAKEN AT:
KILIFI COUNTY, KENYA

FOR THE PERIOD
FROM: 30/11/2020 TO: 29/11/2021

HAS BEEN **APPROVED** BY THE ETHICS REVIEW COMMITTEE

AT ITS SITTING HELD AT PWANI UNIVERSITY, KENYA

ON THE 27/11/2020

CHAIRMAN | SECRETARY | LAY MEMBER

Pwani UNIVERSITY
Ethics Review Committee,
Pwani University, www.pu.ac.ke, email: t.rewe@pu.ac.ke, j.ndiso@pu.ac.ke tell: 0719 182218, 0720785791
The ERC, Giving Integrity to Research for Sustainable Development